# KUCHANGANUA MAKOSA YA KIMOFOFONOLOJIA KATIKA KAZI ANDISHI ZA KISWAHILI MIONGONI MWA WANAFUNZI WENYE ASILI YA LUGHA YA KIKUYU KATIKA SHULE ZA UPILI: KAHURO, MURANG'A

**JULIET ASWANI MUKHWANA**

**Tasnifu hii Imetolewa Kutimiza Baadhi ya Mahitaji ya Shahada ya Uzamili Katika Chuo Kikuu Cha Mount Kenya**

**Mei, 2025**

Mount Kenya University

# UNGAMO NA IDHINI

## UNGAMO NA IDHINI

### UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu binafsi na haijawahi kutolewa kwa nia ya utuzwaji wowote kwenye taasisi nyingine ya elimu ya juu.

Jina: Juliet Aswani Mukhwana

Nambari ya usajili: MAKI/2023/47525

Sahihi__________ Tarehe: 20/05/2025

### IDHINI

Tasnifu hii ilitolewa kwa nia ya kutimiza sehemu ya matakwa ya utuzwaji wa shahada ya uzamili katika Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Mount Kenya kwa idhinisho langu kama msimamizi ambaye aliteuliwa rasmi na chuo kikuu kuisimamia.

Msimamizi

Daktari Rose Kawira Kamwara

Chuo Kikuu Cha Mount Kenya

Sahihi------------------------ Tarehe 20/05/2025

# TABARUKU

Kwa wanangu wapendwa Archilles Hazen na Darrel Mukhwana kwa kuvumilia na kunipa sababu na motisha ya kujitolea kwa bidii.

Mount Kenya University

Mount Kenya University

## SHUKRANI

Fadhila zangu za dhati ni kwa Arabuka kwa kunijalia uwezo na siha njema katika kupata shahada hii ya uzamili katika Kiswahili.

Aidha, namshukuru msimamizi wangu Daktari Rose Kawira Kamwara kwa uongozi na uelekezaji wake kwa njia ya upendo. Ni kwa ajili ya maelekezi yake ndiposa najivunia ufanisi huu.

Siwezi kuwasahau wahadhiri wangu wote; Daktari Rose Kawira Kamwara, Daktari Jackline Murimi, Daktari Aggrey Wanyama, Profesa Kennedy Mutundu na Daktari Maroko walionifunza, hasa wale wa idara ya Kiswahili.

Shukrani za dhati pia ziwaendee wanagenzi wenzangu ambao tumepambana nao kwenye mwendo huu wa kupata shahada ya uzamili kwa vile walinihimiza na kunisaidia. Hawa ni pamoja na Amos, Lynet, Stella, Kariuki na wengineo.

Shukrani za dhati kwa dadangu Melissa Achango kwa kuchukua majukumu ya ulezi wa wanangu wakati nilikuwa chuoni.

Kwenu nyote ambao mlishiriki katika kuhakikisha kazi hii imefanikiwa pokeeni shukrani za dhati.

## IKISIRI

Lugha yoyote ya kwanza kwa kawaida huwa na athari wakati wa harakati za kufahamiana na lugha nyingine. Hiki ndicho chanzo cha ukosaji wa Kiisimu kati ya wanagenzi wanaojifunza lugha ya pili. Hivyo, wanagenzi wengi wa lugha ya Kiswahili hawajaachwa nyuma. Wengi wao wameathirika si haba.Wao hujikuta kwenye makosa yaya haya kwa kuhamisha ruwaza ya Kiisimu ya lugha wanayoimiliki hadi kwa lugha ya pili ambayo ni Kiswahili. Mada ya uchunguzi huu ni uchanganuzi wa makosa yanayohusiana na mofofonolojia kwenye kazi andishi za Kiswahili miongoni mwa wanagenzi wenye asili ya lugha ya Kikuyu katika shule za sekondari: Kahuro, jimbo la Murang’a. Malengo mahususi ni kubainisha ukosaji wa kifonolojia kwenye kazi andishi za Kiswahili miongoni mwa wanagenzi hawa katika jitihada zao za kujifunza lugha ya Kiswahili, kutambua ukosaji wa kimofolojia kwenye kazi andishi za Kiswahili ambao unafanywa na wanagenzi hawa katika ujifunzaji wao wa lugha ya Kiswahili, kubaini asili ya ukosaji wa umofofonolojia katika kazi andishi za Kiswahili katika juhudi za ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili na kutathmini namna ya kurekebisha ukosaji wa kimofofonolojia kwenye kazi andishi za lugha ya Kiswahili kati ya wanagenzi hawa. Ili kufikia malengo haya, mtafiti alijikita kwenye wanagenzi wa shule za sekondari za kutwa katika jimbo dogo la Kahuro lililo katika jimbo la Murang’a. Pia, mtafiti alifanya utafiti maktabani kuchunguza hali ya makosa kwenye lugha tofauti tofauti na pia vyanzo vya makosa na jinsi ya kurekebisha makosa hayo katika lugha. Data ambayo ilikusanywa kwenye uchunguzi huu ni ya aina ya kithamano ambapo makosa ya kifonolojia na kimofolojia katika insha yalibainishwa na kuchanganuliwa kwa kutumia maelezo kulingana na vigezo vya Nadharia ya Uchanganuzi Makosa iliyoanzishwa na mtaalamu Corder katika mwaka wa 1960. Uchunguzi huu ni wa aina ya kimaelezo na ulitekelezwa nyanjani na pia katika maktaba. Sampuli ya uchunguzi huu ilichaguliwa kwa kutumia njia za kimakusudi. Sababu ya kutumia mbinu hii ni kuwa ililenga shule za upili za kutwa katika jimbo dogo la Kahuro, kaunti ya Murang’a ili kupata data kuhusu ukosaji wa kimofofonolojia unaofanywa na wanagenzi wa shule za sekondari katika kazi andishi za Kiswahili. Baada ya data kukusanywa ilichanganuliwa kwa kutumia mbinu ya kimaelezo kwa mujibu wa mihimili ya Nadharia ya Uchanganuzi Makosa na pia madhumuni ya utafiti huu kama yalivyotajwa hapo juu. Kwenye sura ya kwanza, tumeangazia usuli wa mada, suala la uchunguzi, madhumuni ya utafiti, maswali ya uchunguzi, sababu za kuchagua mada, umuhimu wa uchunguzi pamoja na kufafanua istilahi muhimu. Katika sura ya pili tumeangazia

Mount Kenya University

mwauo wa maandishi na misingi ya nadharia ambayo iliongoza utatifi. Katika sura ya tatu, mbinu za uchunguzi, mahali pa uchunguzi, uteuzi wa sampuli, vifaa vya utafiti, kukusanya data, kuchanganua data na maadili ya utafiti yameshughulikiwa. Sura ya nne nayo imeshughulikia maelezo ya kimsingi kuhusu fonolojia, mofolojia mofofonolojia, mifanyiko ya kimofofonolojia, sauti za Kiswahili na Kikuyu, uwasilishaji na uchanganuzi wa data iliyokusanywa ilhali ile ya mwisho inahusu muhtasari, matokeo na pia mapendekezo ya utafiti huu.

## ABSTRACT

Any first language typically has an impact during the process of familiarizing oneself with another language. This is the source of linguistic errors among students who are learning a second language. Thus, many learners of the Kiswahili language have not been left behind as many of them have been significantly affected. They often find themselves making these mistakes by transferring the linguistic patterns of their original language to the second language which is Kiswahili in this case. The topic of this study is to analyze mistakes related to morphophonology in written Kiswahili work among students of Kikuyu language background in secondary schools: Kahuro, Murang'a. Specific objectives of the research are; to recognize phonological errors in Kiswahili written work among these learners in their efforts to learn Kiswahili language, to recognize morphological mistakes in Kiswahili written work made by these learners in their Kiswahili language learning process, to determine the reasons for these morphophonological mistakes in Kiswahili written work as they strive to learn Kiswahili language and to evaluate morphophonological errors in Kiswahili written work among these learners. To achieve these objectives, the researcher focused on students from day secondary schools in Kahuro sub-county located in Murang'a County. Additionally, the researcher conducted a library-based study to examine the concept of errors in various languages, their causes and ways of correcting these errors. The data collected in this study is qualitative, where phonological and morphological errors in students' compositions were identified and analyzed descriptively based on the theory of Error Analysis introduced by Corder in 1960. This study is descriptive and was carried out both in the field and in the library. The sample of the study was selected using purposive sampling techniques because it focused on day secondary schools in Kahuro sub-county, Murang'a County to obtain data on morphophonological mistakes made by secondary school students in their Kiswahili written work. After data collection, it was analyzed descriptively rooted on the principles of Error Analysis Theory and also on the research objectives mentioned above. The first chapter highlights the background of the study, the study problem, study objectives, research questions and why we choose the topic, the importance of the study and definition of key terms. Chapter two focusses on review of literature and the theoretical framework which guided this research. In chapter three, methods of research, the area of study, sample selection, research instruments, collection of data, analysis of data and research ethics have been discussed. Chapter four presents a brief description of phonology, morphology, morphophonology, morphophonological processes, Kiswahili and

Mount Kenya University

Kikuyu phonemes and analyzes the collected data while the final chapter includes a summary, results and recommendations of this study.

Mount Kenya University

# ORODHA YA YALIYOMO


**UNGAMO NA IDHINI** ....... ii
**UNGAMO** ....... Error! Bookmark not defined.
**TABARUKU** ....... ii
**SHUKRANI** ....... iv
**IKISIRI** ....... v
**ABSTRACT** ....... vi
**SURA YA KWANZA** ....... 1
**MISINGI YA UTAFIT1** ....... 1
**1.0Utangulizi** ....... 1
**1.1 Usuli wa mada** ....... 1
**1.2 Suala la utafiti** ....... 4
**1.3 Madhumuni ya utafiti** ....... 5
**1.3.1 Lengo kuu** ....... 5
**1.3.2 Madhumuni mahususi** ....... 5
**1.4 Maswali ya utafiti** ....... 6
**1.5 Sababu za Kuchagua Mada** ....... 6
**1.6 Umuhimu wa Utafiti** ....... 7
**1.7 Upeo na Mipaka** ....... 7
**1.8 Ufafanuzi wa Istilahi Muhimu** ....... 8
**1.9 Hitimisho** ....... 9
**SURA YA PILI** ....... 10
**MAPITIO YA MAANDIKO NA MISINGI YA NADHARIA** ....... 10
**2.0 Utangulizi** ....... 10
**2.1 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada** ....... 10
**2.2 Misingi ya Nadharia** ....... 17
**2.3 Hitimisho** ....... 21
**SURA YA TATU** ....... 22
**MBINU ZA UTAFITI** ....... 22
**3.0 Utangulizi** ....... 22
**3.1 Mbinu za Utafiti** ....... 22
**3.2 Mahali pa Utafiti** ....... 22


Mount Kenya University

3.3 Uteuzi wa sampuli ........ 24
3.4 Vifaa vya Utafiti ........ 24
3.4.1 Kalamu na Shajara ........ 24
3.4.2 Tovuti na Kompyuta ........ 25
3.4.3 Insha za Wanafunzi ........ 25
3.5 Kukusanya Data ........ 25
3.6 Uchanganuzi wa Data ........ 26
3.7 Maadili ya Utafiti ........ 26
3.8 Hitimisho ........ 26
SURA YA NNE ........ 27
MATOKEO YA UTAFITI NA UCHANGANUZI ........ 27
4.0Utangulizi ........ 27
4.1 Kipengele cha Fonolojia ........ 29
4.1.1 Kipengele cha fonimu ........ 32
4.1.2 Sifa za Fonimu ........ 32
4.2 Utanzu wa Fonetiki ........ 33
4.2.1 Fasili ya fonetiki ........ 33
4.2.2 Matawi ya Fonetiki ........ 33
4.3 Uhusiano Uliopo Baina ya Fonetiki na Fonolojia ........ 34
4.4 Kipengele cha Mofolojia ........ 36
4.4.1 Sura za Mofolojia ........ 37
4.4.2 Vipera vya Mofolojia ........ 37
4.4.3 Sifa za Mofimu ........ 37
4.5 Uhusiano uliopo kati ya Fonolojia na Mofolojia ........ 38
4.6 Dhana ya Mofofonolojia ........ 39
4.7 Sauti za lugha ya Kiswahili na lugha ya Kikuyu ........ 39
4.7.1 Sauti za lugha ya Kiswahili ........ 40
4.7.2 Sauti za lugha ya Kikuyu ........ 48
4.8 Miundo ya silabi za Kiswahili na zile za Kikuyu ........ 51
4.8.1 Miundo ya silabi za Kiswahili ........ 51
4.8.2 Miundo ya silabi za lugha ya Kikuyu ........ 53
4.9 Mifanyiko/kanuni za kimofofonolojia katika lugha ya Kiswahili na ile ya Kikuyu ........ 53
4.9. 1 Mikondo ya kimofofonolojia katika lugha ya Kiswahili ........ 54
4.9.2 Mikondo ya Kimofofonolojia ya lugha ya Kikuyu ........ 60

Mount Kenya University

4.10 Kipengele Cha Makosa....64
4.11 Makosa ya Kifonolojia Katika Lugha ya Kiswahili....65
4.12 Makosa ya kimofolojia....83
4.13 Utathmini wa kiwango cha makosa....97
4.13.1 Makundi na kiwango cha makosa....97
4.14 Sababu za wanagenzi wa shule za upili wenye asili ya lugha ya Kikikuyu kufanya makosa katika kazi andishi za Kiswahili....99
4.15 Mbinu za kurekebisha makosa ya kimofofonolojia katika kazi andishi za Kiswahili miongoni mwa wanagenzi wenye asili ya lugha ya Kikikuyu....100
SURA YA TANO....107
MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO....107
5.0Utangulizi....107
5.1Muhtasari....107
5.2 Hitimisho....113
5.3 Mapendekezo....115
MAREJELEO....117
VIAMBATISHO....124
Kiambatisho 1: Mada ya insha....124
Kiambatisho 2: Mifano ya insha....124
Kiambatisho 3: Idhini kutoka idara ya maadili ya utafiti....126
Kiambatisho 4: Idhini ya utambulisho....127
Kiambatisho 5: Cheti cha idhini ya kufanya Utafiti....128
Kiambatisho 6: Fomu ya idhini ya kushiriki utafiti....129
Kiambatisho 7: Ripoti ya Turntin....132
Kiambatisho 8: Ramani ya Kaunti ya Murang'a....134
Kiambatisho 9: Ramani ya Kaunti ndogo ya Kahuro....135

Mount Kenya University

## ORODHA YA MAJEDWALI


**Jedwali 4.7.1: Mukhtasari wa sifa za konsonanti** ..... 47
**Jedwali 4.7.2: Mukhtasari wa sifa irabu za Kikuyu** ..... 49
**Jedwali 4.7.3:Konsonanti za lugha ya Kikuyu** ..... 51
**Jedwali 4.11.1:Mifano ya maneno yaliyochopeka fonimu /u/** ..... 66
**Jedwali 4.11.2:Mifano ya maneno aliyochopeka fonimu /i/** ..... 67
**Jedwali 4.11.3:Mfano wa neno lililochopekwa fonimu /h/** ..... 68
**Jedwali 4.11.4:Mifano ya maneno yaliyochopekwa kiyeyusho** ..... 68
**Jedwali 4.11.5: Mifano ya maneno yaliyodondoshwa fonimu /h/** ..... 69
**Jedwali 4.11.6:Mifano ya maneno yaliyodondoshwa irabu /a/** ..... 70
**Jedwali 4.11.7:Mifano ya maneno yaliyodondoshwa fonimu/i/** ..... 72
**Jedwali 4.11.8:Mifano ya maneno yaliyotumia fonimu /r/ badala ya /l/** ..... 72
**Jedwali 4.11.9:Mifano ya maneno yaliyotumia /l/ badala ya /r/** ..... 74
**Jedwali 4.11.10: Mifano ya maneno yaliyotumia /s/ badala ya /sh/** ..... 75
**Jedwali 4.11.11: Mifano ya maneno yaliyotumia /sh/ badala ya /s/** ..... 76
**Jedwali 4.11.12: Mifano ya maneno yaliyotumia /d/ badala ya /nd/** ..... 76
**Jedwali 4.11.13: Mifano ya maneno yaliyotumia /nd/ badala ya /d/** ..... 77
**Jedwali 4.11.14: Mifano ya maneno yaliyotumiwa /b/ badala ya /mb/** ..... 78
**Jedwali 4.11.15: Mifano ya maneno yaliyotumia fonimu /mb/ badala ya /b/** ..... 79
**Jedwali 4.11.16: Mifano ya maneno yaliyotumia /g/ badala ya /ng/** ..... 80
**Jedwali 4.11.17: Mifano ya maneno yaliyotumia /ng/ mahali pa /g/** ..... 81
**Jedwali 4.11.18: Mifano ya maneno yaliyotumia /nj/ badala /j/** ..... 82
**Jedwali 4.11.19:Mifano ya maneno yaliyotumia /s/ badala ya /z/** ..... 82
**Jedwali 4.11.20: Mifano ya maneno yaliyotumia /sh/ badala ya /ch/** ..... 83
**Jedwali 4.12.1: Mifano ya maneno yaliyodondoshwa irabu /a/** ..... 84
**Jedwali 4.12.2: Mifano ya maneno yaliyodondoshwa irabu /e/** ..... 85
**Jedwali 4.12.3: Mifano ya maneno yaliyodondoshwa irabu /i/** ..... 85
**Jedwali 4.12.4: Mifano ya maneno yaliyodondoshwa /h/** ..... 86
**Jedwali 4.12.5: Mifano ya maneno yaliyodondoshwa /w/** ..... 86
**Jedwali 4.12.6: Mifano ya maneno yaliyodondoshwa /y/** ..... 87
**Jedwali 4.12.7: Mfano wa neno lililodondoshwa /u/** ..... 87
**Jedwali 4.12.8: Mifano ya maneno yaliyochopekwa /ma/** ..... 88
**Jedwali 4.12.9: Mifano ya maneno yaliyochopekwa /ku/** ..... 89
**Jedwali 4.12.10: Mifano ya maneno yaliyochopekwa /ni/** ..... 89
**Jedwali 4.12.11: Mfano wa neno ambalo lilichopekwa /m/** ..... 90
**Jedwali 4.12.12: Mfano wa neno lililochopekwa viambishi vya wingi** ..... 90
**Jedwali 4.12.13: Mifano ya maneno yaliyoongezewa kiambishi tamati /ng/** ..... 91
**Jedwali 4.12.14 : Mifano ya maneno yaliyotumia /l/ badala ya /r/** ..... 91
**Jedwali 4.12.15: Mifano ya maneno yaliyotumia /th/ badala ya /dh/** ..... 92
**Jedwali 4.12.16: Mifano ya maneno yaliyotumia /ka/ badala ya /ki/** ..... 93
**Jedwali 4.12.17: Mfano wa neno lililotumia /ng/ badala ya /ng'/** ..... 93
**Jedwali 4.12.18: Mfano wa neno lililotumia /c/ badala ya /z/** ..... 94
**Jedwali 4.12.19: Mifano ya maneno yaliyotumia irabu badala ya kiyeyusho.** ..... 94


Mount Kenya University

**Jedwali 4.12.20: Mifano ya maneno yaliyobadilishwa mpangilio wa vipashio**.................................... 95
Jedwali 4.12.21: **Mifano ya maneno yaliyobadilishwa mofu**.................................................................. 96
**Jedwali 4.12.22: Mfano wa neno liliIonyambuliwa vibaya**.................................................................... 96
**Jedwali 4.13.1: Kiwango cha makosa ya kifonolojia** .............................................................................. 97
**Jedwali 4.13.2: Kiwango cha makosa ya kimofolojia** ............................................................................. 98
**Jedwali 4.13.3: Muhtasari wa jumla ya makosa ya kimofofonolojia** ................................................... 98

Mount Kenya University

# ORODHA YA MICHORO

**Mchoro 1:Irabu za Kiswahili**........................................................................................................44
**Mchoro 2:Irabu za lugha ya kikuyu**...........................................................................................48

Mount Kenya University

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.0Utangulizi

Katika sehemu hii tumeangazia dhana muhimu za utafiti. Miongoni mwa dhana zilizojadiliwa ni usuli wa mada, tatizo la uchunguzi, maswali ya uchunguzi pamoja na madhumuni ya uchunguzi, sababu za uchaguzi wa mada, na pia upeo na mipaka ya uchunguzi.

## 1.1 Usuli wa Mada

Dhana ya makosa katika lugha ni jambo ambalo limeshughulikiwa sana na wanaisimu na watafiti mbalimbali (Richard, 1971). Makosa ya lugha yanarejelea hali ambapo mtu hukosa kufuata kanuni za lugha hiyo kwa kupungukiwa na ustadi katika lugha inayolengwa. Aghalabu, makosa ya lugha hutafitiwa miongoni mwa watu ambao wanazungumza lugha zaidi ya moja.Wazungumzaji hawa huweza kuingiza ujuzi wa lugha moja hadi lugha hiyo inayokusudiwa. Richard (1971) anadai kuwa makosa haya huingilia ujuaji wa lugha nyingine katika vipengele vya ufonolojia, umofolojia na usintaksia. Anadai kwamba makosa pia huweza kusababishwa na mzungumzaji kushindwa na kuzingatia sheria na utaratibu wa lugha ya pili nyakati za kuandika au kuzungumza.

Dhana hii imewashughulisha watafiti pamoja na wanaisimu wengi wanaofanya tafiti kuhusu mapungufu yanayohusishwa na wanagenzi wanapojaribu kujifundisha lugha nyingine. Vilevile, wanachunguza vyanzo vya makosa ya kifonolojia na kimofolojia (Corder, 1971).

Lugha ya Kiswahili ni kati ya zile lugha zilizohusishwa na Wabantu kama ilivyo ile ya Kikuyu. Ni lugha ambayo inazungumzwa Barani Afrika hususan ile ya ukanda wa Mashariki (Ali, 2013). Kiswahili hufungamanishwa kwa kiwango kikubwa na Wabantu. Ni lugha inayoainishwa kwenye kundi la kumi. Huhusishwa na watu wa ukanda wa Pwani ya eneo la Mashariki ila lugha hii

ilisambaa hadi bara na nchi zingine (Nchimbi, 2008). Kulingana na Odeo na Maina (2008) lugha hii ya Kiswahili ni lugha yenye lahaja nyingi na makubaliano kamili hayajatolewa kuhusu mipaka na idadi ya vilugha vya Kiswahili. Kati ya lahaja hizi ni lahaja ya Kiunguja iliyoteuliwa kuisanifisha lugha hii ya Kiswahili. Kupitia usanifishaji huu, kuna haja ya kujifunza Kiswahili Sanifu ili kuwezesha mawasiliano miongoni mwa watumizi wake mbalimbali.

Lugha ya Kiswahili imetumika nchini Kenya sana tangu enzi za ukoloni kufanikisha mawasiliano. Ni lugha ambayo ilipewa dhima ya kufundishwa na kutahiniwa katika viwango vya kitaifa kwenye shule za msingi na za sekondari katika nchi ya Kenya. Isitoshe, somo la Kiswahili ni mojawapo ya masomo ya lazima kufanywa na wanagenzi wa mitalaa ya 8.4.4 na pia mtalaa mpya wa Kiumilisi. Hivyo, kila mwanagenzi anapaswa kuipa lugha hii hadhi inayostahili sio tu kwa kupita mtihani ila pia kwa shughuli nyingine zinapohitaji umaarufu wake. Kwa ajili hii, Kiswahili ikiwa lugha ya pili hufunzwa na kutahiniwa sio nchini Kenya pekee bali pia kwenye nchi mbalimbali za Afrika ya Mashariki. Mbali na kutumika katika uwanja wa elimu, Kiswahili kama lugha ya mawasiliano imepitishwa na kuidhinishwa kikatiba kama lugha ya taifa na pia ya mawasiliano rasmi nchini Kenya na Tanzania. Pia, lugha ya Kiswahili imetambulika kama lugha ya kimataifa inayotumika kama kifaa cha mawasiliano kati ya mataifa mbalimbali. Isitoshe, Kiswahili ni lugha inayotumiwa katika tasnia za kisiasa, biashara, kisheria na katika vyombo vya habari. Hadhi ya lugha hii imeiwezesha kufundishwa katika vyuo vingi katika bara la Afrika, Marekani, Asia na Ulaya. Nchimbi (2008) anasema kuwa usanifishaji wa Kiswahili ulitokana na kuondolewa kwa utofauti wa kimatamshi, msamiati na kimaandishi kwenye hii lugha. Shughuli hii ilitekelezwa na kamati ya lugha ya Kiswahili ya Afrika Mashariki (KKAM) kwa kupendekeza lahaja ya Kiunguja katika kusanifisha Kiswahili. Jambo hili liliwezesha kuwapo kwa mfumo mmoja wa maandishi, matamshi na uundaji wa msamiati.

Mount Kenya University

Kikuyu kama lugha ya Wabantu huwa inazungumzwa na watu wa jamii ya Wakikuyu inayopatikana katika eneo la kati ya nchi ya Kenya.

Suala la makosa ya kifonolojia na kimofolojia kati ya wanagenzi ambao wanajifunza Kiswahili kama lugha yao pili ni suala linalowashughulisha waandishi, watafiti na wasomi wa masuala ya Kiisimu ulimwenguni kote. Wengi huashiria kuchunguza makosa yanayofanywa na wanafunzi, chanzo chake na namna ya kuyatatua. Jambo hili ndilo lililochochea kuchunguza ukosaji ya kifonolojia na kimofolojia kati ya wanagenzi wa somo la Kiswahili katika shule za upili katika kaunti ndogo ya Kahuro, kaunti ya Murang'a katika maandishi. Ijapokuwa lugha ya kwanza ya wanagenzi ni Kikuyu, wanafunzi wengi Wakikuyu hutumia lugha ya Kiswahili sambamba na Kikuyu katika mandhari ya nyumbani. Wakati mwingine wanafunzi wanaojifunza lugha ya Kiswahili hutatizika kimatamshi, kimaandishi na kimsamiati wanapokitumia. Ellis (1997) anafafanua kosa katika lugha kama mfumo potofu kwa wanaojifunza lugha unaohusiana na sarufi, msamiati au matamshi ya lugha hiyo. Hata hivyo, Muftah (2016) anadai kuwa kosa katika kujifunza lugha ya pili ni sehemu muhimu katika ujifunzaji wa lugha hiyo. Gass & Selinker (2001) wanashikilia kuwa makosa ya ujifunzaji lugha huashiria matatizo waliyo nayo wanaojifunza lugha kuhusiana na vipengele fulani vya lugha hiyo mathalani, sarufi, matamshi na msamiati. Kwa kuzingatia haya uchunguzi wetu ulichunguza chanzo cha ukosaji wa kimofofonolojia kwenye kazi andishi za Kiswahili kati ya wanagenzi Wakikuyu katika shule za sekondari wanaojifunza lugha ya Kiswahili Sanifu Kahuro, kaunti ya Murang'a nchini Kenya. Katika eneo hili, wakaazi wengi huzungumza Kikuyu kama lugha ya mwanzo na eneo hili lina shule za upili tofauti tofauti ambapo baadhi ni za bweni na zingine ni za kutwa. Shule za bweni husajili wanafunzi kutoka maeneo mengine na huwa na lugha za kwanza tofauti lakini shule za kutwa huwa na wanafunzi kutoka maeneo ya karibu na kwa hivyo, lugha yao ya awali huwa ni lugha ya Kikuyu. Imebainika kwamba

wanagenzi wengi ambao ni wa asili ya jamii ya Kikuyu hufanya makosa wanapoandika Kiswahili na ndiposa utafiti huu umebainisha na kutambua makosa haya ya kifonolojia na kimofolojia ambayo hutokea kwenye kazi andishi za wanagenzi wa lugha ya Kiswahili wa skuli za sekondari wenye asili ya lugha ya Kikuyu. Utafiti huu pia umebainisha vyanzo vya ukosaji unaohusishwa na mofofonolojia katika kazi andishi za Kiswahili kati ya wanagenzi wa shule za sekondari wenye asili ya lugha ya Kikuyu na jinsi ya kurekebisha makosa hayo ya kimofofonolojia katika jitihada zao za kujifunza lugha ya Kiswahili.

### 1.2 Suala la Utafiti

Huu uchunguzi ulichochewa na utambuzi kwamba wanagenzi wa somo la Kiswahili kwenye shule za sekondari kwenye kaunti ndogo ya Kahuro, jimbo la Murang'a hutekeleza makosa tofauti tofauti kwenye somo hili wanapoandika kazi zao. Ukosaji huu huwa wa kifonolojia, kimofolojia, kisintaksia, kisemantiki na hata kisarufi. Makosa haya huadhibiwa kwenye mitihani ya kitaifa ya kidato cha nne kwenye mtihani wa karatasi la kwanza na la pili na kwa hivyo ikiwa mwanagenzi atadhihirisha makosa mengi, hilo huenda likadidimiza matokeo yake katika somo la Kiswahili.Hivyo, ni bora kutambua makosa haya mapema kwenye shule za sekondari na sababu za ukosaji huo kutokea ili kujaribu kuyarekebisha mapema. Utafiti huu unajihusisha na kuchanganua makosa yanayohusiana na kiwango cha mofofonolojia kwenye kazi andishi za Kiswahili baina ya wanagenzi ambao ni wa asili ya lugha ya Kikuyu kwenye shule za sekondari, jimbo dogo la Kahuro, kaunti ya Murang'a. Uchunguzi huu umedhihirisha na kutambua ukosaji wa kifonolojia na kimofolojia, vyanzo vya makosa ya kimofofonolojia kwenye kazi andishi za Kiswahili baina ya wanagenzi walio na asili ya lugha ya Kikuyu katika shule za sekondari na pia njia za kurekebisha makosa hayo ya kimofofonolojia. Hii ni kwa sababu utafiti uliofanywa maktabani unabainisha kuwa ukosaji wa kimofofonolojia kwenye lugha ya Kiswahili kati ya

wanafunzi wenye asili ya lugha ya Kikuyu na vyanzo vyake katika Kiswahili kati ya wanagenzi walio na asili ya lugha ya Kikuyu haujafanyiwa utafiti wa kutosha. Uchunguzi wa kitaaluma ambao ulifanywa na Wanjala V. na Mwaura F.(2022) kuhusu athari za Kikuyu katika kujifunza Kiswahili Sanifu kwenye shule za sekondari, jimbo dogo la Othaya, kule Nyeri, Kenya haukugusia suala la makosa ya kifonolojia na kimofolojia. Hali hii imeacha pengo la kielimu ambalo litazibwa kupitia utafiti huu ambao unashughulikia uchanganuzi wa makosa ya kimofofonolojia, sababu za ukosaji huu na jinsi ya kurekebisha makosa haya.

## 1.3 Madhumuni ya Utafiti

### 1.3.1 Lengo Kuu

Kuchanganua makosa ya kimofofonolojia katika kazi andishi za Kiswahili miongoni mwa wanafunzi wenye asili ya lugha ya Kikuyu katika shule za upili, Kahuro, Murang'a.

### 1.3.2 Madhumuni Mahususi

Huu uchunguzi una malengo yafuatayo:

1. Kubainisha makosa ya kifonolojia katika kazi andishi za Kiswahili miongoni mwa wanafunzi wa shule za upili wenye asili ya lugha ya Kikuyu katika jitihada zao za kujifunza lugha ya Kiswahili.
2. Kutambua makosa ya kimofolojia katika kazi andishi za Kiswahili yanayofanywa na wanafunzi wa shule za upili wenye asili ya lugha ya Kikuyu katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili.
3. Kubaini vyanzo vya makosa ya kimofofonolojia kwenye kazi andishi za Kiswahili katika juhudi za ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili miongoni mwa wanafunzi wa shule za upili wenye asili ya lugha ya Kikuyu.

Mount Kenya University

4. Kutathmini namna ya kurekebisha makosa ya kimofofonolojia kwenye kazi andishi za lugha ya Kiswahili miongoni mwa wanafunzi wa shule za upili wenye asili ya lugha ya Kikuyu.

### 1.4 Maswali ya Utafiti

Uchunguzi husika umejikita kwenye maswali yafuatayo:

1. Je, makosa ya kifonolojia yanajitokeza vipi kwenye kazi andishi za lugha ya Kiswahili kati ya wanagenzi wa shule za sekondari wenye asili ya lugha Kikuyu?
2. Je, ni makosa yepi ya kimofolojia ambayo yanajitokeza kwenye kazi andishi za lugha ya Kiswahili kati ya wanagenzi wa shule za sekondari wenye asili ya lugha ya Kikuyu?
3. Je, ni nini kinachosababisha makosa ya kimofofonolojia kwenye kazi andishi za lugha ya Kiswahili kati ya wanafunzi wa shule za sekondari wenye asili ya lugha ya Kikuyu?
4. Je, ni vipi ambavyo makosa ya kimofofonolojia kwenye kazi andishi za lugha ya Kiswahili kati ya wanafunzi walio na asili ya lugha ya Kikuyu yanavyoweza kurekebishwa?

### 1.5 Sababu za Kuchagua Mada

Kichocheo cha kuteua mada hii ya utafiti kimsingi ni kuwa, mahitimisho ya watafiti wa awali wa suala la ukosaji wa kimofofonolojia baina ya wanagenzi wanaojifunza lugha ya Kiswahili yanaweza kutiliwa shaka. Kwa upande mwingine, taaluma ya kimofofonolojia haijatafitiwa kwa kushughulikia makosa ya wanagenzi walio na asili ya lugha ya Kikuyu kwenye kujifunza lugha ya Kiswahili. Pia, eneo la Murang'a ambalo linaaminiwa kuwa na Wakikuyu asilia halijazingatiwa katika tafiti za hapo awali.

Mount Kenya University

**1.6 Umuhimu wa Utafiti**

Kupitia kuangazia mada hii, tunaonyesha ukosaji wa kimofofonolojia kwenye kazi andishi za Kiswahili baina ya wanagenzi wenye asili ya lugha ya Kikuyu. Vilevile, tunaangazia vianzo vyake kisha namna ya kuyarekebisha makosa yale. Licha ya hayo, tunatazamia kuwafaidi waandishi wa vitabu vya isimu na lugha katika uandishi wa kazi zao. Isitoshe, tunakusudia kuwapa mshawasha wahakiki na wasomi wa taaluma nyingine za isimu ya lugha ili kuangazia changamoto za kujifunza lugha ya pili kwenye jamii. Fauka ya hayo, uchunguzi wetu utatumiwa kama kumbukumbu muhimu ya marejeleo kwa wachunguzi wa mambo ya kiisimu katika siku za halafu hasa katika uendelezaji wa uchunguzi wao anuwai.

Vilevile, utafiti huu utaweza kuwaongoza washikadau katika sekta ya elimu wanapoandaa mitaala kwani utawapaa mwongozo wa njia na ala za kufundishia lugha ya pili hasa Kiswahili. Kwa upande wa walimu wa Kiswahili, wataweza kung'amua makosa na chanzo chake kwenye ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili. Huu uchunguzi pia unachangia katika kuangazia athari za lugha ya Kikuyu kwenye umilisi na utendaji wa lugha ya Kiswahili. Hili linaafikiwa kwa kubainisha tofauti katika lugha hizi na mwingiliano wazo unaosababisha makosa kwenye lugha ya mwanafunzi.

**1.7 Upeo na Mipaka**

Katika utafiti huu, tunachunguza makosa ya kimofofonolojia yanayojitokeza kwenye kazi andishi za Kiswahili kati ya wanagenzi walio na asili ya lugha ya Kikuyu katika jitihada zao za kujifunza lugha ya Kiswahilii. Watafiti, wahakiki na wasomi katika viwango mbalimbali wameshughulikia ukosaji wa wanafunzi wanapojifunza lugha ya pili. Kati ya wanaisimu hawa ni Corder (1971) anayedai kuwa makosa miongoni mwa wanafunzi hutokea kwenye viwango vya kiisimu hasa fonetiki, semantiki, mofolojia, fonolojia na sintaksia. Utafiti huu unaangazia na kujikita katika

makosa ya kimofofonolojia. Kwa kuwa taaluma za kiisimu hutegemeana na kukamilishana, tuliweza kuhusisha taaluma nyingine za kiisimu kadri ilivyotupasa. Haya yote ni kutuwezesha kuafikia malengo ya uchunguzi huu kwa kuzingatia mihimili ya nadharia ya Uchanganuzi Makosa.

**1.8 Ufafanuzi wa Istilahi Muhimu**

**Fonolojia-** Hii ni sehemu ya sarufi ambayo hujishughulisha na kazi ya kuchambua mfumo wa sauti unaopatikana kwenye lugha (Massamba na wenzake, 2001).

**Isimu-** Hii ni taaluma inayojishughulisha na kazi ya kufafanua, kuchambua na kuchanganua lugha fulani kwa kutumia sayansi fulani (Massamba, 2004).

**Lugha-** Hii ni ruwaza ya sauti zenye unasibu na ambazo hubuniwa na jamii kwa kusudi la mawasiliano miongoni mwao (Massamba, 2004).

**Lugha lengwa**- Hii inamaanisha lugha ambayo mwanafunzi ananuia kujifunza.

**Lugha Rasmi-** Hii ni lugha iliyoteuliwa ili kuendesha shughuli rasmi za taifa fulani.

**Lugha ya kwanza-** Hii ni ile lugha anayojifunza mwana baada ya kuzaliwa kabla ya lugha yoyote nyingine.

**Lugha ya pili-** Hii ni ile lugha anayojifunza mtu baada ya kujifunza lugha ya kwanza.

**Lugha ya Taifa-** Hii ina maana ya lugha ambayo iliteuliwa kuwa kama kitambulizi cha utamaduni na ustaarabu wa taifa kwa jumla.

**Makosa-** Hizi ni kanuni ambazo zinakwenda kinyume na kanuni zilizowekwa.

**Mofofonolojia-**Huu ni utanzu wa isimu ambayo hujishughulisha na uhusiano wa fonolojia na mofolojia.

**Mofolojia**- Hiki ni kipera cha isimu kinachohusika na kuchambua na kuchunguza wa kanuni na mifumo ambayo inahusu upangaji au miundo ya maneno kwenye lugha (Kamusi ya karne ya 21).

**Sarufi**- Hii ni taaluma ambayo hujumuisha viwango vyote vya kuchunguza na kuchanganua Lugha. Viwango hivyo ni vile vya kifonolojia, kimofolojia, kisintaksia na kisemantiki (TUKI, 1990).

**Uchanganuzi makosa**- Huu ni mtazamo ambao hutumiwa kuthibitisha makosa yanayopatikana katika lugha ambayo mwanafunzi anajifunza.

### 1.9 Hitimisho

Kwenye hii sura, tumeangazia usuli wa mada na suala la uchunguzi. Isitoshe, tumeweza kuelezea maswali ya utafiti, madhumuni yake, sababu za uchaguzi wa mada, umuhimu wa uchunguzi na pia upeo na mipaka ya huu uchunguzi pamoja na istilahi muhimu zilizotumika. Sura inayofuata inahusu mwauo wa maandishi na misingi ya nadharia.

Mount Kenya University

# SURA YA PILI

# MAPITIO YA MAANDISHI

## 2.0 Utangulizi

Hii sura imeshughulikia yaliyoandikwa kuhusiana na mada na vilevile misingi ya nadharia ambayo imetumika kwenye uchunguzi husika.

## 2.1 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada

Dhana ya makosa katika lugha ya pili imetafitiwa kwa kipindi kirefu. Kwa mujibu wa Corder (1967), waja hujifundisha lugha nyingine wakiwa tayari na ile asilia waliojifunza na kumudu kanuni na kaida zake wanapojitahidi kuelewa ile ya pili. Corder (keshatajwa) anazidi kudai kuwa utumizi wa kaida za kujifunza lugha nyingine ndio huchochea wazungumzaji kukosea wakati wa kuizungumza au kuiandika lugha ile. Kazi ya Corder ina umuhimu kwa utafiti huu kwani imemsaidia mtafiti kuelewa vyema aina za makosa katika lugha na kinachochoea watu kuyafanya katika maandishi ya wanagenzi walio na asili ya lugha ya Kikuyu wanapoandika Kiswahili.

Wilkins (1972) anakiri kuwa, ukoseaji wa matamshi, sarufi na istilahi yanaweza kujidhihirisha katika lugha za waja ainaaina wanapojifundisha lugha nyingine. Katika uchunguzi wake, mtaalamu huyu anathibitisha kuwa uzungumzi na uandishi wa mwanagenzi anayejifundisha lugha mpya yakichunguzwa, baadhi ya hitilafu hujitokeza katika lugha ile mpya mwanagenzi azungumzapo ama aandikapo huwa yametokana na lugha asilia. Anasema kuwa kiini kikuu cha athari za namna hii ni kule kutolingana kwa mifumo ya lugha mbili. Kazi hii ni ya maana kwa uchunguzi wetu kwa vile inaweka msingi kuhusu suala la hitilafu zinazojitokeza katika harakati za ujifunzaji wa lugha nyingine na kisababishi chake.

Naye Massamba (1986) katika Makala yake anaangazia suala la lugha za mama kuathiri Kiswahili katika mkoa wa Mara, katika nchi ya Tanzania kwa kuzingatia nadharia ya Uchanganuzi Makosa. Kwenye uchunguzi huu, Massamba (ashatajwa) anagundua kuwa lugha asilia na ile ya Kiswahili zinaathiriana. Pia, anachunguza namna lugha asilia zinavyoathiri Kiswahili kwenye viwango vya aina tofauti. Anabaini kuwa uzungumzaji wa mashinani kwenye eneo chunguzwa zinakiathiri Kiswahili kiistilahi, kisarufi na pia kifonolojia. Kazi ya Massamba ina manufaa makuu kwa utafiti huu kwani imemwongoza mtafiti kubainisha makosa ya kimofofonolojia kwenye Kiswahili kati ya wanagenzi walio na asili ya Kikuyu. Kazi yake ina uwiano na yetu kwa vile inatumia nadharia sawia ya yetu. Utofauti unadhihirika pale ambapo kazi yake inashughulikia eneo la Mara, Tanzania na jinsi lugha za kwanza huarithi ujifunzaji wa Kiswahili ilhali yetu imejikita katika kaunti ya Murang'a na kushughulikia makosa ya kimofofonolojia.

Kwa upande mwingine, Mudhune (1994) akifanya utafiti katika kiwango cha uzamili anaangazia ujifundishaji wa kimofosintaksia ya Kiswahili baina ya wanagenzi wa Kidholuo kwa falsafa ya Uchanganuzi Linganuzi. Katika utafiti wake, anabaini kuwa hitilafu nyingi zinazojitokeza katika kazi za wanagenzi husika zinatokana na miathiriano ya lugha yao asilia. Hitilafu zingine zinatokana na kujumlisha sana kaida katika ngeli ya tisa ya lugha ya Kiswahili. Sababu kuu ni kuwa ngeli hii huwa na nomino nyingi kuliko ngeli zingine na vile vile huwa na sifa zenye upekee. Tofauti na utafiti huu, tunatafiti baadhi ya makosa ya kimofofonolojia ambayo hutokea kati ya wanagenzi wa Kiswahili walio na asili ya Kikuyu na visababishi vya makosa haya kwenye kazi za wanafunzi husika. Zaidi ya hayo, tunaongozwa na falsafa ya Uchanganuzi Makosa.

Kimathi (2013) katika uchunguzi wake katika kiwango cha uzamili anachunguza makosa ya kifonolojia kati ya wanagenzi wa jamii ndogo ya Kigembe katika ujifunzaji wa Kiswahili kwa kutumia misingi ya falsafa ya Uchanganuzi Linganuzi. Anadai kuwa makosa mengi

yanayotekelezwa na wanafunzi huhusiana na uchopekaji wa sauti kama vile irabu, viyeyusho au konsonanti katika sehemu ya maneno. Fonimu zisizopatikana kwenye lugha ya Kiigembe kwa mfano /j/, /g/ na /d/ hunazalishwa na kupelekea kuwe na athari kuu kwenye lugha ya Kiswahili, kudondosha konsonanti /h/ kwa sababu fonimu hii haimo kwenye mfumo wa lugha ya Kigembe, ubadilishanaji wa fonimu kama vile kutumia /s/ mahali pa /z/, /b/ mahali pa /v/ na /s/ mahali pa /ch/ kwa sababu fonimu hizi hazipatikani katika lugha asilia. Kazi yake ni muhimu kwa sababu inamsaidia mtafiti kubaini na kuainisha aina ya hitilafu za kifonolojia katika Kiswahili miongoni mwa wanafunzi walio na asili ya lugha ya Kikuyu na sababu za wanafunzi husika kukumbwa na hitilafu za kimatamshi na pia njia za kurekebisha baadhi ya makosa yanayotokea. Uchunguzi wake una utofauti na wetu kwa kuwa tunatumia falsafa ya Uchanganuzi Makosa na kushughulikia makosa ya kimofofonolojia.

Nyaga (2016) kwenye tasnifu yake ya uzamili anachunguza suala la hitilafu za kimatamshi na kimaandishi unaojitokeza wakati wa matumizi kwenye kazi zilizoandikwa za wanagenzi wa sekondari kule Tigania, kaunti ya Meru kwa kutumia falsafa ya Lugha-Kati yake Selinker (1972). Mtafiti huyu anasema kuwa upungufu wa kimaandishi ambao ni pamoja na unazalishaji wa fonimu kama vile vizuiwa na vizuiwa-kwamizwa ghuna, udondoshaji wa sauti kama vile wa fonimu /h/, udondoshaji wa nazali /n/ na /m/, kuchopeka irabu /u/ na pia /i/ na kuchopeka fonimu /h/ pamoja na utumiaji wa sauti mbadala kama vile matumizi ya fonimu /s/ mahali pa /z/, /g/ mahali pa /r/, /b/ mahali pa /v/ na kadhalika. Kazi ya Nyaga imetusaidia kutambua makosa wanayofanya wanagenzi wanaojifunza lugha ya Kiswahili walio na asili ya Kikuyu katika uandishi wao. Pia, msomi huyu anabaini vyanzo vya baadhi ya ukosaji huu. Kulingana naye asili kuu ya ukosaji huu ni lugha ya asilia kuathiri lugha hii na vile vingine ni pamoja na uhawilishaji wa ufundishwaji, ujumlishaji mno, mikakati ya mawasiliano na mikakati ya ujifundishaji. Ingawa utafiti huu unatumia Nadharia

ya Lugha-kati yake Selinker (1972) na utafiti wetu unatumia ile ya Uchanganuzi Makosa, ni uchunguzi ambao ni wa maana sana kwa kazi hii kwani umemwezesha mtafiti kutambua aina za makosa katika Kiswahili kati ya wanagenzi walio na asili ya lugha ya Kikuyu. Pia, umesaidia kubaini na kueleza vyanzo vya makosa husika katika kiwango cha mofofonolojia na jinsi ya kurekebisha makosa hayo.

Mwita (2018) katika tasnifu yake ya uzamili anachunguza makosa ya ufonolojia, umofolojia na mofofonolojia baina ya wanagenzi wa Kiswahili wa vilugha vya Kikuria na wale wa Kidholuo kwa kutumia falsafa ya Uchanganuzi Makosa. Uchunguzi wake unabaini kuwa baadhi ya makosa katika viwango hivi ni pamoja na kuchopeka na kudondosha nazali /n/, /m, fonimu /h, / kiyeyusho /w/ na /j/ miongoni mwa sauti nyinginezo. Pia, inabainika kuwa kuna matumizi ya konsonanti mbadala kama vile /r/ mahali pa /l/, /l/ mahali pa /r/, /s/ mahali pa /z/, /f/ mahali pa /v na nyinginezo mahali pasipofaa. Zaidi ya hayo, mtaalamu huyu anaonyesha wanafunzi wa Kiluo hutumia irabu mbadala kwa sababu Kidholuo huwa na sauti za irabu tisa huku Kiswahili kikiwa na irabu tano. Hatimaye, anabaini sababu kuu za wanafunzi kufanya makosa hayo ni uhawilishaji na upijinishaji wa lugha asilia hadi ile ya pili. Uchunguzi huu ni muhimu sana kwetu kwani umesaidia kubaini mihimili ya Nadharia ya Uchanganuzi Makosa, kubaini aina ya ukosaji unaojikita ndani ya fonolojia na mofolojia na pia kubaini sababu za makosa husika na jinsi ya kurekebisha baadhi ya makosa hayo. Kazi yake uwiano na yetu kwani tunatumia nadharia yiyo hiyo ya Uchanganuzi Makosa na pia inashughulikia makosa ya fonolojia na mofolojia. Utofauti ni kuwa yeye anatafiti lugha za Kidholuo na Kikuria nasi tunatafiti lugha ya Kikuyu.

Naye Frederick (2019) anajishughulisha na uchunguzi wa makosa yanayohusiana na kiwango cha ufonolojia yanayotekelezwa na wakaazi wa jamii ya Kihaya wanaojifundisha Kiswahili kilicho na usanifu: Mfano wake ulitoka Manispaa ya Bukoba katika kiwango cha shahada ya uzamili. Kazi

hii inatumia Nadharia ya Uchanganuzi Makosa iliyohusishwa na Corder (1960). Kazi ya msomi huyu ina umuhimu kwa uchunguzi huu kwa vile umemwezesha mtafiti kutambua mihimili ya nadharia tumizi na namna ya kuitumia kuchanganua makosa ya kimatamshi na kiuandishi katika Kiswahili kati ya wanafunzi wenye asili ya Kikuyu. Aidha, utafiti wa mtaalamu huyu unabaini aina ya ukosaji wa sauti mbadala kama vile sauti /s/ mahali pa /th/, /z/ mahali pa /dh/, /ng/ mahali pa /ng'/, kuchanganya sauti kwa mfano; sauti /a/ na /n/, /l/ na /r/, /dh/ na /th/, /a/ na /w/, udondoshaji wa sauti kama vile /h/ na /u/ na kuchopeka sauti kama vile /h/, kuchopeka wa fonimu /u/ na /i/ kwenye silabi zilizo funge na mofimu za konsonanti tupu. Anabaini kinachosababisha Wahaya kukosea wakati wa ujifundishaji wa Kiswahili kilicho na usanifu ni pamoja na kutolingana kwa mifumo-sauti kwenye lugha hizo, ufundishaji mbovu wa lugha nyingine, wakufunzi kupungukiwa na utaaluma wa ufonetiki wa matamshi na utumikizi wa Kihaya kwa kiasi kikubwa miongoni mwa walimu, wanafunzi na jamii wanazotangamana nayo kwa jumla. Kazi hii inanufaisha hii yetu kwani inasaidia kutambua aina ya makosa yanayohusiana na fonolojia na sababu zake miongoni mwa wanafunzi wa Kiswahili walio na asili ya Kikuyu na pia jinsi ya kurekebisha makosa yaliyotambuliwa. Kazi ya Frederick ni sawia na yetu kwa vile inachunguza makosa ya kifonolojia na pia anatumia falsafa ya Uchanganuzi Makosa. Tofauti ni kuwa anashughulikia jamii ya Kihaya nasi tunashughulika na jamii ya Wakikuyu.

Kalungu (2020) katika tasnifu yake ya uzamili alitafiti kuhusu uchanganuzi makosa katika kiwango cha mofofonolojia katika Kiswahili baina ya wanagenzi walio na asili ya lugha ya Kikamba. Msomi huyu, kwa kutumia nadharia ya Uchanganuzi Makosa anabaini kuwa wanagenzi hutekeleza makosa ya uchopekaji, kudondosha sehemu ya fonimu za Kiswahili na kutumia sauti mbadala. Anahoji kwamba sababu kuu ya makosa haya ni ukosefu wa fonimu husika katika lugha ya Kikamba. Utafiti wake Kalungu unatusaidia kuchunguza iwapo wanagenzi walio na asili ya

lugha ya Kikuyu wanaathirika sawia na wa Kikamba katika uandishi wao. Isitoshe, umetuwezesha kujua vyanzo vya makosa hayo na pia jinsi ya kuyarekebisha. Kazi yake ina uwiano na yetu kwa vile tunashughulikia makosa yayo hayo ya kimofofonolojia kwa kutumia falsafa ya Uchanganuzi Makosa. Tofauti ni kwamba tunajikita kwenye lugha ya Kikuyu naye alijikita kwenye lugha ya Kikamba.

Wanjala na Mwaura (2022) kwenye tasnifu yao ya shahada ya kwanza katika shule ya ualimu walichunguza hali ya lugha ya Kikuyu kuathiri ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili sanifu kwenye shule za sekondari, jimbo dogo la Othaya, Nyeri kwa misingi ya falsafa ya Uchanganuzi Makosa. Wasomi hawa wanabaini wanafunzi kwenye kiwango hiki hudondosha na kuchopeka sauti mbalimbali. Hivyo, lugha ya Kikuyu huathiri matumizi ya Kiswahili Sanifu kati ya wanagenzi walio na asili ya Kikuyu kwenye kazi zao andishi. Kupitia kazi hii, tutaweza kubaini baadhi ya sauti ambazo hudondoshwa na pia kuchopekwa katika Kiswahili pamoja na kubaini sababu za makosa hayo na namna ya kurekebisha baadhi ya makosa husika. Kazi yao ni tofauti na yetu kwani ilijikita huko Othaya, Nyeri na yetu imejikita Kahuro, Murang'a na vilevile yetu inashughulikia makosa ya kimofofonolojia na wala si athari za Kikuyu kwenye ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili Sanifu.

Kanake & Kobia (2023) kwenye makala yao wamechunguza makosa yanayohusiana na ufonolojia kwa wanagenzi wa Kigembe katika ujifundishaji wa Kiswahili. Watafiti hawa wameainisha makosa haya kwa kuzingatia falsafa ya Uchanganuzi Linganuzi. Wasomi hawa wanahoji kuwa ukosaji wa kifonolojia unaofanywa na baadhi ya wanagenzi ni kuchopeka sauti /n/ kwenye maneno ya Kiswahili kwa maneno yaliyo na fonimu /d/, hili hutokana na fonimu /d/ kukosekana kwenye lugha ya Kiigembe. Kwa upande mwingine, sauti /j/ inasemwa kama /nj/ miongoni mwa wanafunzi hawa. Mbali na hayo, wanafunzi hawa hudondosha konsonanti ambapo sauti /h/ hudondoshwa

katika maneno yenye sauti hii. Wanafafanua kiini cha udondoshaji huu kuwa ni kutokuwa kwa sauti hii katika ruwaza ya hii lugha. Isitoshe, kuna ubadilishaji wa fonimu kama vile kutumia /s/ mahali pa /z/ kutumia /b/ mahali pa /v/, kutumia /s/ mahali pa /ch/ na nyinginezo. Wasomi hawa wanabaini kuwa sababu kuu ya makosa haya ni tofauti katika miundo ya lugha hizo mbili. Kazi hii ni ya umuhimu kwa utafiti wetu kwani imetuwezesha kupata taarifa za msingi kuhusu mada yake, kujua aina za makosa yanayohusiana na ufofonolojia na pia sababu za wanagenzi kuyatekeleza na jinsi ya kuyashughulikia makosa hayo. Kazi yao ina utofauti na uchunguzi huu kwani uchunguzi wetu unatumia falsafa ya uchanganuzi makosa na unatafiti lugha ya Kikuyu.

Ni dhahiri kuwa suala la makosa katika ujifunzaji wa lugha nyingine ni suala ambalo limeshughulikiwa na wengi wa watafiti. Kazi hizi zimejengea utafiti huu mrundiko wa data za kimsingi zilizotumika kuchanganua makosa ya kimofofonolojia kwenye kazi andishi za Kiswahili kati ya wanagenzi walio na asili ya lugha ya Kikuyu kwenye shule za sekondari Kahuro, jimbo la Murang’a.

Pia, imebaini kuwa kuna upungufu wa tafiti zinazohusiana na uchanganuzi wa hitilafu za kimatamshi na kimaandishi katika Kiswahili kati ya wanagenzi walio na asili ya Kikuyu kaunti ndogo ya Kahuro, kaunti ya Murang’a na kwa hivyo utafiti huu unaziba pengo lililopo kwa kujikita katika makosa ya kimofofonolojia yanayofanywa na wanagenzi wenye asili ya lugha ya Kikuyu katika kazi andishi za Kiswahili.

**2.2 Misingi ya Nadharia**

Nadharia inaelezwa kwamba ni maelezo, mawazo na mwongozo uliopangwa kwa nia ya kusaidia uelezaji, utatuaji na utekelezaji wa jambo maalumu (TUKI, 2004). Nao Mdee J. S. & wenzake (2011) wanafasiri nadharia kama mpango wa mawazo ambao umetungwa kwa nia ya kuelekeza

namna ya ufanyaji au utekelezaji wa jambo maalumu. Falsaya ambayo imetumiwa katika huu uchunguzi ni ile ya Uchanganuzi Makosa iliyoasisiwa na Stephen Pit Corder katika mwaka wa 1960 na ikaenea sana miaka ya sabini. Nadharia hii inaangazia makosa ambayo mwanafunzi hufanya anapojifunza lugha nyingine na haswa ya pili (Selinker, 2008).Falsafa ya Uchanganuzi Makosa ni mbinu ya utafiti na uchambuzi inayolenga kutambua, kueleza na kurekebisha makosa katika lugha.Nadharia hii hutumika sana katika taaluma ya isimu na elimu hususan katika kujifunza lugha ambapo inasaidia wanafunzi na wataalamu kuelewa wapi na kwa nini makosa yanatolewa na jinsi ya kuyarekebisha.Nadharia hii hutumiwa na watafiti kuonyesha makosa ambayo wanagenzi wanaojifundisha lugha ya pili hufanya. Nadharia hii huchunguza aina ya makosa katika lugha ya uzungumzaji na uandishi na pia vyanzo vyake.

**Misingi ya Nadharia ya Uchanganuzi Makosa**

1. Wakati wanagenzi wanajifunza lugha ya pili ni sharti wafanye makosa.

2. Mwanagenzi asiadhibiwe wakati anafanya makosa kwani ni hali ya kawaida kwenye ujifunzaji wa lugha nyingine yoyote.

**Mihimili ya Nadharia ya Uchanganuzi Makosa**

1. Uchambuzi wa makosa. Unahusisha ukusanyaji wa data kuhusu makosa yanayofanywa na wanafunzi wa lugha na kisha kuyachambua ili kuelewa aina na vyanzo vya makosa hayo.

2. Sababu za makosa. Sababu za makosa zinaweza kujumuisha mwingiliano baina ya lugha ya kwanza, kukosa ujuzi wa lugha ya pili na matumizi mabaya ya kaida za lugha.

3. Aina za makosa yanaweza kugawanywa katika makundi ya aina tofauti mathalani, ya kifonolojia, kimofolojia, kifonetiki, kimsamiati, kisarufi na kisintaksia.

4. Marekebisho. Nadharia hii ya uchanganuzi makosa pia inahusisha njia za kurekebisha makosa ambayo yanaweza kuhusisha mazoezi ya ziada, ufafanuzi wa arudhi za lugha na kutoa marekebisho yanayosaidia.

Uchunguzi huu wetu umetumia mihimili yote minne katika kuchambua makosa ya kifonolojia na kimofolojia kwenye kazi andishi za wanagenzi, kueleza sababu za wanagenzi hawa kufanya makosa ya kimofofonolojia na pia kueleza jinsi ya kurekebisha na kupunguza makosa haya ya kimofofonolojia katika kazi andishi za Kiswahili kati ya wanafunzi hawa.

**Hatua za Uchanganuzi Makosa**

Kulingana na maelezo ya Mwanaisimu Corder (1960), anayechunguza makosa huhitajika kufuata hatua zifuatazo;

1. Kuweka pamoja sampuli hitajika za wajifunzaji lugha.

2. Utambuzi wa palipo na ukosaji.

3. Kuyaeleza makosa kwa kuyapanga kwenye vikundi na kuyaeleza kisarufi.

4. Kufafanua kilichosababisha makosa.

5. Kutathmini au kusahihisha makosa husika kwa lengo la kuyatafutia suluhu.

6. Kuonyesha athari inayosababishwa na makosa hayo.

Utafiti huu ulizingatia mihimili mitano inayofuata ya falsafa hii ya Uchanganuzi Makosa kama inavyofafanuliwa na mtaalamu Ellis (1994):

1. Kukusanya data.Katika hatua hii data hukusanywa kupitia njia ya masimulizi na maandishi kwa sababu makosa ya kimaandishi na kimasimulizi huweza kutofautiana kwa Sababu

watu mara nyingi huweza kuwa makini wanapoandika kuliko wanapozungumza.Utafiti huu umetumia data kutoka maandishi ya insha za wanafunzi.

2. Kubainisha makosa.Hapa, mtafiti huyabainisha makosa baada ya kupata data kutoka kwa lugha ya mwanafunzi.Ubainishaji huu wa data humwezesha mtafiti kuamua mapema mambo muhimu au sifa ambazo zinayabainisha makosa ya mwanafunzi.Mtafiti pia, huweza kujiwekea kanuni za kuzingatia katika uchunguzi wake wa kuyabainisha makosa.Aidha, uamuzi hufanywa kwa kuzingatia makosa ambayo ni bayana na yale ambayo si bayana.
3. Kufafanua makosa.Ellis(1994) anasema kuwa maelezo kuhusu makosa ya mwanafunzi huleta ulinganishi wa semi za mwanafunzi na miundo ambayo inapaswa kuzingatiwa katika lugha lengwa.Hali hii huambatana sana na uainishaji wa makosa ambayo yamebainishwa katika hatua iliyotangulia.Ufafanuzi wa makosa huambatana na uainishaji wake pale ambapo makosa hupangwa katika kategoria tofauti tofauti kulingana na vigezo ambavyo mtafiti amejiwekea.Pia, katika hali hii ya ufafanuzi wa makosa ya mwanafunzi ndipo mtafiti huweza kuonyesha pia kiwango cha makosa hayo ili kuifanyia uchunguzi wa kina katika mhimili unaofuata.
4. Kueleza makosa.Hii inahusisha kueleza makosa yaliyobainishwa na kufafanuliwa.Ellis(1994) anaonyesha kuwa kuyaeleza makosa kunachangia sana katika kuonyesha chanzo cha makosa hayo.Kwa hivyo, uchanganuzi makosa unaleta uwezo mkubwa wa kupata maelezo ya makosa ya mwanafunzi wa lugha ya pili hasa kwa kuzingatia vipengele vifuatavyo viwili;

Mount Kenya University

a) Kipengele cha maingiliano ya lugha.Kwa kuzingatia mwingiliano wa lugha, makosa yana uwezekano wa kutoka kwa lugha ya kwanza kwa vile yanahusisha ruwaza za lugha tofauti.

b) Kipengele cha makosa ya masuala ya ndani ya lugha ambayo hujitokeza wakati yanatokana na lugha yenyewe inayofunzwa au inayochunguzwa kwa mfano, kosa la ujumuishaji wa baadhi ya kanuni za kisarufi anazozimudu mwanafunzi.

5. Kutathmini makosa.Hatua hii ya kutathmini makosa ni jambo linalohusisha kuchunguza athari za makosa kwa mwanafunzi anayetafitiwa kwa ajili ya kuboresha mikakati ya ufundishaji wa lugha.Hii huhusisha pia, kuchunguza vyanzo vya utokeaji wa makosa fulani na njia za kuepuka makosa hayo kupendekezwa.

Tulitambua mihimili ifuatayo ili kutuelekeza katika kuchanganua data ya uchunguzi huu: Ukusanyaji wa data, kubainisha makosa, kufafanua makosa, kueleza makosa na kutathmini makosa. Mihimili hii imetumika kwenye uchunguzi wetu kwa vile imetuwezesha kuchunguza makosa ya kimofofonolojia kwa utaratibu mwafaka kwenye kazi andishi za Kiswahili baina ya wanagenzi walio na asili ya lugha ya Kikuyu katika shule za sekondari Kahuro, jimbo la Murang'a. Aidha, mihimili hii imemwezesha mtafiti kuchanganua vyanzo vya makosa ya kimofofonolojia na pia kueleza njia za kuepukana na makosa hayo kwenye kazi andishi za Kiswahili kati ya wanagenzi wenye asili ya lugha ya Kikuyu kwenye shule za sekondari, Kahuro, kaunti ya Murang'a.

## 2.3 Hitimisho

Sura ya pili imejihusisha na yale ambayo yameandikwa juu ya mada inayolingana na viwango vya lugha na pia ile falsafa iliyotumika kwenye uchunguzi huu.

Mount Kenya University

Mount Kenya University

# SURA YA TATU

# MBINU ZA UTAFITI

## 3.0 Utangulizi

Hii sura imezingatia sehemu za umuhimu zikiwemo mbinu zilizotumiwa katika utafiti, vifaa vya utafiti, sampuli ya utafiti na njia za kukusanya data pamoja na mbinu zilizotumiwa kuwasilisha na kuchanganua data.

## 3.1 Mbinu za Utafiti

Watafiti tofauti tofauti wameeleza ufafanuzi wa mbinu zinazotumika wakati wa utafiti. Kulingana na Kothari (2004), hizi ni zile njia zinazoweza kutumiwa na mtafiti katika kazi yake. Utafiti huu

ulifanywa nyanjani na maktabani. Kule nyanjani, mtafiti alikusanya data kwa njia ya maandishi ambapo aliwapa insha wanagenzi wa shule za upili katika shule ya upili ya kutwa ya Koimbi katika jimbo dogo la Kahuro, kaunti ya Murang'a.Insha hizi zilipeanwa kwa wanafunzi wa kidato cha pili, kidato cha tatu na kidato cha nne.Wanafunzi hawa waliandika insha yenye mada "Siku ya kukumbukwa maishani mwangu" na kisha mtafiti akasoma insha hizo huku akidondoa makosa ya kifonolojia na kimofolojia ambayo yalijitokeza. Maktabani, mtafiti alizuru maktaba mbalimbali na mitandaoni ili kusoma makala mbalimbali, tasnifu za wasomi mbalimbali pamoja na vitabu na kubaini sababu za wanagenzi ambao wanajifunza lugha ya pili kufanya makosa na jinsi ya kukabiliana na makosa ya kimofofonolojia kati ya wanagenzi wanaojifunza lugha ya pili.

### 3.2 Mahali pa Utafiti

Kulingana na Babbie (1992), pahali pa utafiti huwa ni pale ambapo utafiti fulani hutekelezwa. Naye Enon (1998) anasema kuwa hapa ni pale ambapo mtafiti anatumia ili kukusanya data inayohusu mada yake. Kwa hivyo, eneo au mahali pa utafiti ni sehemu mbalimbali ambazo mtafiti huzuru kwa nia ya kukusanya data ya uchunguzi. Huu utafiti unahusu kuchanganua makosa ya kimofofonolojia kwenye kazi andishi za Kiswahili baina ya wanagenzi wa shule za sekondari wenye asili ya lugha ya Kikuyu kutoka kaunti ndogo ya Kahuro, jimbo la Murang'a.Eneo hili la Kahuro, Murang'a lilichaguliwa na mtafiti kwa sababu kulingana na Corder(1981),ili kueleza lugha, data inayokubalika sharti itolewe kwa wazungumzaji wa lugha hiyo. Eneo la Kahuro, Murang'a ni mojawapo ya maeneo ambayo wazungumzaji asili wa lugha ya Kikuyu wanapatikana.Mtafiti amechagua kaunti ndogo ya Kahuro, Murang'a kwa kimakusudi kwa vile ni eneo mojawapo ambalo lina Wakikuyu asilia(Rukwaro,2015) na pia ndilo eneo lililo karibu na mtafiti. Mtafiti alitumia maktaba na mtandao kukusanya data kwa njia ya kusoma vitabu, Makala na tasnifu kuhusu makosa ya kisarufi, makosa ya kifonolojia na kimofolojia kati ya wanagenzi

wanaojifunza lugha ya pili na vyanzo vya makosa ya kimofofonolojia na namna ya kurekebisha makosa hayo ya kimofofonolojia .Nyanjani, mtafiti aliwasilisha insha kwa wanagenzi wa shule za sekondari kwenye shule ya sekondari ya kutwa ya Koimbi katika jimbo dogo la Kahuro, jimbo pana la Murang'a.Hii ni baada ya mtafiti kutambua kwamba shule hii huwasajili wanafunzi kutoka shule za msingi tofauti zinazoizunguka ambazo zimo katika vijiji tofauti katika jimbo hili dogo la Kahuro, hivyo mtafiti aliweza kupata data ya kuridhisha kwani hawa ni wanafunzi ambao wametoka vijiji tofauti na shule za msingi tofauti.Mtafiti alitumia mbinu ya maandishi kwa kupeana insha kwa sababu uandishi wa insha humpa mwanafunzi uhuru wa kujieleza atakavyo na pia wanafunzi huwa makini sana kutumia lugha sahihi wanapoandika kuliko wanapozungumza. Hivyo, makosa ambayo yalijitokeza katika kazi andishi yalidhihirisha tatizo ambalo linafaa kushughulikiwa.

### 3.3 Uteuzi wa Sampuli

Sampuli huwa ni ile sehemu ndogo ya watafitiwa walioteuliwa kuiwakilisha idadi yote ya watu ambao wanalengwa katika utafiti (Mugenda na Mugenda, 1990) naye Kothari (2004) anaeleza kuwa hiki ni kikundi kidogo cha watafitiwa kilichochaguliwa ili kuwakilisha mienendo ya kundi zima ambalo humwezesha mchunguzi yeyote kupata taarifa atakayo inayohusiana na sampuli hiyo ili kutoa ujumuisho wa utafiti.Utafiti huu ulifanyiwa wanagenzi 120 wa shule ya upili ya kutwa ya Koimbi. Katika uchunguzi wetu, mtafiti alitumia njia ya kimakusudi kuteua sampuli yake. Sababu kuu ya kutumia shule iliyopo katika jimbo la Murang'a ni kwa kuwa sehemu hii ni mojawapo ya sehemu ambayo Wakikuyu asilia wanapatikana (Rukwaro, 2015). Mtafiti aliwachagua wanagenzi 30;kumi kutoka kidato cha pili,kumi cha tatu na kumi cha nne; ambao ni sehemu ya wanagenzi wa shule ya upili ya kutwa ya Koimbi ambayo ni shule mojawapo kwenye kaunti ndogo ya Kahuro, jimbo la Murang'a na huwasajili wanagenzi kutoka shule za msingi tofauti kutoka eneo



Mount Kenya University

hili.Wanafunzi katika kila kidato walihitajika kila mmoja kuchukua kijikaratasi kilichoandikwa la au ndio.Kisha wanagenzi ambao walichagua vijikaratasi vilivyoandikwa ndio walishirikishwa katika utafiti kwa kupewa mtihani wa insha kisha mtafiti akasoma insha hizi na kuchanganua makosa ya kifonolojia na kimofonolojia na pia kutambua sababu za wanafunzi hawa kufanya makosa ya kimofonolojia na jinsi ya kurekebisha makosa hayo.

## 3.4 Vifaa vya Utafiti

### 3.4.1 Kalamu na Shajara

Mtafiti alivitumia vifaa hivi kuandika habari muhimu ambazo zilimsaidia katika utafiti wake na kumfanya asiyasahau yaliyo muhimu.

### 3.4.2 Tovuti na Kompyuta

Mtafiti alitumia tovuti na kompyuta kwa kiwango cha juu sana ili kuweza kupata habari za msingi na za ziada kuhusu mada hii.Tovuti na kompyuta pia ilimsaidia mtafiti kutalii mahitaji ya utafiti na kuchapisha makala na kuhifadhi data ya utafiti.

### 3.4.3 Insha za Wanafunzi

Herbert na wenzake (1989) walipendekeza mbinu tatu za kusaka data inayohusiana na makosa ya wanagenzi katika kujifunza lugha nyingine isiyo yao asilia, ni wao kutoa majibu ya maswali ya utafsiri kutoka kwa hojaji, kupewa mtihani na pia kutengewa vipindi vya hadithi. Mtafiti aliwapa wanafunzi mtihani wa insha yenye mada “Siku ya kukumbukwa maishani mwangu”

## 3.5 Kukusanya Data

Kulingana na Kothari (2004), kukusanya data huwa ni ile shughuli ya mwanzo zaidi kwenye uchunguzi na ambayo humfanya mtafiti kuweza kuibuka na habari muhimu ili kumwezesha

kuyafikia malengo kusudiwa. Naye Enon (1998), anadai kwamba kukusanya data ni kazi ya mwanzo ya uchunguzi ambayo humuauni yule mchunguzi kupata ujumbe aliokusudia ili kumwezesha kufikia lengo alilokuwa nalo kabla ya utafiti. Ukusanyaji wa data ni muhimu kwani vipengele vya kuwasilisha na kuchambua data haviwezi kutimilika kabla ya kitendo cha kukusanya data kutekelezwa. Ukusanyaji wa data ya uchunguzi huu ulihusika na kuwapa wanafunzi wa shule ya upili ya kutwa ya Koimbi iliyo katika jimbo dogo la Kahuro, Murang'a insha yenye mada "Siku ya kukumbukwa maishani mwangu" ambapo makosa ya kifonolojia na kimofolojia yalinakiliwa kisha yakaainishwa kabla ya kuchambuliwa na kuwasilishwa.

### 3.6 Uchanganuzi wa Data

Data ambazo zilikusanywa ziliwekwa pamoja na uchanganuzi kufanyika kwa utaratibu kwa mujibu wa falsafa ya Uchanganuzi Makosa.Insha za wanafunzi ziliainishwa ili kubaini makosa ya kifonolojia na kimofolojia na kuelezwa.Uchanganuzi ulifanyika kwa mbinu ya kimaelezo na baadaye matokeo ya uchunguzi yakaandikwa na kuwasilishwa.

### 3.7 Maadili ya Utafiti

Huu uchunguzi ulifanyika punde tu kibali cha kufanya utafiti kutoka chuo kikuu cha Mount Kenya kilipopatikana, msimamizi kupeana idhini na pia baada ya kupata cheti cha uchunguzi kutoka shirika la NACOSTI .Pia, utafiti huu uliendelezwa kwa njia wazi bila hisia au ubaguzi wa aina yoyote.Aidha, siri zote zilitunzwa.

### 3.8 Hitimisho

Sehemu hii, imeshughulika na njia za kufanya utafiti, mahali pa kufanyia uchunguzi, kuteua sampuli, ala za utafiti, kukusanya data na uwasilishaji wa data, maadili ya uchunguzi na kuchanganua data.

## SURA YA NNE

## MATOKEO YA UTAFITI NA UCHANGANUZI

### 4.0 Utangulizi

Kwenye sura hii, mchunguzi ameeleza dhana muhimu zinazohusiana na utafiti huu.Dhana ambazo zimeelezwa kwa kina ni pamoja na fonolojia, fonetiki, mofolojia na ulinganishi baina ya fonolojia na fonetiki, aidha ulinganishi baina ya fonolojia na mofolojia.Dhana ya mofofonolojia pia imefafanuliwa katika sura hii.

Aidha, mofofonolojia ya lugha ya Kiswahili na pia ya Kikuyu imefafanuliwa. Aidha, mifanyiko ya kimofofonolojia imeshughulikiwa kwenye sura hii. Dhana ya makosa katika lugha pia haijawachwa nje.

Kisha sehemu ya kuchanganua data ambayo ni sehemu inayonuia kujibu maswali ya uchunguzi huu ambayo ni kubainisha makosa ya kifonolojia kwenye kazi andishi za Kiswahili kati ya wanagenzi wa shule za sekondari wenye asili ya lugha ya Kikuyu katika jitihada zao za kujifunza lugha ya Kiswahili, kutambua makosa ya kimofolojia kwenye kazi andishi za Kiswahili katika

juhudi za ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili baina ya wanagenzi wa shule za sekondari wenye asili ya lugha ya Kikuyu, kubaini vyanzo vya makosa ya kimofofonolojia kwenye kazi andishi za Kiswahili katika juhudi za ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili miongoni mwa wanafunzi wa shule za sekondari wenye asili ya lugha ya Kikuyu na kutathmini namna ya kurekebisha makosa ya kimofofonolojia kwenye kazi andishi za lugha ya Kiswahili kati ya wanagenzi wa shule za upili wenye asili ya lugha ya Kikuyu.Uchanganuzi wa data hii ulifanywa kwa kuzingatia falsafa ya Uchanganuzi Makosa kwa kuzingatia mihimili na hatua ambazo zilipendekezwa na kuelezwa na wataalamu Corder(1960) na Ellis (1994).

Ili kubainisha na pia kubaini makosa ya kifonolojia na kimofolojia mtawalia, mtafiti aliweza kukusanya insha ambazo ziliandikwa na wanafunzi aliowahusisha katika sampuli yake na kuzipitia akizisahihisha huku akidondoa makosa ya kifonolojia na kimofolojia yaliyofanya na wanagenzi kwenye insha zao. Katika hali ya kubainisha na kutambua makosa hayo ya kifonolojia na kimofonolojia, mtafiti alitumia umilisi wa lugha ya Kiswahili sanifu alio nao.Aidha, mchunguzi alifuata hatua ya pili ya falsafa hii ya Uchanganuzi Makosa iliyoanzishwa na mwanaisimu Corder mwaka wa 1960.Hatua hii inapendekeza kwamba makosa ambayo yanatambuliwa yawekwe kwenye makundi.Kuna namna mbili za kupanga makosa kwenye makundi (Waweru,2012) akimnukuu Norrish(1987).Namna hizi mbili ni kuunda makundi yake kabla ya kubainisha na kutambua makosa hayo na kisha kuyapanga makosa hayo kwenye makundi ambayo umekwisha yatambua, na namna ya pili ni pale ambapo mtafiti anabainisha na kutambua makosa mwanzo na baada ya kubainisha na kutambua makosa anatengeneza makundi kutokana na makosa aliyoyatambua. Kwenye uchunguzi huu, mtafiti alihusisha mbinu ya pili kwani alibainisha na kutambua makosa ya kifonolojia na kimofolojia kwanza kisha akatengeneza makundi kutokana na makosa ambayo yalidhihirishwa. Makosa ya kifonolojia yaliyobainishwa ni kama vile; kuchopeka

sauti mbalimbali, kudondosha sauti mbalimbali na pia kutumia fonimu mbadala.Makosa ya kimofolojia ni pamoja na; kuchopeka vipashio mbalimbali katika neno, kudondosha baadhi ya vipashio katika neno, uyeyushaji wa irabu, ubadilishanaji wa vipashio na kubadili mpangilio wa vipashio katika neno.

Baada ya kubainisha na utambuzi wa makosa ya kifonolojia na kimofolojia, mtafiti anaeleza sababu za wanagenzi wa lugha ya Kiswahili walio na asili ya lugha ya Kikuyu kufanya makosa ya kimofofonolojia kwenye kazi andishi za Kiswahili ambazo ni pamoja na; utofauti wa mfumo wa sauti za Kikuyu na Kiswahili, kutumia Kikuyu kwa muda mwingi, taathira za lugha ya Kikuyu kwenye Kiswahili, miundo tofauti ya kimofofonolojia ya maneno ya Kiswahili na ya Kikuyu, kutomudu sawasawa sheria za lugha ya Kiswahili na wakufunzi kutokuwa na utaalamu wa somo la fonetiki.Baada ya hapo, mtafiti anaeleza mifano ya mbinu ambazo zina uwezo wa kutumiwa ili wanagenzi wa lugha ya Kiswahili kwenye shule za sekondari wenye asili ya lugha ya Kikuyu kuepukana na kupunguza makosa ya kimofofonolojia kwenye kazi andishi za Kiswahili.

Sehemu hii inatamatika kwa kutoa muhtasari wa sura nzima.

### 4.1 Kipengele cha Fonolojia

Wanaisimu wengi wameshughulikia kipengele hiki cha fonolojia. Mathalan; Massamba na wenziwe (2004) wanaifasili fonolojia kuwa ni utanzu unaoshughulika na kuchambua mifumo ya sauti kwenye lugha mbalimbali. Mgullu (1999) anafasili fonolojia kama tawi la sauti ambazo zinatumiwa ndani mwa lugha mahususi na utekelezaji wa sauti hizo katika mfumo wa lugha ambayo inahusika. Njogu na wenzake (2006) anadai kuwa fonolojia ni tawi mojawapo la lugha maalumu ambalo lina vipashio vidogo zaidi ikilinganishwa na vipashio vingine vyovyote vya lugha kama vile semantiki, sintaksia na mofolojia. Anaendelea kusema kwamba vipashio vya

fonolojia ni pamoja na, fonimu na alofoni zake. TUKI (1990) nao wanasema kwamba fonolojia ni kipengele mojawapo cha isimu ambacho kinajishughulisha na kuchambua mifumo ya sauti ambazo zinatumiwa ndani mwa lugha fulani mahususi. Massamba (1996) naye anaeleza utanzu huu wa fonolojia kwa kusema kuwa ni utanzu wa isimu ambao huchunguza ruwaza za fonimu za lugha maalumu. Massamba&wenziwe (2004) wanadai kwamba fonolojia ni uwanja wa isimu unaojishughulisha na kuchughuza, kuchambua na kuainisha sauti ambazo ni pambanuzi na zinatumika kwenye mifumo tofauti tofauti ya fonimu za lugha ambayo ni sifa ya mwanadamu. Habwe & Karanja (2004) nao wanaeleza fonolojia kama tawi la isimu ambalo linachunguza namna sauti za lugha fulani zinafanya kazi yake ndani ya lugha tofauti tofauti.Wanaendelea kusema kwamba fonolojia huwa inashughulikia namna sauti zinatumika, zinapangwa na kuunganishwa katika lugha yoyote ile maalumu kwa minajili ya kutengeneza maneno, sentensi na vifungu vya maneno vyenye maana. Massamba (2012) naye anaifasili fonolojia kuwa ni kipengele mojawapo cha isimu ambacho kinajishughulisha na kuchughuza mifumo tofauti tofauti ya lugha ya mwanadamu. Hii ni kwa kuwa kila lugha ya mwanadamu ina ruwaza yake ya sauti inayoongoza kuunda kwa maneno kwenye lugha husika.Taaluma ya fonolojia ni kitengo ambacho huwa na shughuli zifuatazo;

i) Kuonyesha fonimu za lugha maalumu.

ii) Kuzieleza fonimu za lugha hiyo maalumu kwa kutumia sifa ambazo zimebainishwa.

iii) Uchunguzi wa kuathiriana kwa mifumo ya sauti katika sentensi mbalimbali za lugha mahususi.

iv) Uchunguzi wa mifumo ya kiimbo katika lugha mahususi.

Kwa kufuata fasili hizi basi ni sahihi kusema kuwa fonolojia ni tawi la isimu ambalo linachunguza sauti za lugha kwenye ruwaza au mfumo wa lugha mahususi.Fonolojia inahusiana na jinsi sauti za lugha hutumika na pia kusanifishwa kwa sauti hizi kwenye lugha.Huhusisha namna ambavyo sauti zinabadilika, zinatenganishwa na pia kutofautiana ili ziweze kutoa maana. Fonolojia kwa ujumla, inajishughulisha na uchunguzi wa namna sauti huwakilishwa ubongoni mwa wazungumzaji wa lugha fulani na namna ambavyo wanatumia sauti hizo ili kuwasilisha maana tofauti tofauti.

Wataalamu mbalimbali wanakubaliana kwamba tawi hili la fonolojia linaweza kuwekwa katika vipera viwili vikuu;

a) Fonolojia ya vipande
b) Fonolojia ya arudhi

Vipengele vya fonolojia ni pamoja na;

a) Fonimu-Hizi ni sauti za kimsingi ambazo hugeuza maana kwenye neno.
b) Sifa za kifonolojia-Hizi ni sifa ambazo hutumiwa kufafanua sauti fulani maalumu kama vile sauti za midomo, sauti za kaakaa laini na kadhalika.
c) Mifumo ya sauti-Kipengele hiki cha fonolojia kinachunguza kanuni na kaida zinazotawala namna sauti huingiliana na pia kutumika katika lugha mahususi.Kwa mfano, lugha fulani inaweza kuruhusu mfuatano wa sauti fulani na kwa upande mwingine, nyingine isiruhusu mfuatano huo.

Kwa hivyo ni dhahiri kuwa fonolojia ni taaluma ambayo inajishughulisha na namna sauti za lugha mbalimbali zinatumika katika kutengeneza maneno yanayowakilisha maana katika lugha hizo mbalimbali.Fonolojia pia, hujishughulisha na miundo, kujengwa na pia uamilifu wa sauti za lugha tofauti tofauti za wanadamu. Fonolojia hutambua ni sauti gani ambazo

Mount Kenya University

zinatumika kwenye lugha mahususi na ni sauti gani ambazo hazitumiki kwenye lugha hiyo mahususi.Aidha, fonolojia hutuonyesha ni sauti gani ambazo huungana na masharti ambayo yanazuiwa kuunganika kwa sauti fulani.

Kwa vile kila lugha ina mfumo na ruwaza yake maalumu ya sauti basi ni vigumu kupata lugha mbili zilizo na mfumo mmoja wa sauti.

### 4.1.1 Kipengele cha Fonimu

Kwa vile fonimu ndicho kipengele cha kimsingi cha fonolojia, ni bora zaidi kukizungumzia katika utafiti huu kwani fonolojia haiwezi kuwepo bila fonimu.Hii ni kwa sababu fonimu ndicho kipashio cha kimsingi cha lugha ambacho kinashughulikiwa katika fonolojia.Massamba & wenziwe (2004) wanadai kwamba fonimu ni vitamkwa ambavyo vina maana au ni vitamkwa ambavyo vina uwezo wa kugeuza maana ya maneno. Habwe & Karanja (2004) wanadai kwamba fonimu ni kipengele cha msingi sana ndani ya lugha ambacho kinabainisha maana. Njogu na wenziwe (2006) wanafasili fonimu kama kipengele kidogo sana cha fonolojia kinachobadili maana ya neno.

### 4.1.2 Sifa za Fonimu

Kulingana na Mgullu (1999) fonimu ina sifa zifuatazo;

a) Kila fonimu ina tabia zake mahususi za ufonetiki ambazo zinaweza kuelezewa kwa ajili ya kuifasiri fonimu husika.
b) Kila fonimu ina hulka zake ambazo ni za ufonolojia zinazoonyesha mpangilio wa fonimu husika kwenye lugha mahususi.
c) Wazungumzaji wa lugha mahususi huweza kuelewa tabia kamilifu za fonimu za lugha yao ambayo ni sehemu moja ya umilisi walio nao wa lugha hiyo maalumu.
d) Kina fonimu huweza kushiriki katika kuunda na kuleta tofauti katika maana ya neno.

e) Kuwa fonimu moja ikiwa peke yake huwa haina maana.Hii inamaanisha kuwa fonimu hii si kiashiria cha kiashiriwa chochote kile.
f) Kama fonimu yoyote itaongezwa kwenye neno lolote lile basi maana ya neno hilo itaweza kubadilika ama pia kupotea.
g) Aidha, ukipunguza idadi ya fonimu kwenye neno fulani basi neno hilo hubadilika kimaana au kupoteza maana husika.
h) Ruwaza ya fonimu kwenye neno pia ukipanguliwa neno husika hupoteza au kubadilisha maana.
i) Anasema kuwa lugha yoyote ile huwa na fonimu zake maalumu na pia fonimu za lugha mbalimbali hazina ufanano katika muundo au utendakazi wake.

Kipengele hiki cha a fonimu ni cha maana katika uchunguzi wetu kwa kuwa ni kwenye kumaizi fonimu za lugha ya Kiswahili na zile za lugha ya Kikikuyu ambapo tuliweza kubaini makosa ya kifonolojia na pia makosa ya kimofolojia.

## 4.2 Utanzu wa Fonetiki

Katika utafiti huu ni vyema kuangazia dhana ya fonetiki kwa sababu hili ni tawi la isimu ambalo lina uhusiano wa karibu sana na tawi la fonolojia ambalo tunaliangazia katika uchunguzi huu wetu.Tunaangalia maana ya fonetiki, matawi ya fonetiki na uhusiano baina ya fonolojia na fonetiki.

### 4.2.1 Fasili ya Fonetiki

Massamba (2016) anaeleza fonetiki kwamba ni utanzu wa isimu ambao unachunguza na kuchambua sauti zinazotumiwa na wanadamu wakati wanawasiliana wakitumia lugha, yaani usikiaji na utamkaji wa lugha.Sauti katika kiwango cha fonetiki huwa zinaitwa foni.Hivyo, ni

Mount Kenya University

sahihi kusema kuwa fonetiki ni tawi la sayansi ya lugha ambalo linachunguza namna sauti za lugha zinavyotamkwa, zinavyosikika na zinavyotambulika.Tawi hili la fonetiki linajumuisha uchambuzi wa namna sauti zinavyotengenezwa na viungo vya sauti, namna sauti zinavyosafiri kupitia hewa kama mawimbi ya sauti na pia namna sauti zinavyopokelewa na masikio na ubongo wa binadamu.

**4.3 Uhusiano Uliopo Baina ya Fonetiki na Fonolojia**

Mgullu(1999) anasema kuwa fonetiki na fonolojia ni vipengele viwili vya taaluma ya isimu ambavyo vina uhusiano wa karibu na hivyo vipengele hivi hutegemeana na pia kukamilishana.Hivyo ni muhimu kwa mwanataaluma yeyote anayechunguza tawi la fonolojia kuelewa tawi la fonetiki.Hii ni kwa sababu tanzu hizi mbili, yaani fonetiki na fonolojia hujihusisha na utafiti wa kitu kimoja ambacho ni sauti.Ingawa tawi la fonetiki linakaribiana sana na tawi la fonolojia, kuna tofauti kati ya matawi haya mawili.Tofauti hizi ni pamoja na;

a) Fonetiki huchunguza lugha kwa ujumla pasipo kuwekea maanani mpangilio ambamo sauti husika huwa inatumika kwa upande mwingine, fonolojia nayo huchunguza sauti ambazo zimo kwenye lugha maalumu.

b) Kitaaluma, fonetiki ni moja pekee lakini taaluma ya fonolojia ni nyingi kulingana na zilivyo lugha zenyewe.Hivyo basi, tuna fonolojia ya Kiswahili na fonolojia ya Kikikuyu kwa mfano lakini fonetiki ni fonetiki tu bila kuzingatia lugha mahususi.

c) Aidha,sauti ambazo zimekusanywa na wanataaluma wa fonetiki katika mifumo ya lugha tofauti tofauti ni nyingi mno na pia wangali wanaendelea na utafiti wa kukusanya sauti mbalimbali katika lugha mbalimbali, tofauti na fonolojia ya lugha maalumu ambayo huwa inatumia sauti kidogo maalumu kati ya zile sauti ambazo zimeorodheshwa na wataalamu wa kifonetiki.

d) Fonetiki ni mkusanyo wa sauti ambao hauna mwisho, kinyume na fonolojia ambayo ina kikomo.Wataalamu wanaamini kuwa lugha nyingi humu ulimwenguni huweza kutumia kati ya sauti ishirini na arobaini pekee yake.

e) Katika utanzu wa fonetiki, sauti zote huainishwa na kufafanuliwa kwa umakinifu ili kudhihirisha tofauti za kifonetiki katika foni.Ufafanuzi huu ni kinyume na ufafanuzi wa kifonolojia kwa sababu ufafanuzi wa kifonolojia ni wa unukuzi ambao ni mpana na huonyesha sifa za sauti ambazo ni bainifu kutoka lugha mahususi ambayo inashughulikiwa.

f) Katika utanzu wa kifonetiki, sauti kwa jumla huanishwa na kuelezwa kwa njia ya sifa bainifu ambazo huonyesha tofauti zote zilizo za kifonetiki za foni mbalimbali, kwa upande wa fonolojia, ni sauti bainifu katika lugha hiyo maalumu zinazoorodheshwa kama fonimu za lugha hiyo mahususi na kuelezwa kwa kuzingatia sifa bainifu ambazo ni za kimsingi kuleta utofauti wa fonimu husika katika lugha hiyo mahususi.Hii ina maana kwamba,sifa zingine za sauti kifonetiki zisizo sifa bainifu ndani ya lugha mahususi si lazima zitumiwe katika kuzifafanua fonimu za lugha hiyo maalumu.

g) Kipengele cha kueleza fonetiki huwa ni foni.Foni huelezwa kama kipashio cha kimsingi kabisa cha sauti kisichohusishwa na lugha yoyote maalumu.Hii ni kinyume na kiwango cha fonolojia ambapo kipashio cha kimsingi cha ufafanuzi ni fonimu.Ni wazi kuwa foni fulani inaweza kuwa fonimu katika lugha fulani lakini isiwe fonimu katika lugha nyingine.

h) Fonetiki ni taaluma ambayo haitilii maanani mpangilio maalumu katika uchambuzi wa foni lakini fonolojia ni taaluma ambayo huzingatia ruwaza mahususi iliyo na mpangilio maalumu ambao huchambua fonimu na pia mambo mengine kuhusu lugha.

i) Fonetiki hubainisha na kufafanua sifa za arudhi za sauti jinsi ambavyo zinatokea katika lugha tofauti tofauti ilhali fonolojia hushughulikia tu zile sifa za arudhi za sauti zilizo wazi katika lugha ambayo inachunguzwa na kutojishughulisha na zile sifa ambazo si wazi katika lugha hiyo maalumu inyotafitiwa.

Hivyo basi, ni sahihi kusema kuwa taaluma ya fonetiki na taaluma ya fonolojia ni taaluma ambazo zinategemeana na kukamilishana. Kwa hakika uchambuzi ulio wa kifonetiki husaidia kwa kiwango kikubwa uchambuzi wa kifonolojia na vivyo hivyo, utafiti wa fonolojia husaidia utafiti wa fonetiki.

Pili, fonetiki huwa ni msingi dhabiti ambao hutumika kurahisisha utafiti wa kifonolojia.

Tatu, sifa bainifu ambazo zinatumiwa katika taaluma ya fonolojia ni sawa na sifa bainifu ambazo zilitambuliwa na zinatumiwa katika uchunguzi wa kifonetiki.

Nne, inaaminika kuwa ingekuwa hakuna fonolojia za lugha tofauti tofauti basi wanataaluma wa fonetiki hawangeweza kuwa na jambo la kutafiti kwani taaluma ya fonetiki hupata foni zake zote kwenye lugha tofauti tofauti yaani fonolojia za lugha tofauti tofauti.

Mwisho, uchanganuzi wa kifonolojia aghalabu hutegemewa utumike kama njia ya kuchanganua fonetiki.Uchambuzi huwezesha watafiti kuelewa miundo ya lugha zinazochunguzwa zaidi na ndio msingi mkuu wa kuchunguza lugha.

### 4.4 Kipengele cha Mofolojia

Mathews (1974) akinukuliwa na Mgullu (1996) anaifasili dhana ya mofolojia kwa kusema kuwa ni tawi la somo la isimu linalotafiti miundo ya maneno na hasa miundo ya mofimu. Habwe & Karanja (2004) wanaeleza mofolojia kama neno ambalo linatumiwa kueleza utanzu wa isimu unaojikita kwenye uchunguzi wa maumbo ya maneno. TUKI (1990) nao hawajawachwa nyuma

kueleza dhana ya mofolojia.Wanasema kwamba mofolojia ni kiwango cha isimu kinachochunguza maneno na aina za maneno.

### 4.4.1 Sura za Mofolojia

Taaluma ya mofolojia hupewa sura mbili kuu ambazo ni;

a) Mofolojia kama kiwango cha sarufi au isimu ambayo huwa na jukumu la kuchunguza maneno ili kujua yalivyo maumbo yake.
b) Mofolojia kama kipengele mojawapo cha lugha.

Kwa ujumla basi, tunaweza kusema kwamba mofolojia ni utanzu wa isimu ambao unachunguza mpangilio wa maneno.Hii ni pamoja namna maneno huwa yanaunganishwa, namna maneno yanabadilishwa na pia namna maneno yanatumika katika lugha na uchambuzi wa miundo ya maneno mbalimbali.

Kipashio cha kimsingi katika tawi la mofolojia ni mofimu. Martin (2002) anaeleza kwamba mofimu ni kipengele cha msingi sana kwenye lugha ambacho kina maana. Anaendelea kudai kwamba maana hiyo ya mofimu husika huwa inatofautiana na mofimu zingine kwenye lugha hiyo mahususi. TUKI (1990) wanafasiri mofimu kuwa ni kipengele kidogo sana kilicho na uamilifu kwenye maumbo ya maneno.

### 4.4.2 Sifa za Mofimu

1) Mofimu ni kipashio kilicho na umbo maalumu.
2) Mofimu huwa na umbo lake la kifonetiki.
3) Mofimu huwa na maana.

4) Kila mofimu huwa na sehemu yake ya kisintaksia kwenye kuunda vipashio vilivyo vikubwa zaidi.

### 4.5 Uhusiano Uliopo Kati ya Fonolojia na Mofolojia

Ni vigumu kuchunguza mofolojia bila kuzingatia fonolojia kwani matawi haya mawili hushirikiana na kukamilishana.Aidha, mabadiliko ya kimofolojia hutegemea mabadiliko ya kifonolojia.

Matawi haya mawili yana uhusiano ufuatao;

a) Mpangilio wa kifonolojia na kimofolojia huwa na uwezo wa kuingiliana wakati wa kuchambua mabadiliko katika maumbo ya maneno. Wanaisimu wanakubaliana kuwa arudhi fulani za kifonolojia huweza kutokea kabla ya zile za kimofolojia.
b) Viwango vya fonolojia na mofolojia hufuatana na kushirikiana katika kutekeleza kazi kwenye ngazi tofauti tofauti ili kupata leksia mpya iliyo na muundo tofauti na neno asilia.
c) Mofimu, ambacho dicho kipashio cha kimsingi katika mofolojia yaani kipashio kidogo sana cha maana kwenye lugha na fonimu ambacho dicho kipashio kidogo sana cha sauti na msingi wa fonolojia huweza kutofautisha maana hivyo, tunasema kuwa ili mofimu itamkwe, lazima ifuate kanuni za kifonolojia na kwa hivyo mofolojia inategemeana na fonolojia ili kuhakikisha kuwa mofimu husika zinatamkwa kwa usahihi.
d) Fonolojia huangazia namna sauti huweza kubadilika kulingana na mazingira ambayo yanaizunguka na mabadiliko haya huwa ya maana ili kujua mofimu mbalimbali.Kwa mfano, mofimu moja ina uwezo wa kuwa tofauti kifonolojia ila ikabeba maana ile moja.
e) Huwa kuna mofimu ambazo wakati zinafungamanishwa na neno huweza kubadilisha matamshi ya hilo neno kwa mujibu wa kanuni za kifonolojia.

f) Ni wazi kuwa fonolojia huhusisha sauti namna ambavyo zinatumika katika kuleta tofauti za maana ya maneno na pia tunajua mofolojia inahusiana na namna mofimu zinaunda maneno.Kwa hivyo, ni sharti uhusiano wa sauti yaani fonolojia na vipengele vya maana yaani mofolojia ifahamike ndiposa tuweze kuelewa miundo ya maneno na namna maana hubadilika.

g) Mofolojia huwa inashughulikia namna ambavyo sauti zinapangwa na kutamkwa na kwa upande mwingine, mofolojia inachunguza namna vipande vya maneno yaani mofimu huunda maneno ambayo yana maana.Kwa hivyo, ni lazima fonolojia na mofolojia kushirikiana ndiyo maneno yaundwe na kubadilishwa katika lugha.

### 4.6 Dhana ya Mofofonolojia

Neno hili mofofonolojia limetengenezwa kutokana na maneno mawili ambayo ni mofolojia na fonolojia. Maneno haya mawili huwa ni kiwakilisho cha viwango viwili tofauti kwenye taaluma ya isimu.Kama tulivyotanguliza kusema hapo juu, fonolojia ni taaluma ya isimu inayohusu utumiaji wa sauti kwenye lugha maalumu ilihali mofolojia ni tawi la isimu linalojishughulisha na kuchunguza, kuchambua na kufafanua maumbo ya maneno kwenye lugha maalumu.

Haya maneno mawili yana uhusiano kwa sababu sheria za kifonolojia huweza kurejelewa katika kueleza maumbo ya kimofolojia. Arudhi hizi pia huwa na uwezo wa kubadilisha umbo na neno yaani, umbo la ndani na umbo la nje. Maneno haya yakifungamanishwa yanaunda neno mofofonolojia.

Mofofonolojia ni istilahi inayotumiwa kumaanisha tawi la isimu ambalo linashughulika na matumizi ya mofolojia ili kueleza baadhi ya tofauti katika fonolojia zisizowezakana kuelezwa kwa kutumia data za kifonetiki ama kifonolojia peke yake ( Massamba, 2010).

Mount Kenya University

### 4.7 Sauti za Lugha ya Kiswahili na Lugha ya Kikuyu

Sauti ni kipengele kidogo kabisa cha neno ambacho hakiwezi kugawika zaidi.Pia tunaweza kusema ni mlio au tamko ambalo hutokana na kutagusana kwa ala za kutamkia.

#### 4.7.1 Sauti za Lugha ya Kiswahili

Kulingana na Mgullu (1999) lugha ya Kiswahili ina sauti au fonimu 31.Sauti hizi ni;

| Herufi | Ukubwa | Mnukuu |
|---|---|---|
| 1. a | A | [a] |
| 2. b | B | [b] |
| 3. ch | CH | [tʃ] |
| 4. d | D | [d] |
| 5. dh | DH | [ ð] |
| 6. e | E | [ ɛ] |
| 7. f | F | [ƒ] |
| 8. g | G | [g] |
| 9. gh | GH | [γ] |
| 10. h | H | [h] |
| 11. i | I | [i] |
| 12. j | J | [J] |
| 13. k | K | [k] |
| 14. kh | KH | [k] |
| 15. l | L | [l] |

| | | |
|---|---|---|
| 16. m | M | [m] |
| 17. n | N | [n] |
| 18. ng’ | NG’ | [ŋ] |
| 19. ny | NY | [ɲ] |
| 20. o | O | [o] |
| 21. p | P | [p] |
| 22. r | R | [r] |
| 23. s | S | [s] |
| 24. sh | SH | [ʃ] |
| 25. t | T | [t] |
| 26. th | TH | [θ] |
| 27. u | U | [u] |
| 28. v | V | [v] |
| 29. w | W | [w] |
| 30. y | Y | [j] |
| 31. z | Z | [z] |

Sauti hizi zimegawanywa katika aina mbili kuu:

a) Irabu

b) Konsonanti

Mount Kenya University

Irabu ni sauti ambazo zinapotamka hewa huwa haizuiliwi katika sehemu yoyote katika mkondo hewa na konsonanti ni sauti zinapotamka hewa huwa inazuiliwa kwenye sehemu tofauti tofauti za kutamka (Waihiga, G. na Wamitila, W. (2003).

**4.7.1.1 Irabu za Lugha ya Kiswahili**

Lugha ya Kiswahili ina fonimu za irabu tano. Hizi ni;

| Irabu | Nukuu | Mfano katika neno |
|---|---|---|
| 1. a | /a/ | b**a**b**a** |
| 2. e | /ɛ/ | y**e**y**e** |
| 3. I | /i/ | m**i**m**i** |
| 4. O | /⊃/ | mt**o**t**o** |
| 5. u | /U/ | mt**u** |

Mgullu (1999) anasema kuwa irabu hubainishwa kutegemea sifa tatu kuu ambazo ni;

1. Sehemu ya kutamkiwa irabu kwenye ulimi
2. Hali ya mwinuko wa ulimi
3. Hali ya mkao wa midomo wakati wa kutamka

**Hali ya Mwinuko wa Ulimi**

Mgullu (1999) anaeleza kuwa hali ya mwinuko wa ulimi huwa ni wa aina zifuatazo;

a) **Mwinuko wa chini-**katika aina hii ya mwinuko ulimu huinuka kidogo sana kwa hivyo huwa umelala chini katika upande wa kinywa chini.

b) **Nusu-chini-** katika aina hii ya mwinuko ulimi huwa hauendi chini sana ila huwa umekaribia chini.

c) **Nusu-juu**-katika aina hii ya mwinuko ulimi huwa karibu na upande wa juu ila haujafika juu sana.

d) **Juu**-ulimi huwa upo upande wa juu kabisa wa kinywa.

**Mkao wa Midomo**

Wanaisimu wa kifonetiki wanakubaliana ya kwamba irabu zinapotamkwa midomo huweza kuchukua mkao wa namna mbili kuu:

i)Mkao wa kuviringa.

ii) Mkao wa kutandaza.

Utafiti umebainisha ya kwamba irabu zote ambazo hutamkiwa mbele ya ulimi hutamkwa midomo ikiwa tandaze ilhali irabu zote zinazotamkiwa nyuma ya ulimi hutamkwa midomo ikiwa viringe.

**Mahali pa Kutamkiwa Kwenye Ulimi**

Irabu hutamkwa kwenye sehemu tatu tofauti za ulimi. Sehemu hizi ni;

a) Sehemu ya mbele ya ulimi
b) Sehemu ya kati ya ulimi
c) Sehemu ya nyuma ya ulimi

**Muhtasari wa Sifa za Irabu za Kiswahili**

/a/- irabu ya chini, kati, tandazwa

/e/-irabu ya wastani na mbele, tandazwa


/i/- irabu ya juu na mbele, tandazwa

/o/- irabu ya wastani, nyuma, viringwa

Mount Kenya University

/u/- irabu ya juu, nyuma, viringwa

**Mchoro 1: Irabu za Kiswahili**




Mchoro wa ulimi kinywani mwa mdomo wa mwanadamu.

Muhtasari wa sifa za irabu kutegemea sehemu za ulimi.

**Asili**: Waihiga, G. na Wamitila, K. (2003)

### 4.7.1.2 Konsonanti za Lugha ya Kiswahili

Mgullu (1999) anaorodhesha konsonanti 26 za Kiswahili ingawa orodha ifuatayo ina konsonanti 27 kutokana utafiti wa mtafiti mwenyewe (2024) ambaye ameongeza konsonanti /ng/ katika orodha. Orodha hii ni;

| Konsonanti | Nukuu ya kifonetiki | mfano wa neno |
|---|---|---|
| 1. b | /b/ | **b**a**b**a |
| 2. ch | /tʃ/ | **ch**ama |
| 3. d | /d/ | **d**a**d**a |
| 4. dh | /ð/ | **dh**ambi |
| 5. f | /f/ | **f**ua |
| 6. g | /g/ | o**g**opa |
| 7. gh | /γ/ | **gh**adhabu |

Mount Kenya University

| | | |
|---|---|---|
| 8. h | /h/ | **h**apa |
| 9. j | /j/ | **j**ana |
| 10. k | /k/ | **k**a**k**a |
| 11. kh | /x/ | **kh**anga |
| 12. l | /l/ | **l**a**l**a |
| 13. m | /m/ | **m**eza |
| 14. n | /n/ | **n**e**n**a |
| 15. ng’ | /η/ | **ng**’a**ng**’ana |
| 16. ny | /ɲ/ | **ny**ama |
| 17. ng | /ng/ | **ng**oma |
| 18. p | /p/ | **p**a**p**a |
| 19. r | /r/ | **r**udi |
| 20. s | /s/ | **s**ema |
| 21. sh | /ʃ/ | **sh**ati |
| 22. t | /t/ | **t**iti |
| 23. th | /θ/ | **th**amani |
| 24. v | /v/ | **v**aa |
| 25. w | /w/ | **w**eza |
| 26. y | /j/ | **y**a**y**a |
| 27. z | /z/ | me**z**a |

Konsonanti za Kiswahili huainishwa kwa mujibu wa sifa tatu kuu ambazo ni;

a) Mahali pa kutamkia/mahali hewa huzuiliwa

b) Jinsi hewa inavyozuiliwa kwenye ala za matamshi

Mount Kenya University

c) Hali ya kutetemeka kwa nyuzi za sauti wakati wa kutamka konsonanti

**Aina za Konsonanti Kutegemea Mahali Hewa Huzuiliwa Wakati wa Kutamka**

-Konsonanti za midomo-m, p, b, w,

-Konsonanti za meno-th, dh

-Konsonanti za mdomo na meno-f, v

-Konsonanti za ufizi- t, d, n, s, z, l, r

-Konsonanti za kaakaa gumu- j, ch, ny, sh, y

-Konsonanti za kaakaa laini-k, g, ng', gh

-Konsonanti ya koromeo-h

**Aina za Konsonanti Kutegemea Jinsi Hewa Inavyozuiliwa Kwenye Ala Mbalimbali za Kutamkia**

-Vipasuo-p, b, t, d, j, k, g

-Vikwamizo-f, v, th, dh, s, z, sh, gh, h

-Kipasuo-kwamizo-ch

-Nazali/ving'ong'o-m, n, ny, ng'

-Kitambaza-l

Kimadende-r

Nusu irabu/viyeyusho-y, w

**Aina za Konsonanti Kutegemea Mtetemeko Katika Nyuzi za Sauti**



Mount Kenya University

Sauti ambazo zinapotamkwa hutokea mtetemeko katika nyuzi za sauti huitwa konsonanti ghuna (GH), mifano ya konsonanti ghuna ni v, z, dh na b na kadhalika ilhali zile ambazo wakati wa kuzitamka hakuna mtetemeko katika nyuzi za sauti huitwa konsonanti sighuna au hafifu (H). Mifano ya konsonanti sighuna ni f, s, p na kadhalika.

**Jedwali 4.7.1: Mukhtasari wa sifa za konsonanti**

| Mahali<br>aina | Midomo/meno | mdomo | meno | ufizi | Kaakaa<br>gumu | Kaakaa<br>laini | koromeo |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| H<br>VipasuoGH | P<br>b | | | t<br>d | j | k<br>g | |
| Kipasuo H<br>kwamizo | | | | | ch | | |
| Nazali | m | | | n | ny | Ng’ | |
| VikwamizoH<br>GH | | f<br>v | th<br>dh | s<br>z | sh | | h |
| Kitambaza | | | | l | | | |
| Kimadende | | | | r | | | |
| Nusu irabu | w | | | | y | | |

Asili: Wamitila, K.W. na Waihiga, G. (2003)

Mount Kenya University


### 4.7.2 Sauti za Lugha ya Kikuyu

Lugha hii ya Kikuyu ina sauti 25 ambapo 18 ni konsonanti na 7 ni vokali (Iribe, 2016).

#### 4.7.2.1 Irabu za Lugha ya Kikuyu

Iribe M. P. (2016) anadai kwamba irabu za lugha ya Kikuyu ni saba.Hizi ni;

| Irabu | Nukuu | mfano wa neno | maana |
|---|---|---|---|
| 1. /a/ | /a/ | mboga | mboga |
| 2. /e/ | /ɛ/ | mite | itupe |
| 3. /i/ | /i/ | ini | ini |
| 4. / Ĩ/ | /e/ | mitĨ | miti |
| 5. /o/ | /⊃/ | iboko | viboko |
| 6. /u/ | /u/ | mabuku | vitabu |
| 7. / Ū/ | /o/ | mbŪku | sungura |




Mount Kenya University

**Mchoro 2: Irabu za lugha ya kikuyu**

Asili: Iribe, P. (2016)

**Jedwali 4.7.2 Mukhtasari wa Sifa Irabu za Kikuyu**

| Sehemu ya ulimi | mbele | wastani | nyuma |
|---|---|---|---|
| juu | i | | u |
| Kati-juu | Î | | Ū |
| Kati-chini | ε | | ⊃ |
| chini | | a | |

Asili: Mutahi K.E (1983)

**4.7.2.2 Konsonanti za Lugha ya Kikuyu**

Konsonanti za lugha hii ya Kikuyu ni 18(Mutahi, 1983).Konsonanti hizi ni;

| Konsonanti | Mfano wa neno | maana |
|---|---|---|
| 1. b(mb) | mburi | mbuzi |
| 2. d(nd) | kuenda | penda |
| 3. n(ng) | tongoria | ongoza |
| 4. β(b) | βaβa | baba |
| 5. ʃ(c) | ici | hizi |

| | | |
|---|---|---|
| 6. h(h) | haha | hapa |
| 7. th | maitho | macho |
| 8. γ(g) | mŪgate | mkate |
| 9. m(m) | makia | shitua |
| 10. n(n) | ina | imba |
| 11. t(t) | tata | shangazi |
| 12. k(k) | mwaki | moto |
| 13. r | ruma | uma |
| 14. ng’ | ng’eni | geni |
| 15. ny (η) | nyama | nyama |
| 16. nj(d) | njina | nichome |
| 17. w | ndawa | dawa |
| 18. y(j) | kaya | piga nduru |

Konsonanti hizi huainishwa kutegemea mahali zinapotamkwa na jinsi hewa inazuiliwa wakati wa kuzitamka.Tazama jedwali lifuatalo:

**Jedwali 4.7.3: Konsonanti za Lugha ya Kikuyu**

| **Mahali** <br> **Namna** | **midomo** | **meno** | **ufizi** | **Nyuma ya ufizi** | **Kaakaa gumu** | **Kaakaa laini** | **koromeo** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| vipasuo | b(mb) | | t d(nd) | | | k g | |

Mount Kenya University

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| nazali | m | | n | | ny | ng’ | |
| kimadende | | | r | | | | |
| vikwamizo | bβ | th | | c | | | h |
| Vipasuo-vikwamizo | | | | nj | | | |
| kikwamizo | w | | | | j | | |

**Asili**: Iribe (2016)

### 4.8 Miundo ya silabi za Kiswahili na zile za Kikuyu

Massamba na wenziwe (2004) wanasema kuwa silabi ni sehemu ya neno inayoweza kutamkwa kwa tamko moja na pia kwa pamoja. Kwa hivyo tunaweza kusema kuwa silabi ni tamko moja katika mfumo wa sauti.

#### 4.8.1 Miundo ya silabi za Kiswahili

Iribe M. (2008) anadai kuwa lugha ya Kiswahili ina miundo saba ya silabi. Hii ni;

1. **Vokali pekee( I)**

   Mfano; **o**-a

2. **Konsonanti na vokali (KI)**

   Huu ndio muundo pendwa wa silabi za lugha ya Kiswahili kama mojawapo ya lugha za Kibantu.

   Mfano**; ka**-la-mu

3. **Konsonanti mbili na vokali(KKI)**

   Mfano; **mba**-li

Mount Kenya University

4. **Konsonanti zaidi ya mbili na irabu(KKKI)**

   Huu si muundo maarufu katika lugha ya Kiswahili.

   Mfano; **mbwe**-ha

5. **Konsonanti na vokali mbili( KII)**

   Huu pia si muundo maarufu katika lugha ya KiswahIli.

   Mfano; **mii**-ko

6. **Konsonanti na kiyeyusho na irabu (KYI)**

   Mfano; **pwe**-za

7. **Konsonanti pekee(K)**

   Mfano; **m**-tu

**Silabi Funge**

Massamba na wenziwe (2001) wanasema kuwa huu ni muundo ambao unatokana na hali ya lugha ya Kiswahili kuwa na uwezo wa kukopa maneno kutoka kwenye lugha zingine, kwa mfano Kiarabu na Kiingereza.

Mfano**; muk**-ta-dha

**Dak** -ta-ri

**4.8.2 Miundo ya Silabi za Lugha ya Kikuyu**

Kulingana na Iribe (2016), miundo ya silabi za lugha ya Kikuyu ni saba.Hizi ni;

1. **Irabu ndefu pekee (I: )**

Mfano; ma-**î**-maji

2. **Konsonanti- irabu(KI)**

Mount Kenya University

Mfano**; ba**-ra-barabara

3. **Konsonanti mbili na irabu(KKI)**

   Mfano; **mwe**-ri

4. **Irabu ya kawaida moja(I)**

   Mfano; **i**-ge-go-jino

5. **Irabu mbili(II**)

   Mfano; **ui**-ru-wivu

6. **Konsonanti na vokali tatu(KIII)**

   Mfano; **niai**-na-ga-yeye huimba

7. **Konsonanti na Irabu mbili(KII)**

   Mfano; **ria**-kula

### 4.9 Mifanyiko/Kanuni za Kimofofonolojia Kwenye Lugha ya Kiswahili na ile ya Kikuyu

Pia hujulikana kama mikondo au kanuni za kifonolojia.Haya ni mabadiliko tofauti tofauti yanayotokea wakati fonimu tofauti tofauti zimewekwa pamoja tunapounda vipashio vingine vilivyo vikubwa zaidi kuliko fonimu hizo zenyewe.Vipashio ambavyo huundwa na fonimu husika vinaweza kuwa mofu, silabi na maneno. Kanuni au mikondo ya kifonolojia ni maandishi rasmi yanayowakilisha mchakato au mabadiliko asilia katika lugha.Kanuni za kifonoljia zimejikita katika nadharia za umuundo ilizoasisiwa na kuelezwa na Chomsky (1957) na Halle(1973).Wanasarufi hawa walibainisha muundo-ndani na muundo-nje wa maneno.Umbo-ndani na umbo-nje ni sura mbili tofauti ambazo zinarejelea muundo wa neno.Umbo-ndani na umbo-nje hueleza kuhusu vipengele vya mpangilio vielezo vya maneno na mifanyiko ambapo vigezo hivi viliegemewa kutoa ufafanuzi na maelezo zaidi kuhusu mabadiliko katika maumbo ya maneno na nomino mbalimbali.  Imebainika kuwa fonimu ziwekwapo pamoja huweza kuathiriana

mara nyingi kwa viwango tofauti tofauti na baadhi ya athari huwa ndogo na isiyobainika waziwazi ila wakati mwingine kuathiriana huko huwa kubwa kiasi cha kudhihirika waziwazi.Kwa kawaida mabadiliko haya hutokea kwa sababu ya fonimu kuwa karibu wakati wa kutamka hasa wakati wa kutamka silabi kwa mfululizo katika neno au mofu.Ingawa mabadiliko ya kifonolojia hutokea katika maneno, huwa hayabadili maana ya neno husika.

Wanaisimu wanakubaliana kuwa kila lugha ina mifanyiko/mikondo au kanuni zake za kifonolojia ambazo ni mahususi katika lugha hiyo maalumu.

**4.9. 1 Mikondo ya kimofofonolojia Kwenye Lugha ya Kiswahili**

Lugha yoyote ile ina ruwaza yake ya kimofofonolojia.Yaani hakuna lugha zinazofanana katika idadi zake za alofoni na fonimu.

Kuna mabadiliko au michakato aina mbili;

1. Michakato au mabadiliko ya kiusimilisho
2. Michakato au mabadiliko yasiyo ya kiusimilisho

**Mabadiliko ya Kiusimilisho**

Hii ni michakato ambayo inahusu kulandana kwa njia kiwango kikubwa kwa vitamkwa ambayo hutokana na ukaribu wake.Yaani, ujirani wa vitamkwa.Hii inamaanisha kuwa kitamkwa hupata sifa za kipande sauti chenzake ambacho kiko karibu na kitamkwa hicho.

Kuna aina mbili ya usimilisho ambayo ni;

1. Usimilisho mbele
2. Usimilisho nyuma

Mount Kenya University

Usimilisho mbele_ni usimilisho ambao hutokea pale ambapo fonimu ya kwanza ina uzito zaidi kiasi cha cha kufanya fonimu ya pili ifanane nayo ilhali usilimisho nyuma ni aina ya usilimisho ambao hutokea wakati konsonanti inakuwa karibu sawa na ile ambayo inaifuata hivyo basi nguvu za mabadiliko huelekea nyuma kutoka kwa fonimu ya kulia hadi kwa ile ya kushoto.Aghalabu mabadiliko haya ya usilimisho nyuma hutokana na mahali pa kutamkia sauti.

**Mabadiliko yasiyo ya Kiusimilisho**

Haya ni mabadiliko ambayo yanahusu sauti au vitamkwa ambazo hazina ufanano wa kiasi fulani wakati wa mchakato au ubadilikaji.

**Mabadiliko ya Kiusimilisho ya Kanuni za Kimofofonolojia**

1. **Uyeyushaji**

Haya ni mabadiliko ambapo sauti ambayo siyo kiyeyusho huathiriwa na kubadilika na kuwa kiyeyusho.Hii hufanyika wakati sauti mbili au irabu mbili au tatu zinapokutana na kutokea kuwa sauti moja.Katika lugha ya Kiswahili wakati mwingine hubadilika na kuwa nusu-irabu au kiyeyusho.Kwa mfano; irabu zinapotokea kwenye mazingira ya kufuatana huwa inabadilika na kuwa kiyeyusho.Kwa mfano;

a) (mu) + (ana ) ⟹ mwana
b) (mu) + (eupe) ⟹ mweupe
c) (vi) + (etu) ⟹ vyetu

2. **Unazalishaji wa Irabu**

Haya ni mabadiliko yanayohusu irabu kupata sehemu ya sifa za nazali inayotokana na irabu yenyewe kutangamana au kutagusana na konsonanti iliyo n nazali. Hivyo basi, irabu ambazo zinatangamana na nazali hupata sifa za unazali pia. Kwa mfano;

a) (muwa) ⟶ [m̑uwa]

b) (nuru) ⟶ [n̑uru]

3. **Ukaakaaishaji**

Katika aina hii ya mabadiliko ya kifonolojia, konsonanti ambayo hapo mwanzo haikuwa na sifa za kaakaa au haikuwa inatamkiwa katika kaakaa ngumu inapata sifa ya ukaakaa yaani, inatamkwa katika kaakaa ngumu.Hii hutokana na konsonanti kufuatwa na irabu au kiyeyusho. Kwa mfano;

(ki) + (etu) ⟶ chetu

(ki ) + (akula) ⟶ chakula

(ki) + (ombo) ⟶ chombo

4. **Utamkaji Pamwe wa Nazali**

Huu ni ubadilikaji ambapo konsonanti iliyo nazali hutamkwa mahali pamoja na konsonanti inayofuatia katika neno husika. Kwa mfano;

a) ndama----(n) inatamkwa mahali ambapo (d) inatamkwa katika sauti (nd)

b) mbuzi -----(m) inatamkwa mahaliambapo (b) inatamkwa katika sauti (mb)

5. **Mvutano wa Irabu**

Pia huitwa kuungana kwa sauti.Katika aina hii ya mabadiliko au mchakato, sauti mbili hukutana au kuungana .Hili hufanyika irabu ya juu na chini zinapokutana na kutangamana na irabu ya kati.Irabu za Kiswahili huvutana zinapokuwa zimetokea mahali pamoja au kufuatana na ambapo irabu moja ni ya juu na nyingine ni ya chini.Mvutano wa aina hii kwenye lugha ya Kiswahili

Mount Kenya University

hutokea zaidi kati ya irabu /a/ ambayo ni irabu ya chini na irabu /i/ ambayo ni irabu ya juu. Mvutano wa irabu /a/ na irabu /i/ huleta irabu/e/. Kwa mfano;

a) (ma) + (iko) ⟹ meko

b) (ma) + (ino) ⟹ meno

c) (wa) + (ingi) ⟹ wengi

**6. Konsonanti Kuathiri Nazali**

Haya ni mabadiliko ambapo utamkaji wa konsonanti huathiri nazali iwe inafanana na konsonanti inayoifuata katika neno. Kwa mfano;

a) (n) + (goma) ⟹ ngoma

b) (m) + (buzi) ⟹ mbuzi

**7. Nazali Kuathiri Konsonanti**

Katika aina hii ya mabadiliko, nazali ndiyo ambayo inaathiri konsonanti ili konsonanti husika iwe sawa na nazali.Mwanaisimu Katamba (1993) anadai kuwa mabadiliko haya ni kuimarika kwa sauti karibu. Kunazo sauti zilizo ndefu. Kwa mfano;

a) (u) +(limi) ⟹ ulimi

(n) +(limi) ⟹ ndimi

b) (u) + (refu) ⟹ urefu

(n) +(defu) ⟹ ndefu

Mount Kenya University

**8. Kulegea na Kukaza Sauti**

Kulegea na kukaza sauti ni aina ya mabadiliko ambapo sauti au kipande sauti fulani hubadilika na kulegea kutokana na mpito wa wakati.Mfano mzuri ni ambapo kipasuo/p/ huaminika kuwa kilizaa sauti/β / kutokana na kulegea kwa sauti/p/.Kwa mfano,Katika lahaja ya Chichifundi

(ha +pa) huwa (ha+βa) katika Chichifundi.

**9. Tangamano Irabu**

Huu ni mchakato ambapo vokali na vokali nyingine hupata kuathiriana kwa kiwango kwamba hulazimika kupata ufanano na kupeana sifa ambazo zifanana. Mfano, mofimu ya kutendea huwa inabadilika kutoka kwa irabu ambayo inafuata shina la neno.Kwa mfano;

a) Sema ⟹ semea

b) Pika ⟹ pikia

Kwa kawaida, irabu /a/, /u/ na /i/ mofimu yake ya kutendea ni /i/ nayo irabu /e/ na /o/ mofimu yake ya utendea huwa /e/.

Mchakato huu pia hutokea katika kuweka vitenzi katika kauli ya kutendesha

**Mabadiliko yasiyo ya Usimilisho Katika Kanuni za Kimofofonolojia**

**1. Udondoshaji**

Haya ni mabadiliko ambapo kitamkwa au sauti ambayo awali ilikuwa katika neno hudondoshwa au kuangushwa katika neno.Kwa mfano;

a) (mu)+ (tu) ⟹ (mtu) –hapa irabu /u/ inadondoshwa.

b) (mu) + (toto) ⟹ (mtoto)-hapa pia irabu/u/ inaangushwa

c) waliokuja ⟹ walokuja-hapa irabu /i/ inadondoshwa

**2. Uchopekaji**

Haya ni mabadiliko ambayo huwa kuna kuingizwa kwa sauti ambazo hazikuwa kwenye neno. Kwa mfano, uchopekaji wa irabu hutokea katika misamiati au istilahi za kigeni ambazo zimeingizwa kwenye lugha ya Kiswahili.Utohozi unapotokea na kuswahilishwa kwa maneno yaliyokopwa ili yaafikiane na utaratibu wa Kiswahili, irabu huchopekwa au kuingizwa katika baadhi ya sehemu za neno ambazo zina konsonanti. Kwa mfano;

| Kiingereza | | Kiswahili |
|---|---|---|
| 1. Ticket | ⟹ | tiketi |
| 2. Chalk | ⟹ | chaki |

| Kiarabu | | Kiswahili |
|---|---|---|
| 1. Maalum | ⟹ | maalumu |
| 2. Dhulma | ⟹ | dhuluma |

**3. Tabdili**

Haya ni mabadiliko yanayohusisha sauti mbili ambazo ziko karibu au zina ujirani hubadilishana nafasi. Hii ina maanisha kuwa fonimu moja huchukua nafasi ya fonimu nyingine katika neno

Mount Kenya University

fulani.Mfano mzuri ni mifano ya sauti za maneno ya Kiarabu ambayo yamekopwa na kuingizwa katika lugha ya Kiswahili hubadilishana nafasi katika neno husika. Kwa mfano;

a) Ihsa:n ⟹ hisani
b) Ikhtila:f ⟹ hitilafu

Maneno haya yamebadilisha baadhi ya fonimu zake ili kuchukua muundo na utaratibu wa lugha ya Kiswahili.

### 4.9.2 Mikondo ya Kimofofonolojia ya Lugha ya Kikuyu

Tafiti mbalimbali zinaonyesha kuwa lugha ya Kikuyu ilivyo lugha zingine ikiwemo lugha ya Kiswahili hudhihirisha mifanyiko mbalimbali ya kimofofonolojia.Mifanyiko hii ya lugha ya Kikuyu ni pamoja na;

1. Kuimarika kwa konsonanti
2. Muungano wa konsonanti
3. Usimilisho pamwe wa nazali
4. Kudondoshwa kwa irabu
5. Uchopekaji wa irabu
6. Usimilisho

**1. Kuimarika kwa Konsonanti**

Katika isimu, kuimarika kwa sauti kunahusisha ongezeko la nguvu ya muundo katika sauti.Kuimarisha konsonanti huonekana iwapo kuna utolewaji wa sauti.

Katika lugha ya Kikuyu, sauti /t/ na /k/ huimarika na kuwa /g/.

Mfano;

| Neno | maana | muundo | neno | muundo | maana |
|---|---|---|---|---|---|
| koma | lala | /n+koma/ | gome | /γome/ | nilale |
| kora | pata | /n+kora/ | gore | /γore/ | mnipate |
| tema | kata | /n+tema/ | gŪtema | /γutema/ | kukata |

1. **Usimilisho**

Njogu na wenziwe (2006) wanafasili usimilisho kuwa ni hali ambayo sauti moja huweza kuathiri sauti nyingine hadi ziweze kufanana kwa kiasi fulani. Sehemu ya sauti za lugha ya Kikuyu huweza kuathiriana mfano, vokali husimilishwa zikakaribia nazali /n/ na /m/,

| Neno | maana | muundo | neno | muundo wa kifonetiki | maana |
|---|---|---|---|---|---|
| tega | tega | /mu+tega/ | mŪtego | (mŪtego) | mtego |
| cama | onja | /mu+cama/ | mŪcama | (mŪcamo) | muonjo |

2. **Udondoshaji wa Vokali**

Huku ni kuachwa kwa sauti fulani wakati sauti mbili zinakutana. Massamba (2009) anafasili kudondosha sauti kuwa ni utaratibu wa kuondoa kipengele fulani cha isimu kwenye kirai, silabi, neno na kishazi. Lugha ya Kikuyu inadododosha irabu /a/ kwenye sehemu ya maneno.Kwa mfano;

| Neno | maana | udondoshaji | maana |
|---|---|---|---|
| /nina/ | maliza | /ninÎtɛ/ | nimemaliza |
| /Ūka/ | kuja | /ŪkÎtɛ/ | umekuja |

| | | | |
|---|---|---|---|
| /ruga/ | pika | /dugȋtɛ/ | nimepika |

3. **Muungano wa Sauti**

Huu ni mfanyiko wa kuunganisha sehemu mbili ambazo zina sifa bainifu.Muungano wa sauti huhusisha uhawilishaji wa sauti na pia upunguzaji.Hata hivyo, hakuna ushahidi uliowekwa wazi kuonyesha kuwa muungano na aina zake tofauti tofauti zinapaswa kuonekana kama uhawilishaji unaofuatwa na upunguzaji.Lugha ya Kikuyu huwa na muungano wa konsonanti na unazalishaji pamwe.

Mfano wa muungano wa konsonanti.

**Sauti /r/ na /t/ huunganishwa na /n/ kuunda /nd/**

Mfano;

| Kiswahili | Kikuyu | muundo |
|---|---|---|
| kata | [ tema] | [dɛmɛtɛ] |
| lea | [rɛra] | [dɛrɛtɛ] |

**Unazalishaji Pamwe**

Mfano;

| Neno | maana | muundo | neno | muundo | maana |
|---|---|---|---|---|---|
| cina | choma | /n+ʃina/ | njine | [dzine] | imechomeka |
| caria | tafuta | /n+ʃaria/ | njarie | [dzarie] | tafuta kitu maalum |
| ciuria | swali | /n+ʃiuria] | njuria | [ndzuria] | niulize |

Mount Kenya University

katika mifano hii, /s/ huungana na /n/ kuunda /ndz/.

4. **Kuchopeka**

Massamba (2009) anadai kwamba kuchopeka ni kuingiza kiyeyusho, vokali ama konsonanti katika neno.Kuchopeka ni pale ambapo kitamkwa fulani huingizwa kwenye mpangilio fulani wa vipashio ambavyo tayari vipo kwenye neno fulani. Katika lugha ya Kikuyu, vokali /i/ huongezwa kabla ya vokali /a/ katika konsonanti zifuatao; /d/, /k/, /m/, /r/, /h/.

Mfano;

| Neno | muundo | maana | neno | muundo | maana |
|---|---|---|---|---|---|
| hitha | [hida] | ficha | hithia | [hidia] | kuficha |
| nyita | [nita] | shika | nyitia | [nitia] | kaza |

## 4.10 Kipengele Cha Makosa

Corder (1967) anadai kuwa kufanya makosa katika lugha ni jambo lisilo la ajabu jinsi ilivyo unapojifunza aina yoyote ya jambo.Anasema kuwa, watu hufanya makosa wanapojifunza lugha ya pili. Ellis(1997) anafasili makosa ya lugha kwa kusema kwamba ni miundo ya kimaongezi na pia kimaandishi ambayo inakiuka kaida na sheria za lugha ambayo mtu anajifunza.Hii ina maana kuwa, kazi ya mwanagenzi anayejifunza lugha inadaiwa kuwa na makosa kama lugha yake ina utofauti wowote na muundo sahihi ambao unakubalika wa lugha ya pili ambayo mwanagenzi huyu anajifunza. Ellis (2003) anasema kwamba makosa ni hali ambapo mwanagenzi hukiuka kaida na taratibu wakati anajifunza lugha. Kwa hivyo, makosa hutokea mwanagenzi anayejifunza lugha anapokosa kuzingatia kanuni na kaida zilizopo katika lugha lengwa.Richard na wenziwe (2002) wanasema kwamba makosa ni matumizi ya lugha kwa njia mzawa wa lugha hiyo atasema kuwa si

sahihi.Kulingana na maelezo ya wanaisimu hawa, tutakubaliana kuwa ni mzawa wa lugha ama mtu aliye na umilisi wa lugha fulani ataweza kubaini makosa kwenye lugha ya pili ama lugha lengwa.Kamusi ya Kiswahili Fasaha (2010) inaeleza makosa kwa kusema kuwa ni hali ama jambo lisilokubalika kitaratibu ama kisheria ndani ya ustaarabu na desturi za jamii maalumu.Kwa hivyo, ni sahihi kusema kuwa makosa huwa yanatokea wakati ambapo kaida na kanuni ambazo zimewekwa hazijatiliwa maanani.Kwa kuwa utafiti huu wetu unahusu makosa ya kifonolojia na kimofolojia basi tutajikita kwenye makosa ya kifonolojia na kimofolojia katika lugha.

Kwa mujibu wa Ellis (1994), hali ya makosa huchimbukia katika umilisi alionao mwanagenzi na ruwaza maalumu.Umilisi unafasiriwa kama ujuzi alionao mzawa asilia wa lugha maalumu ambao anao juu ya lugha yake hii. Huu ni ujuzi unaomwezesha kuzalisha na kuunda tungo nyingi ajabu. Tukizingatia maelezo haya basi sababu kuu ya mwanagenzi kufanya makosa katika lugha fulani huwa ni bado mwanagenzi huyu hajapata ujuzi kamili katika lugha anayojifunza.

Gass & Selinker (2008) wanadai kwamba hali ya makosa kwenye kazi za wanagenzi huweza kuonekana na kutambuliwa tu na mwalimu au mtafiti.Mwanafunzi mwenyewe hawezi kutambua makosa haya, hii ni kwa sababu mwanagenzi mwenyewe huwa bado hajazielewa vizuri kaida na kanuni za lugha anayojifunza.Cook (1992) naye akitoa mchango wake katika suala hili la makosa anasema kuwa athari ya mwanzo kabisa kwenye lugha ya pili hutokea kwa sababu ingawa mwalimu hutumia juhudi nyingi katika kufundisha lugha ya pili, wanagenzi huwa tayari wamepata umilisi wa lugha yao ya kwanza akilini mwao.Kwa maana hii, mwanagenzi hutumia ujuzi ambao anao kutoka lugha aliyo nayo ya kwanza ndani ya lugha ya pili anayojifundisha.

Aina mbalimbali za makosa nazo zimefanyiwa utafiti na wataalamu tofautitofauti ambao wanaeleza kwamba makosa ambayo yanatokana na lugha ya kwanza huathiri lugha ya pili.

Richard (1974) anabainisha makosa ya aina mbili; makosa ambayo hutokana na athari ya lugha ya kwanza kwenye lugha ya pili na makosa yanayotokana na lugha ya pili yenyewe.Mwanagenzi huwa anafanya makosa haya kwa vile hajajifunza na kufahamu kwa ukamilifu kanuni na kaida zilizopo kwenye lugha ya pili ambayo anajifunza.

### 4.11 Makosa ya Kifonolojia Katika Lugha ya Kiswahili

**Kuchopeka Fonimu**

Jinsi tulivyoelezea hapo juu, kuchopeka fonimu ni kuongeza kipashio cha kifonolojia kwenye sehemu ambapo hakistahili kuwa.

1. **Kuchopeka Fonimu /u/ katika baadhi ya maneno**

   Baadhi ya wanagenzi walio na asili ya lugha ya Kikuyu wanaojifunza lugha ya Kiswahili waliweza kuchopeka sauti /u/ katika kiambishi cha kuwakilisha hali ya umoja /m/ katika nomno za ngeli ya u-I na pia katika viwakilishi nafsi.Kwa mfano;

**Jedwali 1.11.1: Mifano ya maneno yaliyochopeka fonimu /u/**

| **Umbo la neno lisilo sahili** | **umbo la neno lililo sahihi** |
|---|---|
| muchele | mchele |
| muhubiri | mhubiri |
| mudogo | mdogo |
| mupango | mpango |

| | |
|---|---|
| muke | mke |
| muzuri | mzuri |
| muheshimiwa | mheshimiwa |
| niliamuka | niliamka |
| akishutuka | akishtuka |

Sababu kuu ya kutokea kwa kosa hili katika kazi za wanagenzi wa Kiswahili wenye asili ya lugha ya Kikikuyu ni utofauti wa kifonolojia baina ya lugha ya Kikuyu na lugha ya Kiswahili. Katika lugha ya Kikuyu silabi nyingi huchukua muundo wa Konsonanti Vokali (KI) ambao ni muundo wa silabi pendwa ilhali kwenye lugha ya Kiswahili baadhi ya nomino katika ngeli ya U-I hudondoshwa irabu hiyo ya u/.Hili hutokea ili matamshi yaweze kurahisishwa na kuondoa hali ya konsonanti mbili kufuatana.

**Kuchopeka Fonimu /i/ katika baadhi ya maneno**

Baadhi ya wanagenzi waliweza kuongeza irabu /i/ katika konsonanti.Kwa mfano;

**Jedwali 4.11.2: Mifano ya maneno aliyochopeka fonimu /i/**

| Muundo usio sahihi | Muundo ulio sahihi |
|---|---|
| bisikuti | biskuti |
| baisikeli | baiskeli |

| | |
|---|---|
| inje | nje |
| inchi | nchi |
| raisi | rais |
| asikari | askari |

Kosa hili la kuchopeka fonimu/i/ linajitokeza kwa sababu ya miundo tofauti ya silabi baina ya lugha ya Kikuyu na ile ya Kiswahili. Hii ni kwa kuwa kwenye lugha ya Kikuyu ni vigumu kupata silabi ambayo ina muundo wa silabi funge lakini katika lugha ya Kiswahili sehemu ya nomino ambazo zimetokana lugha nyingine huchukua muundo wa silabi funge.Hivyo, wanafunzi walifanya kosa hili wakijaribu kuunda silabi pendwwa ya Konsonanti Irabu (KI) na pia ili kurahisisha matamshi ya maneno hayo.

**Kuchopeka Fonimu /h/**

Baadhi ya wanagenzi walichopeka konsonanti /h/ katika sehemu ya maneno ya Kiswahili. Kwa mfano;

**Jedwali 4.11.3: Mfano wa neno lililochopekwa fonimu /h/**

| **Muundo usio sahihi** | **Muundo sahihi** |
|---|---|
| harusi | arusi |

Ingawa kosa hili halikujitokeza sana kwa sababu lugha zote mbili zina fonimu /h/.Kwa hivyo wanagenzi ambao walidhihirisha kosa hili ni wale ambao hawajamudu Kiswahili vizuri.

**Kuchopeka Kiyeyusho /y/ au /w/**

Baadhi ya wanagenzi wanachopeka viyeyusho katika sauiti ambazo ni za irabu.Kwa mfano;

**Jedwali 4.11.4: Mifano ya maneno yaliyochopekwa kiyeyusho**

| **Muundo usio sahihi** | **Muundo ulio sahihi** |
|---|---|
| peya | pea |
| ambiya | ambia |
| kuwa | kua |
| owa | oa |
| walifurahiya | walifurahia |
| matokeyo | matokeo |
| nilimkimbiliya | nilimkimbilia |

Sababu za wanagenzi hawa kuchopeka fonimu /y/ au /w/ katika sauti ambazo ni irabu ni ili kuunda silabi pendwa yenye muundo wa Konsonanti Irabu (KI) na sababu nyingine ni kusahilisha matamshi.

**Kudondosha Fonimu**

Mount Kenya University

Hii ni hali ya kutowekwa kwa fonimu fulani au kuwachwa kwa kipashio fulani cha isimu kwenye neno, silabi, kirai au kishazi.Wanagenzi hawa walidhihirisha kudondoshwa kwa fonimu mbalimbali katika silabi za maneno.

**Kudondosha Fonimu /h/**

Wanagenzi kadhaa waliweza kudondosha fonimu /h/ katika baadhi ya maneno ambayo yana fonimu hiyo. Kwa mfano;

**Jedwali 4.11.5: Mifano ya maneno yaliyodondoshwa fonimu /h/**

| **Muundo usio sahihi** | **Muundo ulio sahihi** |
|---|---|
| aya | haya |
| iyo | hiyo |
| ata | haya |
| iyo siku | Hiyo siku |
| araka | haraka |
| apo | hapo |
| atawai | hatawahi |
| alafu | halafu |
| asubui | asubuhi |

Wanagenzi hawa walidondosha konsonanti /h/ kwenye baadhi ya maneno. Hii ni kwa sababu udondoshaji huu ni juhudi za wanagenzi husika kusahilisha miundo ya maneno ya lugha lengwa ili kurahisisha mawasiliano yao.

**Kudondosha Irabu /a/**

Kutokana na data ambayo tulikusanya, ilithibitishwa kuwa baadhi ya wanagenzi walidondosha irabu /a/ katika baadhi ya maneno.Kwa mfano;

**Jedwali 4.11.6: Mifano ya maneno yaliyodondoshwa irabu /a/**

| **Muundo usio sahihi** | **Muundo ulio sahihi** |
|---|---|
| akaniambi | akaniambia |
| sakumi | Saa kumi |
| yani | yaani |
| ikanzia | ikaanzia |
| zikanza | zikaanza |
| wakanionyesh | wakanionyesha |
| isiyofa | isiyofaa |
| mta | mtaa |
| nikawambia | nikawaambia |

Mount Kenya University

| | |
|---|---|
| wameanda | wameandaa |
| hakukata | hakukataa |

Sababu kuu ya wanagenzi kudondosha fonimu /a/ katika baadhi ya maneno ni athari ya lugha ya Kikuyu kwa lugha ya Kiswahili. Hii ni kwa vile maneno mengi ya lugha ya Kikuyu hayana irabu /a/ inayofuatana.Sababu nyingine ya wanagenzi hawa kufanya kosa hili ni kusahilisha matamshi na maandishi kwa muktadha huu.

**Kudondosha Fonimu /i/**

Inadhihirika kwamba katika maneno ambayo irabu /i/ zilifuatana, wanagenzi wengi walidondosha irabu /i/ moja na hivyo kutatiza matamshi na hata maana ya neno husika.Kwa mfano;

**Jedwali 4.11.7: Mifano ya maneno yaliyodondoshwa fonimu/i/**

| **Muundo usiofaa** | **Muundo unaofaa** |
|---|---|
| walimba | waliimba |
| aliba | aliiba |

Sababu kuu ya makosa ya kudondosha irabu /i/ ni kurahisisha matamshi ambayo ni athari ya lugha ya Kikuyu kwenye lugha ya Kiswahili.

**Kutumia Fonimu Mbadala**

Haya ndiyo makosa makuu yaliyojitokeza kwenye insha za wanafunzi hawa walio na asili ya lugha ya Kikuyu katika lugha ya Kiswahili.Asilimia kubwa ya makosa yalikuwa ya kutumia fonimu mbadala.

**Kutumia Fonimu /r/ mahali pa /l/**

Wanafunzi wengi walidhihirisha kosa hili katika kazi zao.Kwa mfano;

**Jedwali 4.11.8: Mifano ya maneno yaliyotumia fonimu /r/ badala ya /l/**

| **Muundo usiofaa** | **Muundo unaofaa** |
|---|---|
| pahari | pahali |
| kura | kula |
| vigeregere | vigelegele |
| warikaribishwa | walikaribishwa |
| baiskeri | baiskeli |
| wamekura | wamekula |
| turibaki | tulibaki |
| walisaria | walisalia |

Mount Kenya University

| | |
|---|---|
| asari | asali |
| kuwarinda | kuwalinda |
| serekari | serekali |
| ajari | ajali |
| sheira | sheila |
| rori | lori |
| tumbiri | tumbili |
| arafu | alafu |
| irifika | ilifika |

Sababu kuu ya kosa hili kutokea baina ya wanagenzi wa Kiswahili wenye asili ya lugha ya Kikuyu ni kwa kuwa hakuna fonimu /l/ katika lugha ya Kikuyu.Kwa hivyo wakati walihitajika kutumia fonimu /l/ katika maandishi yao walijikuta wakitumia fonimu /r/.

**Kutumia Fonimu /l/ mahali pa /r/**

Baadhi ya wanafunzi waliweza kutumia sauti ya /l/ mahali ambapo panafaa kuwa na sauti /r/.Kwa mfano;

**Jedwali 4.11.9: Mifano ya maneno yaliyotumia /l/ badala ya /r/**

| Muundo usiofaa | Muundo unaofaa |
|---|---|

| | |
|---|---|
| askali | askari |
| gali | gari |
| kutayalisha | kutayarisha |
| kujitayalisha | kujitayarisha |
| kasilika | kasirika |
| sikuyatalajia | sikuyatarajia |
| watalajia | watarajia |
| ndelemo | nderemo |
| langi | rangi |
| alaka | haraka |
| kalibu | karibu |
| alifulahia | alifurahia |

Sababu kuu ya wanagenzi hawa kufanya kosa hili ni kutokana na kuchanganyikiwa ni wapi watumie fonimu /l/ au fonimu /r/ kwani lugha ya Kikuyu haina fonimu /l/ hivyo kuishia kufanya kosa hili.

**Matumizi ya Fonimu /s/ mahali pa Fonimu /sh/**

Baadhi ya wanagenzi walitumia fonimu /sh/ walipokumbana na maneno yenye fonimu /s/. Kwa mfano;

**Jedwali 4.11.10: Mifano ya maneno yaliyotumia /s/ badala ya /sh/**

| **Muundo usiofaa** | **Muundo unaofaa** |
|---|---|
| serehe | sherehe |
| serekea | sherehekea |
| kisa | kisha |
| tuose | tuoshe |
| ametayalisa | ametayarisha |

Wanagenzi walitumia /s/ badala ya /sh/ kwa sababu sauti /sh/ haipatikani katika muundo wa lugha ya Kikuyu.Hii inasababisha baadhi ya wanagenzi kutumia fonimu hii kiholela bila kujua ni wapi sahihi kuitumia.

**Matumizi ya Fonimu /sh/ mahali pa Fonimu /s/**

Wanagenzi wachache walidhihirisha kosa hili.Kwa mfano;

**Jedwali 4.11.11: Mifano ya maneno yaliyotumia /sh/ badala ya /s/**

| **Muundo usiofaa** | **Muundo unaofaa** |
|---|---|
| shauti | sauti |
| | |

Mount Kenya University

Sababu kuu ya kosa hili ni kwa sababu fonimu/sh/ haipatikani katika lugha ya Kikuyu hivyo mwanagenzi huchanganyikiwa ni wapi atumie /sh/ au /s/ kama ilivyoelezewa katika kosa lililopo hapo juu.

**Matumizi ya Fonimu /d/ mahali pa /nd/**

Baadhi ya wanagenzi walitumia fonimu /d/ mahali pa fonimu /nd/ katika kazi zao.Kwa mfano;

**Jedwali 4.11.12: Mifano ya maneno yaliyotumia /d/ badala ya /nd/**

| **Muundo usiofaa** | **Muundo unaofaa** |
|---|---|
| saduku | sanduku |
| deremo | nderemo |
| dani | ndani |
| yalidodoka | yalidondoka |
| madizi | mandizi |
| Omodi | Omondi |
| dimi | ndimi |

Kwenye lugha ya Kikuyu fonimu /d/ hunazalishwa na kutamkwa /nd/.Hivyo wanagenzi hawa waliathirika kutokana na lugha hii yao ya kwanza na kuishia kufanya kosa hili.

Mount Kenya University

**Matumizi ya Fonimu /nd/ mahali pa Fonimu /d/**

Baadhi ya wanagenzi walitumia /nd/ badala ya /d/ katika baadhi ya maneno.Kwa mfano;

**Jedwali 4.11.13: Mifano ya maneno yaliyotumia /nd/ badala ya /d/**

| **Muundo usiofaa** | **Muundo unaofaa** |
|---|---|
| kindogo | kidogo |
| wakarundi | wakarudi |
| kurundi | kurudi |
| ikindondoka | ikidondoka |
| nilimsaindia | nilimsaidia |
| munda | muda |
| zawandi | zawadi |

Kama mtafiti alivyosema hapo juu, fonimu /d/ hutamkwa kama /nd/ kwa hivyo wanagenzi ambao walifanya kosa hili walichanganyikiwa ni wapi watumie /d/ au /nd/ katika uandishi wao na hivyo kuishia kufanya kosa hili.

**Kutumia Fonimu /b/ mahali pa Fonimu /mb/**

Kuna baadhi ya wanagenzi ambao walifanya kosa la kutumia fonimu /b/ badala ya fonimu /mb/ kwenye insha zao. Mfano wa makosa haya:

**Jedwali 4.11.14: Mifano ya maneno yaliyotumiwa /b/ badala ya /mb/**

| Muundo usiofaa | Muundo unaofaa |
|---|---|
| nyubani | nyumbani |
| boga | mboga |
| maobi | maombi |
| kukubukwa | kukumbukwa |
| bona | mbona |
| wakaniabia | wakaniambia |
| shaba | shamba |

Sababu ya kutokea kwa kosa hili katika insha za baadhi ya wanagenzi ni kwa sababu katika lugha ya Kikuyu, fonimu/b/ hutamkwa kama /mb/ na kwa sababu hii wanagenzi hawa waliathirika kutokana na lugha yao ya kwanza.

**Matumizi ya Fonimu /mb/ mahali pa Fonimu /b/**

Baadhi ya wanagenzi walidhihirisha kosa hili katika kazi zao ambazo waliandika. Mfano;

**Jedwali 4.11.15: Mifano ya maneno yaliyotumia fonimu /mb/ badala ya /b/**

| Muundo usiofaa | Muundo unaofaa |
|---|---|
| nikambemba | nikabeba |
| msimba | msiba |
| mbora | bora |
| kuimba | kuiba |
| waliniimbia | waliniibia |
| mbarambara | barabara |
| niliimbuka | niliibuka |

Sababu ya kosa hili kutokea ni kwa kuwa katika lugha ya Kikuyu /b/ hutamkwa kama /mb/ ilhali katika lugha ya Kiswahili sanifu kuna fonimu zote mbili.Kwa hivyo, wanagenzi hawa walichanganyikiwa ni wapi watumie /mb/ na wapi watumie /b/ na hivyo kuishia kufanya kosa hili.

**Matumizi ya /g/ mahali pa /ng/**

Wanagenzi wengine walishindwa kutofautisha fonimu /g/ na /ng/ na hivyo kuishia kutumia /g/ mahali palistahili kutumiwa fonimu /ng/.Kwa mfano;

**Jedwali 4.11.16: Mifano ya maneno yaliyotumia /g/ badala ya /ng/**

| Muundo usiofaa | Muundo unaofaa |
|---|---|

| | |
|---|---|
| ragi | rangi |
| kugogwa | kugongwa |
| machugwa | machungwa |
| wamenigoja | wameningoja |
| megine | mengine |

Sababu kuu ya kosa hili kutokea ni mfumo tofauti wa kimofofonolojia kati ya lugha ya Kiswahili na ile ya Kikuyu na kwa huvyo, wanagenzi walishindwa ni wapi watumie /g/ na wapi watumie /ng/ kwani sauti hizi hutamkwa karibu sawia.

**Matumizi ya Fonimu /ng/ mahali pa /g/**

Baadhi ya wanagenzi walidhihirisha kosa hili katika insha zao.kwa mfano;

**Jedwali 4.11.17: Mifano ya maneno yaliyotumia /ng/ mahali pa /g/**

| Muundo usiofaa | Muundo unaofaa |
|---|---|
| virango | virago |
| mdongo | mdogo |
| kindongo | kidogo |

Mount Kenya University

| | |
|---|---|
| tuliangizwa | tuliagizwa |

Kama tulivyojadili hapo juu, sababu ya kutokea kwa kutokea kwa kosa hili ni mfumo tofauti wa kimofofonolojia baina ya lugha ya Kiswahili na ile ya Kikuyu kwani sauti hizi mbili hutamkwa karibu sawa kwenye lugha ya Kikuyu na hivyo basi mwanagenzi alichanganyikiwa ni wapi atumie /g/ na wapi atumie /ng/.

**Matumizi ya Fonimu /nj/ mahali pa Fonimu /j/**

Baadhi ya insha za wanagenzi hawa zilionyesha kosa hili.Kwa mfano;

**Jedwali 4.11.18: Mifano ya maneno yaliyotumia /nj/ badala /j/**

| Muundo usiofaa | Muundo unaofaa |
|---|---|
| walikunja | walikuja |
| kukunja | kukuja |
| wakunje | wakuje |

Mount Kenya University

Sababu ya wanagenzi kufanya kosa hili ni kwa sababu ya mifumo tofauti ya kimofofonolojia baina ya lugha ya Kiswahili na ile ya Kikuyu.Katika lugha ya Kikuyu, fonimu /j/ hutamkwa kama /nj/, hivyo wanagenzi waliodhihirisha kosa hili waliathiriwa na lugha yao ya kwanza.

**Kutumia Fonimu /s/ mahali pa /z/**

Kosa hili halikujitokeza sana katika kazi za wanagenzi hawa.Mfano:

**Jedwali 4.11.19: Mifano ya maneno yaliyotumia /s/ badala ya /z/**

| Muundo usiofaa | Muundo unaofaa |
|---|---|
| wasasi | wazazi |
| malisa | maliza |

Sababu ya kosa hili kutokea ni kwa kuwa lugha ya Kikuyu haina /s/ na /z/ na kwa hivyo wanagenzi waliofanya kosa hili walichanganyikiwa kiasi ni wapi watumie /s/ na wapi watumie /z/.

**Kutumia Fonimu /sh/mahali pa /ch/**

Kuna kazi ambayo ilidhihirisha kosa hili. Kwa fano:

**Jedwali 4.11.20: Mifano ya maneno yaliyotumia /sh/ badala ya /ch/**

| Muundo usiofaa | Muundo unaofaa |
|---|---|
| mshele | mchele |

Hili ni kosa linalotokana na taathira ya lugha ya kwanza kwa sababu katika lugha ya Kikuyu fonimu /ch/ hutamkwa /sh/ kwa vile hakuna fonimu /sh/ kwenye lugha ya Kikuyu.



Mount Kenya University

## 4.12 Makosa ya Kimofolojia

Kutokeapo makosa ya kifonolojia katika neno, bila shaka makosa hayo huathiri mofolojia ya neno husika.Katika uchunguzi huu wetu, tuligundua kuwa wanagenzi wa shule za sekondari wenye asili ya lugha ya Kikuyu kwenye kaunti hii ndogo ya Kahuro, jimbo la Murang'a ambao wanajifunza lugha ya Kiswahili ikiwa lugha yao ya pili walifanya makosa ya udondoshaji, uchopekaji, uyeyushaji, ubadilishanaji wa vipashio na pia kubadili mpangilio wa vipashio katika neno.

**Kudondosha Vipashio**

**Kudondosha Irabu /a/**

Baadhi ya wanagenzi walidondoa irabu /a/ katika maneno yaliyo na irabu zinazofuatana.Kwa mfano;

**Jedwali 4.12.1: Mifano ya maneno yaliyodondoshwa irabu /a/**

| **Neno lenye kosa** | **Neno sahihi** |
|---|---|
| nimeja | nimejaa |
| yani | yaani |
| sakumi | Saa kumi |
| akaniambi | akaniambia |
| mishani | maishani |
| mta | mtaani |

| | |
|---|---|
| niliwaga | niliwaaga |
| kinaendele | kinaendelea |
| nikamua | nikaamua |
| mgaga | mgaagaa |

Sababu kuu ya kosa hili kutokea ni kujaribu kuunda silabi pendwa ya konsonanti-irabu na kurahihisha matamshi na mawasiliano.

**Kudondosha Irabu /e/**

Baadhi ya wanagenzi walidondosha irabu /e/ mahali ambapo irabu hii ilifuatana katika neno.Kwa mfano;

**Jedwali 4.12.2: Mifano ya maneno yaliyodondoshwa irabu /e/**

| **Neno lenye kosa** | **Neno sahihi** |
|---|---|
| peke | pekee |
| kipeke | kipekee |

Sababu kuu ya kosa hili ni wanafunzi kujaribu kuunda silabi pendwa ya konsonanti- irabu.

**Kudondosha Irabu /i/**

Mount Kenya University

Baadhi ya wanagenzi walidondosha irabu /i/ katika maneno ambapo irabu hii ilifuatana na irabu nyingine.

**Jedwali 4.12.3: Mifano ya maneno yaliyodondoshwa irabu /i/**

| **Neno lenye kosa** | **Neno sahihi** |
|---|---|
| hujingiza | hujiingiza |
| wamebuka | wameibuka |
| alye | aliye |
| tulisika | tulisikia |

Sababu ya wanafunzi kufanya kosa hili wanapoandika maneno ya lugha ya Kiswahili ni kuunda silabi pendwa ya konsonanti-irabu.

**Kudondosha /h/**

Baadhi ya wanagenzi walidondosha /h/ katika baadhi ya maneno.Kwa mfano;

**Jedwali 4.12.4: Mifano ya maneno yaliyodondoshwa /h/**

| **Neno lenye kosa** | **Neno sahihi** |
|---|---|
| asubui | asubuhi |
| sheree | sherehe |

Mount Kenya University

Kosa hili linasababishwa na athari ya lugha ya Kikikuyu hadi ile ya Kiswahili na tofauti za kimofofonolojia baina ya Kiswahili na lugha ya Kikuyu.Hii inatokea wanafunzi wakijaribu kusahilisha matamshi.

**Kudondosha Kiyeyusho /w/**

**Jedwali 4.12.5: Mifano ya maneno yaliyodondoshwa /w/**

| Neno lenye kosa | Neno sahihi |
|---|---|
| alikua | alikuwa |
| vilikua | vilikuwa |
| kua | kuwa |

Kosa hili linatokea wanafunzi wakirahisisha matamshi.

**Kudondosha Kiyeyusho /y/**

**Jedwali 4.12.6: Mifano ya maneno yaliyodondoshwa /y/**

| **Neno lenye kosa** | **Neno sahihi** |
|---|---|
| viombo | vyombo |
| waviele | wavyele |

Mount Kenya University

| | |
|---|---|
| walivio | walivyo |

Sababu ya kutokea kwa kosa hili ni kurahihisha matamshi na mawasiliano.

**Kudondosha Irabu /u/**

**Jedwali 4.12.7: Mfano wa neno lililodondoshwa /u/**

| **Neno lenye kosa** | **Neno sahihi** |
|---|---|
| akatuliza | akatuuliza |

Kosa hili lilitokea kwa sababu wanagenzi walikuwa wakijaribu kuunda silabi pendwa ya konsonanti-irabu.

**Kuchopeka Vipashio**

**Kuchopeka /ma/**

Wanagenzi walielekea kuongeza kipashio /ma/ ili kuweka nomino za ngeli ya i-zi katika hali ya wingi. Majina haya katika lugha ya Kiswahili hayachukui viambishi vya wingi.Mfano:

**Jedwali 4.12.8: Mifano ya maneno yaliyochopekwa /ma/**

| **Neno lenye kosa** | **Neno sahihi** |
|---|---|

Mount Kenya University

| | |
|---|---|
| manyumbani | nyumbani |
| manyasi | nyasi |
| mataa | taa |
| matakataka | takataka |
| marangi | rangi |

Kosa hili lilitokana na utofauti uliopo wa kimuundo baina ya lugha ya Kiswahili na ile ya Kikuyu kwani sehemu ya maneno ya Kiswahili hayachukui mofu ya wingi lakini yanachukua mofu ya wingi katika lugha ya Kikuyu.

**Kuchopeka Mofimu /ku/**

Hili lilitokea sanasana kwenye vitenzi vya silabi moja.Kwa mfano;

**Jedwali 4.12.9: Mifano ya maneno yaliyochopekwa /ku/**

| **Neno lenye kosa** | **Neno sahihi** |
|---|---|
| kukula | kula |
| kukufana | kufana |
| kukuja | kuja |

| | |
|---|---|
| wakuje | waje |

Kosa hili linatokea kwa sababu ya wanagenzi kujumuisha kanuni za lugha ya Kiswahili.

**Kuchopeka Kiambishi Tamati /ni/ kwenye Baadhi ya Majina**

Baadhi ya wanagenzi walichopeka /ni/ mwishoni mwa nomino.kwa mfano;

**Jedwali 4.12.10: Mifano ya maneno yaliyochopekwa /ni/**

| **Neno lenye kosa** | **Neno sahihi** |
|---|---|
| nchini | nchi |
| upishini | upishi |
| langoni | lango |

Sababu ya kutokea kwa kosa hili ni taathira ya lugha ya Kikuyu kwenye lugha ya Kiswahili.

**Kuchopeka Viambishi Ngeli Visivyofaa**

Baadhi ya wanagenzi walichopeka kiambishi/m/ katika maneno yasiyochukuwa viambishi ngeli katika lugha ya Kiswahili.

**Jedwali 4.12.11: Mfano wa neno ambalo lilichopekwa /m/**

Mount Kenya University

| Neno lenye kosa | Neno sahihi |
|---|---|
| msafi | safi |

Sababu ya kutokea kwa kosa hili ni mwanagenzi kujumuisha sheria za lugha ya Kiswahili.

**Kuchopeka Viambishi vya Wingi kwenye Maneno Mkopo**

Baadhi ya wanagenzi pia walichopeka vipashio vya wingi kwenye maneno ya Kiswahili yaliyokopwa. Kwa mfano;

**Jedwali 4.12.12: Mfano wa neno lililochopekwa viambishi vya wingi**

| Neno lenye kosa | Neno sahihi |
|---|---|
| wanapolisi | polisi |

Kosa hili limetokana na utofauti wa miundo ya maneno ya Kiswahili na ya Kikuyu.Baadhi ya maneno ya Kiswahili hayachukui mofu ya wingi lakini katika lugha ya Kikuyu maneno yayo hayo huchukua viambishi vya wingi.

**Kuongeza Kiambishi Tamati /ng/ katika Vitenzi Kuonyesha Mazoea**

Sehemu ya wanagenzi huchopeka kiambishi tamati /ng/ kuonyesha mazoea katika vitenzi.

**Jedwali 4.12.13: Mifano ya maneno yaliyoongezewa kiambishi tamati /ng/**

| **Neno lenye kosa** | **Neno sahihi** |
|---|---|
| ninawapendanga | ninawapenda |
| niliwashukurungu | niliwashukuru |

Kosa hili linatokana na taathira ya lugha ya Kikuyu kwenye lugha ya Kiswahili ambapo /ng/ huongezwa kwenye kitenzi kuonyesha hali ya mazoea.

**Kutumia Vipashio Mbadala**

**Kutumia /l/ mahali pa /r**

Sehemu ndogo ya wanagenzi pia ilidhihirisha kosa hili. Kwa mfano;

**Jedwali 4.12.14: Mifano ya maneno yaliyotumia /l/ mahali pa /r/**

| **Neno lenye kosa** | **Neno lililo sahihi** |
|---|---|
| sale | sare |
| kuzilai | kuzirai |
| makasiliko | makasiriko |
| kuselekea | kusherehekea |

Hili kosa linatokana na taathira ya lugha ya Kikuyu kwa lugha ya Kiswahili.

**Matumizi ya /th/ mahali pa /dh/**

Baadhi ya wanagenzi walitumia /th/ badala ya /dh/ katika maneno.



Mount Kenya University

**Jedwali 4.12.15: Mifano ya maneno yaliyotumia /th/ badala ya /dh/**

| Neno lenye kosa | Neno sahihi |
|---|---|
| tafathali | tafadhali |
| thahabu | dhahabu |
| ungethani | ungedhani |
| wangethani | wangedhani |

Kosa hili lilitokea kwa minajili ya tofauti za kimofofonolojia kati ya lugha ya Kikuyu na Kiswahili.Lugha ya Kikuyu haina /dh/ na /th/ hutamkwa kama /dh/.

**Kutumia /ka/ Badala ya /ki/ ili Kuweka Nomino katika Hali ya Udogo**

Katika kuandika udogo wa baadhi ya nomino na kuonyesha hali ya kudhalilisha, baadhi ya wanagenzi walitumia kipashio /ka/ badala ya kipashio /ki/. Kwa mfano;

**Jedwali 4.12.16: Mifano ya maneno yaliyotumia /ka/ badala ya /ki/**

| Neno lenye kosa | Neno sahihi |
|---|---|
| kanywaji | kinywaji |
| kasichana | kisichana |

Mount Kenya University

Kosa hili linatokana na taathira ya lugha ya Kikuyu kwa lugha ya Kiswahili kwani kwenye lugha ya Kikuyu nomino huwekwa kwenye hali ya udogo kwa kuongeza kiambishi /ka/ kuonyesha dharau.

**Kutumia /ng/ mahali pa /ng'/**

Baadhi ya wanagenzi walidhihirisha kosa hili. Kwa mfano;

**Jedwali 4.12.17: Mfano wa neno lililotumia /ng/ badala ya /ng'/**

| **Neno lenye kosa** | **Neno sahihi** |
|---|---|
| nilingangana | Niling'ang'ana |

Sababu ya kosa hili kutokea ni kurahihisha matamshi.

**Kutumia /c/ mahali pa /z/**

Baadhi ya wanagenzi walidhihirisha kosa hili.Kwa mfano;

**Jedwali 4.12.18: Mfano wa neno lililotumia /c/ badala ya /z/**

| **Neno lenye kosa** | **Neno sahihi** |
|---|---|
| kucuri | kuzuri |

Kosa hili lilitokana na taathira ya lugha ya Kikuyu kwenye lugha ya Kiswahili ambapo mwanagenzi alijaribu kutamka neno hili kwa kuzingatia mofofonolojia ya Kikuyu.



Mount Kenya University

**Kutumia Irabu Badala ya Viyeyusho**

Kosa hili lilitokea sana katika kazi za wanagenzi. Kwa mfano;

**Jedwali 4.12.19: Mifano ya maneno yaliyotumia irabu badala ya kiyeyusho.**

| **Neno lenye kosa** | **Neno sahihi** |
|---|---|
| vilikua | vilikuwa |
| vinyuaji | vinywaji |
| nyuele | nywele |
| namueleza | namweleza |
| muweza | mweza |
| tuende | twende |
| kuenda | kwenda |
| hakuenda | hakwenda |
| kumuombea | kumwombea |
| ngurue | nguruwe |
| suara | swara |
| kinya | kinywa |

Mount Kenya University

Hili kosa lilitokana na wanagenzi kujaribu kurahihisha matamshi.

**Kubadilisha Mpangilio wa Vipashio Katika Neno**

Baadhi ya wanagenzi walibadili mpangilio wa vipashio katika baadhi ya maneno waliyoyatumia katika insha zao. Kwa mfano;

**Jedwali 4.12.20: Mifano ya maneno yaliyobadilishwa mpangilio wa vipashio**

| Neno lenye kosa | Neno sahihi |
|---|---|
| kusheherekea | kusherehekea |
| nikawamibia | nikawaambia |

Kosa hili limesababishwa na taathia ya lugha ya Kikuyu kwenye ile ya Kiswahili kwani lugha ya Kikuyu huruhusu kubadilisha vipashio katika neno.

**Kubadilisha Mofu Katika Neno**

Baadhi ya wanagenzi walibadilisha mofu katika baadhi ya maneno. Kwa mfano;

**Jedwali 4.12.21: Mifano ya maneno yaliyobadilishwa mofu**

| Neno lenye kosa | Neno sahihi |
|---|---|
| kuifanya | kuufanya |

| | |
|---|---|
| kupenye | kupenya |
| waliengua | waliangua |
| waki | wake |
| tuliku | tulikuwa |

Kosa hili lilitokana na wanagenzi kutomakinika wakati wa kuandika na pia kutomudu lugha ya Kiswahili vizuri.

**Mnyambuliko Mbaya wa Vitenzi**

Kosa hili pia lilidhihirika kwenye baadhi ya insha za wanafunzi. Kwa mfano;

**Jedwali 4.12.22: Mfano wa neno lililonyambuliwa vibaya**

| **Muundo usiofaa** | **Muundo unaofaa** |
|---|---|
| Tulitembeshwa | Tulitembezwa |

Hili ni kosa ambalo lilitokana na baadhi ya wanagenzi kujumuisha kanuni za lugha ya Kiswahili.

## 4.13 Utathmini wa kiwango cha Makosa

Kulingana na falsafa ya Uchanganuzi Makosa yake Corder (1960), baada ya kuyaainisha makosa kwenye makundi tofauti tofauti na kuyaeleza, ni bora kuingia kwa hatua inayofuata ambayo ni kutathmini kiwango cha makosa katika kila kundi maalumu. Katika utafiti huu wetu, makosa yalipangwa kwenye makundi mawili makuu. Makundi haya ni;

a) Makosa ya kifonolojia

b) Makosa ya kimofolojia

Kisha makosa ya kifonolojia yalipangwa kwenye makundi matatu yaani makosa ya uchopekaji, makosa ya udondoshaji na makosa ya kubadilisha fonimu na makosa ya kimofolojia yalipangwa kwenye makundi matatu ambayo ni makosa ya uchopekaji, makosa ya udondoshaji, makosa ya na kutumia vipashio mbadala na kisha makosa katika kila kikundi yakabainishwa.

### 4.13.1 Makundi na Kiwango cha Makosa

**Makosa ya Kifonolojia**

**Jedwali 4.13.1: Kiwango cha Makosa ya Kifonolojia**

| **Aina ya makosa ya kifonolojia** | **Kuchopeka** | **Kubadilisha fonimu** | **Kudondosha** | **Jumla** |
|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya makosa** | 24 | 77 | 22 | 123 |
| **Asilimia ya makosa** | 19.5% | 62.6% | 17.9% | 100% |

**Makosa ya Kimofolojia**

**Jedwali 4.13.2: Kiwango cha Makosa ya Kimofolojia**

Mount Kenya University

| Aina ya makosa ya kimofolojia | kuchopeka | Kubadilisha vipashio | kudondosha | jumla |
|---|---|---|---|---|
| **Jumla ya makosa katika kila kikundi** | 16 | 31 | 26 | 73 |
| **Asilimia** | 21.9% | 42.5% | 35.6% | 100% |

**Jumla ya makosa ya Kimofofonolojia**

**Jedwali 4.13.3: Muhtasari wa jumla ya makosa ya kimofofonolojia**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Jumla ya makosa katika kila kundi | 24+16=**40** | 77+31=**108** | 22+26=**48** | **196** |
| **Asilimia** | 20.4% | 55.1% | 24.5% | 100% |

Kutokana na tathmini hii, ni bayana kuwa idadi kubwa ya makosa ya kimofofonolojia yaliyofanywa na wanagenzi ni ya kutumia vipashio mbadala ambapo makosa ya kutumia vipashio mbadala yalichukua asilimia 55.1%, yakafuatwa na makosa ya udondoshaji na makosa ya uchopekaji yakachukua nafasi ya tatu.Sababu kuu ya makosa ya kutumia vipashio mbadala ni kwa

vile lugha ya Kiswahili na ile ya Kikuyu zina miundo tofauti ya kimofofonolojia hivyo basi, athari ya Kikuyu kama lugha ya kwanza ya wanagenzi hawa inadhihirika katika kazi andishi za Kiswahili na kusababisha makosa ya kifonolojia na kimofolojia.

### 4.14 Sababu za Wanagenzi wa Shule za Upili Wenye Asili ya Lugha ya Kikuyu Kufanya Makosa Katika Kazi Andishi za Kiswahili

Kwa mujibu wa mhimili wa pili wa nadharia ya Uchanganuzi Makosa ni sharti kufafanua kilichosababisha makosa ya lugha. Kuna sababu kadhaa zinazopelekea wanagenzi wa shule za upili wenye asili ya lugha ya Kikuyu kufanya makosa ya kimofofonolojia wanapoandika Kiswahili katika jitihada zao za kujifunza lugha ya Kiswahili.

Kwanza, ni ruwaza tofauti wa sauti za Kikuyu na zile za Kiswahili.Katika sehemu ya uchanganuzi wa data hapo juu, tumeona kuwa wanagenzi walifanya makosa ya kifonolojia na kimofolojia walipokumbana na maneno yenye fonimu na mofimu ambazo hazimo katika lugha ya Kikuyu.

Pili, ni mifumo tofauti ya umofolojia baina ya lugha ya Kikuyu na ile ya Kiswahili. Kwa mfano, wanafunzi walichopeka kiambishi /ku/ mwanzoni mwa baadhi ya vitenzi vyenye silabi moja, pia walichopeka kiambishi tamati /ng/ kwenye vitenzi kuonyesha hali ya mazoea kama ilivyo katika lugha ya Kikuyu.

Tatu, ni matumizi ya lugha ya Kikuyu kwa muda mrefu miongoni mwa wanafunzi, walimu na jamii kwa jumla.Ilibainika kuwa wanafunzi hutumia tu lugha ya Kiswahili wakiwa shuleni na pindi tu wanapotoka shuleni wao huwa wanatumia lugha ya Kikuyu kwenye mazungumzo yao. Hali hii husababisha athari ya lugha ya Kikuyu katika Kiswahili hata wakiandika kwa kukosa kufanya mazoezi ya kuzungumza.

Nne, sehemu ya wanagenzi walitekeleza makosa kwa vile hawajamudu sheria za lugha ya Kiswahili ipasavyo kwa hivyo hawajui muundo upi wa kimofofonolojia ulio sahihi na upi usio sahihi hivyo kuishia kufanya makosa ya kimofofonolojia.

Sababu nyingine ni mbinu mbovu za kufundisha lugha ya pili.Hii ni kwa sababu wakufunzi wengi hawana ujuzi wa kutosha wa taaluma ya fonetiki.Kwa sababu hiii huishia kufunza vipengele vya kimofofolojia haraka na bila kufuata hatua ambazo zimependekezwa na wataalamu wa lugha ya pili.

**4.15 Mbinu za kurekebisha makosa ya kimofofonolojia kwenye kazi Andishi za Kiswahili Baina ya Wanagenzi Walio na Asili ya Lugha ya Kikuyu**

Mhimili wa nne unahusu kueleza mbinu zinazoweza kutumiwa kurekebisha makosa katika lugha ya wanafunzi wanaojifunza lugha ya pili. Wataalamu mbalimbali wa isimu wamependekeza kuwe na matumizi ya mbinu mseto tunapokabiliana na tatizo lolote la utokeaji wa makosa miongoni mwa wanagenzi ambao wanajifunza lugha ya pili.Kwa mfano mwanaisimu Sheen (2007) anatoa maoni yake kwa kupendekeza kwamba usahihishaji wa kilengo utumike tunaporekebisha makosa kwenye kazi andishi za wanagenzi.Mkufunzi anapotumia njia hii, yeye hujihusisha tu na aina moja ya kosa bila kushughulikia makosa mengine katika kazi za wanagenzi kwa wakati mmoja.Njia hii husaidia wanagenzi kumakinika zaidi ili kuweza kuepuka kosa hilo mahususi ambalo mkufunzi amelilenga.Aidha, wanagenzi wataweza kulitambua kosa husika na pia wataweza kulinganisha kazi zao. Sababu ya hali hii ni kuwa dhana fulani huweza kuwa wazi zaidi inapokuwa mahususi. Njia hii ya kushughulikia kosa moja maalum kwa wakati mmoja pia ni bora zaidi kutumika katika hali ambapo wakufunzi wana idadi kubwa ya wanagenzi, hivyo mkufunzi ataweza kuchaguwa makosa yale ambayo yanajitokeza zaidi katika kazi za wanagenzi.

Kwenye uchunguzi huu, pia ilibainika kwamba wanagenzi wa Kiswahili wa shule za upili wenye asili ya lugha ya Kikuyu walihamisha ruwaza ya lugha ya Kikuyu hadi katika ile ya Kiswahili walipokuwa wanaandika insha zao.Kwa tatizo kama hili, mtaalamu Ellis (1997) anasema kwamba wakufunzi waweze kutilia maanani vipengele ambavyo ni tofauti baina ya lugha ya kwanza na ile ya pili ambayo wanafunzi wanajifunza.Aidha, miundo ya lugha ya kwanza na lugha ya pili ilinganishwe kwa nia ya kubainisha na kutambua vipengele vinavyoweza kuwa vigumu kwa wanagenzi. Wataalamu Stockwell na wenzake (1968) wanadai kwamba ikiwa lugha mbili zina miundo inayofanana, itakuwa kazi rahisi kwa mwanagenzi kujielimisha lugha ya pili ilhali ikiwa lugha husika zina miundo iliyo tofauti basi ni dhahiri kuwa wanafunzi hao wataweza kupata shida kwenye sehemu ambazo miundo si sawa.Hivyo basi, inabidi miundo hii tofauti itiliwe maanani zaidi wakati wa kujifundisha lugha ya pili.

Pia, wanagenzi wanafaa wajifunze lugha ya pili kwa kutumia ngazi za ugumu wa makosa.Ulinganisho huu wa ugumu una uwezo wa kuwafaa kwa kiwango kikubwa wanagenzi wenye ufahamu wa juu wa lugha ya pili (Kong na Gast, 2009). Makosa yanayofaa kukosolewa na mkufunzi ni yale makosa ambayo mwanagenzi hana uwezo wa kujikosoa akiwa mwenyewe wala si makosa ambayo anaweza kujirekebisha mwenyewe.Mchango huu una upungufu kwa vile ni vigumu kwa mkufunzi kubaini na kutambua makosa ambayo mwanagenzi anaweza kujirekebisha mwenyewe na yale ambayo hawezi kujisahihisha binafsi.Hii ni kwa vile wanagenzi mbalimbali huwa na uwezo tofauti tofauti wa kujifunza lugha na pia vigezo vinavyoweza kutumiwa kutathmini aina za makosa haya mawili.

Mtafiti anapendekeza kuwa walimu katika maeneo haya ya Kahuro wafundishe kwa undani mifumo na ruwaza za sauti za lugha ya Kiswahili huku wakitilia maanani zile sauti ambazo hazimo katika lugha ya Kikuyu.Pia wakufunzi wawasaidie wanafunzi kubaini ukweli kuwa lugha hizo

mbili zina tofauti katika sauti ili kuweza kuzuia mazoea ya kuhamisha vipengele vya lugha ya Kikuyu hadi ya ile ya Kiswahili.

Mbinu nyingine ya kushughulikia makosa ya kimofofonolojia kwenye kazi andishi za wanagenzi, ni kutumia mikakati hii mitatu inayohusiana na muda wa urekebishaji wa makosa.Wanaisimu Allwright na Balley (1991) mikakati hii mitatu ya urekebishaji wa makosa.Wanasema kuwa mbinu hizi tatu hutegemea aina ya kosa na pia hali ya wanagenzi na wakufunzi.Hii inamaanisha kuwa baadhi ya mikakati itafaa wakati wa kuzungumza na nyingine itafaa katika mazungumzo na pia katika kazi andishi.Njia ya kwanza ni kutoa majibu ya papo kwa hapo ambapo mkufunzi humrekebisha mwanagenzi hapo bila kugonja kumrekebisha baadaye, yanaweza pia yakacheleweshwa hadi wakati mwafaka au yakaairishwa hadi baadaye.kwa kuelezea mbinu hizi, ukosoaji wa papo kwa hapo huweza kumsaidia mwanagenzi kulitambua kosa lake na hivyo kulirekebisha ingawa njia hii imepata pingamizi kutoka kwa baadhi ya wataalamu wa elimu, miongoni mwao ni Ur (1996) na Seedhouse (2004) ambao wanadai kuwa mbinu hii haifai kutumiwa katika darasa kwa sababu inaweza kumtoa mwanagenzi darasani kwa kusababisha aibu na pia kumwondoa kwa mada kuu ya mwalimu.Njia ya pili ni ambapo mkufunzi anangonjea hadi wakati ambapo mwanagenzi atawasilisha kazi yake kwake ama wakati wa urekebishaji utakapofika bila kumtatiza mwanagenzi na njia hiyo ya tatu ni pale ambapo mkufunzi anakuwa tu msikilizaji na mtazamaji na kunakili makosa ambayo wanagenzi wanayafanya na kisha kuyaeleza na kuyajadili baada ya somo kuisha ama kwenye somo lifuatalo.Mbinu hii imepata uungwaji mkono na wataalamu wengi kama vile Bartram na Walton(1991) na pia Bastorkmen na wenziwe (2004).

Njia nyingine ambayo tunapendekeza katika kurekebisha na kupunguza makosa ya kimofofofnolojia katika kazi andishi za Kiswahili baina ya wanagenzi walio na asili ya lugha ya

Kikuyu ni kwamba walimu wanaposahihisha insha za wanagenzi watumie mbinu ya kutoa majibu moja kwa moja au mbinu ya kutumia ishara au alama tofauti tofauti kudhihirisha kuwa kosa limetokea.Kwa kutumia mbinu ya kutoa majibu moja kwa moja,mkufunzi huwa anapigia mstari neno ambalo lina kosa au sauti yenye kosa kisha mwalimu huandika sauti au neno sahihi karibu na neno hilo (Sheen na Ellis,2011).Mbinu hii ni nzuri kwa sababu mwanagenzi huweza kutambua papo hapo na kubaini kosa lake na hivyo kuweza kulikosoa pia, humpunguzia mwanafunzi muda wa kwenda kutafuta neno sahihi au sauti sahihi.Kwa kutumia ishara au alama mbalimbali kuonyesha kwamba kosa fulani limetokea, mwalimu huweza kuweka alama au ishara ya kubuni au zile ambazo zimependekezwa na taasisi ambazo zinahusika.Kwa mfano, mwalimu hupigia mstari kosa ambalo limetokea na kuonyesha ni kosa la aina gani kwa kutumia alama mbalimbali.Mbinu hii huwapa wanafunzi changamoto nyingi kwani inabidi wafikirie kosa ni lipi na pia njia ya kulirekebisha kosa hilo (Hormer,2004).Mbinu hii huweza kutumika vizuri ikiwa wanafunzi wamefunzwa maana na matumizi ya ishara husika.

Mbinu nyingine ya kurekebisha makosa ya kimofofonolojia katika kazi andishi za Kiswahili baina ya wanagenzi wa shule za sekondari wenye asili ya lugha ya Kikikuyu ni kuandaa vikao vya uandishi ambapo wanagenzi hupata nafasi ya kuwauliza wakufunzi wao maswali yanayohusiana na makosa ambayo waliyafanya na pia maoni ambayo yalitolewa na mwalimu katika insha za wanafunzi husika.(Goldstein na Conrad,1990).Katika mbinu hii, mkufunzi huweza kutoa ufafanuzi zaidi kuhusu makosa ya wanafunzi ambayo bado hawajaitambua, kutoa miktadha mingine ambayo neno husika hutumika na hata kutoa visawe vya neno husika.Ingawa mbinu hii inahitaji muda mwingi na pia idadi ndogo ya wanafunzi ni mbinu mojawapo iliyo bora zaidi katika kurekebisha makosa ya wanafunzi ambao wanajifunza lugha ya pili( Bitchener & wenziwe, 2005).Hivyo, tunapendekeza wizara ya elimu kuongeza vipindi vya Kiswahili kwenye shule za

sekondari kutoka tano katika kidato cha kwanza na pili, na sita daraja ya tatu na nne ndio walimu wa Kiswahili wapate muda wa kutosha.

Kwa makosa ambayo hutokana na wanagenzi kurithishwa kutoka kwa walimu wao, tunapendekeza wakufunzi wa lugha ya Kiswahili waendelee kupata mafunzo ya kila wakati ili kuwe na kupungua kwa hali yao ya kufanya makosa na pia waweze kutangusana na wanajamii ili kuimarisha umilisi wa lugha ya Kiswahili.

Mtaalamu Hormer (2007) pia anapendekeza kuwa iwapo mwalimu amekuwa katika hali ya kufundisha kipengele fulani cha sheria ya lugha au kiwango fulani ni sharti mwalimu huyu afanye bidii ili mwanafunzi awe na uwezo wa kutambua kuwa kosa limefanyika badala ya mwalimu kutoa jibu la kosa husika.Hii inamaanisha kuwa mwanagenzi anapata uwezo wa kulisahihisha kosa husika kibinafsi na kwa njia hii kurahihisha ujifundishaji wa lugha ya pili.kwa hali hii mkufunzi anafaa kumwagiza mwanafunzi arudie kauli yake, kuuliza swali kwa namna ambayo jibu ambalo litatolewa litahusisha sehemu yenye kosa, mwalimu kujitia kutoelewa kauli yenye kosa, mwalimu kurudia kauli ya mwanagenzi kwa kutilia shadda zaidi sehemu iliyo na makosa kwa kuisema kwa kiimbo cha juu, mwalimu kurudia neno la mwisho ambalo ni sahihi kwa njia ya kusita kidogo halafu kuinua kiimbo na pia kutoa kauli na swali linayoonyesha kuwa kosa la kiisimu limetokea ili mwanagenzi aweze kupata uwezo wa kulisahihisha kosa yeye mwenyewe.

Kwa hivyo, kulingana na falsafa ya Uchanganuzi Makosa ambayo imetumika kwenye utafiti huu, baada ya mtafiti kubaini na kutambua makosa ya mwanagenzi, ni lazima mtafiti apendekeze namna ya kukabiliana na makosa hayo, hivyo basi pamoja na mbinu ambazo zimependekezwa hapo juu, mtafiti anapendekeza njia zifuatazo ili kupunguza na kurekebisha makosa ya kimofofonolojia kwenye kazi andishi za Kiswahili kati ya wanagenzi wa shule za sekondari wenye asili ya lugha ya Kikuyu.

Wakufunzi ambao wanafundisha lugha ya Kiswahili wanafaa kuwa waangalifu wanapokuwa darasani ili wasifanye makosa ya kimofofonolojia.Hii ni kwa vile mwanagenzi hujifunza lugha kwa kumuiga mkufunzi wake hivyo basi, ikiwa mkufunzi atafanya makosa basi wanafunzi pia watafanya makosa yayo hayo, walimu wanaofundisha lugha ya Kiswahili pia wanafaa wawe na ujuzi na umilisi wa hali ya juu ya lugha ya Kiswahili sanifu ndio wanagenzi waweze kuwa na uwezo wa kujifunza kwa utaratibu mzuri na pia walimu wawe kielelezo bora kwa wanagenzi wao, walimu waweze kuwakosoa wanagenzi pindi tu wanapofanya makosa ili wanagenzi wasiyarudie makosa hayo,walimu ambao wanafundisha lugha ya Kiswahili pia sharti wawe makini kujua kuwa mwanafunzi huyu mwenye asili ya lugha ya Kikuyu ana miundo yake ya lugha ya kwanza akili hivyo mwalimu aweze kuchunguza ni vipengele vipi vya kimofofonolojia vinavyofanana baina ya lugha hizi mbili ili aweze kumwelekeza mwanafunzi jinsi anaweza kuvitumia kumsaidia kwenye ujifunzaji wake wa lugha ya Kiswahili na pia achunguze ni vipengele vipi vya kimofofonolojia vilivyo tofauti kati ya lugha ya Kikuyu na ile ya Kiswahili na ambavyo vinaweza kumtatiza mwanagenzi anapojifundisha lugha ya Kiswahili ili mkufunzi aweze kumwelekeza mwanafunzi inavyopaswa ili aweze kuepukana na utata huo,muda wa mtagusano baina ya mwalimu wa lugha ya Kiswahili na mwafunzi uongezwe ili wapate kuingiliana vizuri na hivyo kupata muda wa kukosoa makosa ya kimofofonolojia ya wanafunzi,wanafunzi wanafaa pia kufanya mazoezi mengi katika lugha ya Kiswahili kwa kuandika insha nyingi inavyowezekana ili wapate mazoea ya vipengele ambayo vinawatatiza na hivyo kupunguza makosa ya kimofofonolojia kwenye kazi andishi za Kiswahili, wanagenzi pia waandaliwe mijadala mbalimbali katika lugha ya Kiswahili ili waweze kukuza stadi yao ya kuzungumza ambayo mwishowe itadhihirika katika kazi andishi zao kwa kupunguza makosa,wanafunzi kuzungumza kwa lugha ya Kiswahili hata wanapokuwa nje ya shule na hivyo mazoezi haya yatawasaidia hata kuandika kazi za Kiswahili zisizo na makosa

mengi na mwisho walimu na wanafunzi wanaweza kutumia teknolojia ili kurekebisha makosa ya kimofofonolojia.Walimu na wanafunzi wanaweza kutumia vifaa na programu za mafunzo ya lugha. Mifano ya vifaa hivi na programu hizi ni 'duolingo',' babble', 'google speech-to-text', 'pycharm',' VoiceOver',' Read and Write', 'Dragon Naturally Speaking 'na nyinginezo.

Tunapendekeza walimu na wanagenzi watumie zaidi ya mbinu moja ya kurekebisha makosa ya kimofofonolojia kwenye kazi andishi za Kiswahili kati ya wanagenzi wa shule za sekondari wenye asili ya lugha ya Kikuyu ili waweze kupata matokeo yaliyo bora zaidi.

Mount Kenya University

# SURA YA TANO

# MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.0 Utangulizi

Hii ni sura ambayo ni hitimisho ya utafiti huu wetu.Sura hii imeangazia kwa kifupi muhtasari wa huu utafiti pamoja na mapendekezo ya mtafiti.Mtafiti anaeleza ukweli kwamba kuna makosa ya kifonolojia na kimofolojia ambayo wanagenzi wenye asili ya lugha ya Kikuyu hufanya katika kazi andishi za lugha ya Kiswahili wanapojifunza na kuandika Kiswahili.Sababu kuu ya makosa ya

kimofofonolojia ni tofauti za mifumo ya kimofofonolojia baina ya lugha ya Kiswahili na ile ya Kikuyu pamoja na athari ya lugha ya Kikuyu katika Kiswahili.Aidha, mtafiti anatoa mapendekezo yake ambayo yametokana na utafiti wake huu na pia kutoa mapendekezo zaidi ya tafiti za siku za baadaye.

**5.1Muhtasari**

Mada ya uchunguzi huu ni makosa ya kimofofonolojia kwenye kazi andishi za Kiswahili kati ya wanagenzi walio na asili ya lugha ya Kikuyu katika shule za upili Kahuro, Murang'a.Lengo kuu la utafiti huu lilikua kuchanganua makosa ya kimofofonolojia kwenye kazi andishi za Kiswahili kati ya wanagenzi walio na asili ya lugha ya Kikuyu kwenye shule za sekondari, Kahuro, Murang'a. Malengo mahususi yalikuwa manne ambayo ni kubainisha makosa ya kifonolojia kwenye kazi andishi za Kiswahili baina ya wanagenzi wa shule za sekondari wenye asili ya lugha ya Kikuyu katika jitihada zao za kujifunza lugha ya Kiswahili, kutambua makosa ya kimofolojia kwenye kazi andishi za Kiswahili yanayofanywa na wanagenzi wa shule za sekondari wenye asili ya lugha ya Kikuyu katika kujifunza lugha ya Kiswahili, kubaini vyanzo vya makosa ya kimofofonolojia katika kazi andishi za Kiswahili katika juhudi za ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili kati ya wanafunzi wa shule za sekondari wenye asili ya lugha ya Kikuyu na kutathmini namna ya kurekebisha makosa ya kimofofonolojia kwenye kazi andishi za lugha ya Kiswahili baina ya wanagenzi wa shule za sekondari wenye asili ya lugha ya Kikuyu.Maswali ya uchunguzi ambayo yalinuiwa kujibiwa na uchunguzi huu ni je, makosa ya kifonolojia yanajitokeza vipi kwenye kazi andishi za lugha ya Kiswahili baina ya wanagenzi wa shule za upili wenye asili ya lugha ya Kikikuyu,je ni makosa yepi ya kimofolojia ambayo yanajitokeza kwenye kazi andishi za lugha ya Kiswahili baina ya wanagenzi wa shule za sekondari wenye asili ya lugha ya Kikuyu, je, ni nini kinachosababisha makosa ya kimofofonolojia kwenye kazi andishi za Kiswahili kati ya wanagenzi

wa shule za sekondari wenye asili ya lugha ya Kikuyu na je, ni vipi ambavyo makosa ya kimofofonolojia kwenye kazi andishi za lugha ya Kiswahili baina ya wanafunzi walio na asili ya lugha ya Kikuyu yanavyoweza kurekebishwa.Nadharia ambayo iliongoza utafiti huu ni falsafa ya Uchanganuzi Makosa iliyoasisiwa na mtaalamu Corder mwaka wa 1960.

Uchunguzi huu umegawanya kwenye sura tano kuu. Kwenye sura ya kwanza, tumeangazia usuli wa mada, suala la uchunguzi, madhumuni ya uchunguzi, maswali ya uchunguzi, sababu za kuchagua mada, umuhimu wa uchunguzi pamoja na ufafanuzi wa istilahi muhimu.Ili kupata data iliyokusudiwa, utafiti ulifanyika katika jimbo dogo la Kahuro, kaunti ya Murang'a ambako kuna wakaazi asilia wa lugha ya Kikuyu.Utafiti huu uliwalenga wanagenzi wa shule za upili ambazo ni kutwa ambapo wanafunzi 30; 10 kutoka daraja ya pili, 10 kutoka cha tatu na 10 kutoka daraja ya nne, kwenye shule ya upili ya kutwa ya Koimbi waliandika insha na mtafiti kuzisoma huku akidondoa makosa ya kifonolojia na kimofolojia.Sababu ya kuchagua mada ya utafiti huu ni kwamba ilibainika kuwa watafiti wa awali wa suala la makosa ya kimofofonolojia baina ya wanagenzi wanaojifunza lugha ya Kiswahili yana uwezo wa kutiliwa shaka na pia taaluma ya mofofonolojia haijatafitiwa kwa kuangazia makosa ya kimofofonolojia kati ya wanafunzi walio na asili ya lugha ya Kikuyu kwenye ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili.

Kwenye sura ya pili, utafiti huu umeangazia mapitio ya maandiko na misingi ya nadharia. Uchunguzi huu umeangazia yaliyoandikwa kuhusu dhana ya makosa, makosa ya kifonolojia na kimofolojia kwenye lugha wakati wa kujifunza lugha ya pili, vyanzo vya wanagenzi kutekeleza makosa ya kimofofonolojia na jinsi ya kukabiliana na makosa ya kimofofonolojia baina ya wanagenzi wakati wanajifunza lugha ya pili. Nadharia ambayo iliongoza uchunguzi huu ni ile ya Uchanganuzi Makosa yake Corder (1960). Hii nadharia hutumiwa kuchunguza makosa katika lugha na pia kuangalia sababu za watu kufanya makosa wanapojifunza lugha na pia jinsi ya

kurekebisha au kupunguza utokeaji wa makosa mtu anapojifunza lugha ya pili. Falsafa hii ilikuwa mwafaka kwa uchunguzi huu kwani iliweza kutumika kuonyesha makosa ya kifonolojia na kimofolojia ambayo yanajitokeza kwenye kazi andishi za Kiswahili za wanagenzi wa shule za sekondari walio na asili ya lugha ya Kikuyu na pia kueleza sababu za wanagenzi wa shule za upili walio na asili ya lugha ya Kikuyu kufanya makosa ya kimofofonolojia.Aidha, iliwezesha kueleza namna ya kurekebisha na kupunguza makosa ya kimofofonolojia kwenye kazi andishi za Kiswahili baina ya wanagenzi wa shule za sekondari wenye asili ya lugha ya Kikuyu.

Kwenye sura ya tatu tumeangazia mbinu za utafiti na uchanganuzi wa data. Uchunguzi huu ulifanywa nyanjani na maktabani .Nyanjani data ilikusanywa kwa kutumia mbinu ya maandishi ambapo wanagenzi 30 wa skuli ya sekondari ya kutwa ya Koimbi walipewa insha yenye mada maalumu kisha mtafiti akazisoma huku akidondoa makosa ya kifonolojia na kimofolojia na kisha kuyaainisha.Maktabani, mtafiti alisoma vitabu, tasnifu, Makala na mapendekezo mbalimbali ili kubaini vyanzo vya makosa ya kimofofonolojia na jinsi ya kurekebisha na kupunguza makosa haya ya kimofofonolojia miongoni mwa wanagenzi ambao wanajifunza lugha ya pili.Utafiti huu ulifanywa kwenye jimbo dogo ya Kahuro, jimbo la Murang'a ambako kuna wenyeji asilia wa lugha ya Kikuyu.Aidha, utafiti huu uliangazia wanagenzi wa shule za sekondari za kutwa ambao ni wenyeji wa kaunti hii ndogo ya Kahuro, Murang'a.Mtafiti alichagua wanafunzi 30 kwa njia ya usampulishaji nasibu,kumi kutoka daraja ya pili, kumi kutoka daraja ya tatu na pia kumi kutoka daraja ya nne ambao walipewa mtihani wa insha wenye mada maalumu na kisha mtafiti akazisoma insha hizo huku akidondoa makosa ya kifonolojia na kimofolojia.

Sura ile ya nne nayo imezingatia matokeo ya utafiti, ufasili na uwasilishaji wa data.Kwanza, surah hii imeanza kwa utangulizi ambao ni muhtasari wa sura nzima. Kisha ikajikita katika kuangazia kipengele cha fonolojia kwa undani ambapo ameelezea maana ya fonolojia, vipera vya fonolojia,

vipengele vya fonolojia, aidha kipengele cha fonimu kimeangaziwa na pia mitazamo inayotumiwa kufafanua fonimu.Pia, utanzu wa fonetiki umeelezwa kwa sababu fonetiki na fonolojia ni matawi mawili yanayoingiliana. Kipengele cha mofolojia pia kimeangaziwa kwa undani ambapo maana ya mofolojia, sura za mofolojia, vipera vya mofolojia na pia kipengele cha mofimu ambacho ndicho kipashio cha kimsingi cha mofolojia vimeelezwa. Uhusiano ambao upo kati ya mofolojia na kifonolojia haujawachwa nje.

Pia, sura hii imeangazia dhana ya mofofonolojia, sauti za lugha ya Kiswahili na zile za lugha ya Kikuyu, mifanyiko au kanuni za kimofofonolojia kwenye lugha ya Kiswahili na ile ya Kikuyu pia imeonyeshwa.Aina ya mifanyiko ya kimofofonolojia ni pamoja na kuyeyusha, kudondosha, ukaakaaishaji, kunazalishwa kwa irabu, utamkaji pamwe wa nazali, mvutano wa irabu, nazali kuathiri konsonanti, kulegea na kukaza sauti, tangamano irabu, uchopekaji na tabdili.Mikondo ya kimofofonolojia ya lugha ya Kikuyu ni pamoja na kuimarika kwa konsonanti, muungano wa konsonanti, usimilisho pamwe wa nazali, kudondoshwa kwa sauti, uchopekaji na usimilisho.

Data iliyokusanywa iliweza kuainishwa na kupangwa katika makundi mawili ambayo ni makosa ya kifonolojia na makosa ya kimofolojia ambayo wanagenzi wa shule za sekondari wenye asili ya lugha ya Kikuyu walifanya katika insha walizoziandika.Makosa ya kifonolojia yaliyobainishwa ni pamoja na kuchopeka fonimu kama vile /u/, /i/, /h/,/y/ au /w/,udondoshaji wa sauti kama vile/h/, /a/, /i/; kutumia fonimu mbadala kama vile,kutumia fonimu /r/ mahali pa /l/, /l/ mahali pa /r/, /sh/ mahali pa /s/, /d/ mahali pa /nd/, /nd/ mahali pa /d/, /b/ mahali pa /mb/, /mb/ mahali pa /b/, /g/ mahali pa /ng/, /ng/ mahali pa /g/, /nj/ mahali pa /j/, /s/ mahali pa /z/ na kutumia fonimu /sh/ mahali pa /ch/. Makosa ya kimofolojia yaliyofanywa na wanagenzi katika kazi zao ni pamoja na kudondosha vipashio kama vile kudondosha /i/, /h/, /w/, /y/ na /u/; uchopekaji wa vipashio kama vile /ma/, /ku/, viambishi ngeli visivyofaa, kiambishi tamati /ng/ katika vitenzi kuonyesha mazoea;

kutumia vipashio mbadala kama vile kutumia /l/ mahali pa /r/, /th/ mahali pa /dh/, /ka/ badala ya /ki/, /ng/ mahali pa /ng'/, /c/ mahali pa /z/, irabu badala ya viyeyusho, kubadilisha mpangilio wa vipashio katika neno, kubadilisha mofu katika neno na mnyambuliko mbaya wa vitenzi.

Sababu za wanagenzi wa shule za upili wenye asili ya lugha ya Kikuyu kufanya makosa ya kimofofonolojia kwenye kazi andishi za Kiswahili tulizozizingatia katika utafiti huu ni mifumo tofauti ya sauti za Kiswahili na zile za lugha ya Kikuyu, mifumo tofauti ya kimofolojia kati ya lugha ya Kikuyu na ile ya Kiswahili, kutumia lugha ya Kikuyu kwa muda mrefu miongoni mwa wanafunzi, walimu na jamii kwa jumla, kutomudu sheria za lugha ya Kiswahili ipasavyo na njia mbaya za kufundisha lugha ya pili.

Mbinu za kurekebisha makosa ya kimofofonolojia kwenye kazi andishi za Kiswahili kati ya wanagenzi wa shule za sekondari wenye asili ya lugha ya Kikikuyu ambayo tulizingatia katika kazi hii ni; walimu wa lugha ya Kiswahili wafundishe ruwaza za sauti ya lugha ya Kiswahili huku wakitilia maanani zile sauti ambazo hazimo katika lugha ya Kikuyu, walimu wawasaidie wanafunzi kubaini ukweli kwamba lugha hizi mbili zina tofauti katika sauti ili kuweza kuzuia mazoea ya kuhamisha vipengele vya lugha ya Kikuyu hadi ile ya Kiswahili, kutoa marekebisho ya makosa punde yanapotokea bila kungojea wakati mwafaka, kuandaa vikao vya uandishi ambapo wanagenzi hupata fursa ya kuwauliza walimu wao maswali yanayohusiana na makosa, walimu wa lugha ya Kiswahili waendelee kupata mafunzo kila mara ili kuwe na upungufu wa hali yao ya kufanya makosa na kuimarisha umilisi wao wa lugha, walimu kuwa waangalifu wanapokuwa darasani ili wasifanye makosa ya kimofofonolojia na muda wa mtagusano baina ya mwalimu wa lugha ya Kiswahili na mwanafunzi uongezwe.Aidha, wanagenzi wa lugha ya Kiswahili kufanya mazoezi ya vipengele ambavyo vinawatatiza, kuandaa mijadala ya lugha ya Kiswahili, wanafunzi kuzungumza katika lugha ya Kiswahili na wanafunzi na walimu wanaweza

pia kutumia teknolojia ili kurekebisha makosa ya kimofofonolojia .Tunapendekeza wakufunzi na wanagenzi waweze kutumia njia zaidi ya moja kurekebisha na kupunguza makosa ya kimofofonolojia.

Sura ile ya tano inatamatisha uchunguzi wetu. Inatoa muhtasari wa uchunguzi kwa jumla na pia kutoa mapendekezo ya mtafiti ambayo ni; walimu, wanagenzi na washikadau wote wa lugha ya Kiswahili kutumia mbinu zilizopendekezwa ili kupunguza na kurekebisha makosa ya kimofofonolojia katika kazi andishi za wanafunzi, kutumia mbinu nyinginezo kufanya utafiti, kuchunguza makosa mengine ya lugha, kuchunguza makosa ya kimofofonolia katika stadi nyinginezo, kufanya utafiti katika maeneo mengine , kuongeza vyanzo vya makosa ya kimofofonolojia na pia kufanya utafiti kuhusu njia zingine za kurekebisha na kupunguza makosa ya kimofofonolojia baina ya wanafunzi wa shule za sekondari wenye asili ya lugha ya Kikuyu.

**5.2 Hitimisho**

Utafiti huu ulikuwa unajihusisha na kuchanganua makosa ya kimofofonolojia katika kazi andishi za Kiswahili miongoni mwa wanafunzi wenye asili ya lugha ya Kikuyu katika shule za upili kwa kutumia nadharia ya Uchanganuzi Makosa iliyoasisiwa na mwanaisimu Corder (1960).Malengo ya utafiti huu yalikuwa manne ambayo ni; kubainisha makosa ya kifonolojia katika kazi andishi za Kiswahili miongoni mwa wanafunzi wa shule za upili wenye asili ya lugha ya Kikuyu katika jitihada zao za kujifunza lugha ya Kiswahili, kutambua makosa ya kimofolojia katika kazi andishi za Kiswahili yanayofanywa na wanafunzi wa shule za upili wenye asili ya lugha ya Kikuyu katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili, kubaini vyanzo vya makosa ya kimofofonolojia katika kazi andishi za Kiswahili katika juhudi za ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili miongoni mwa wanafunzi wa shule za upili wenye asili ya lugha ya Kikuyu na kutathmini namna ya kurekebisha makosa ya

kimofofonolojia katika kazi andishi za lugha ya Kiswahili miongoni mwa wanafunzi wa shule za upili wenye asili ya lugha ya Kikuyu.

Kupitia utafiti huu, mtafiti alibaini kuwa wanagenzi wa shule za upili wenye asili ya lugha ya Kikuyu walifanya makosa ya kimofofonolojia walipoandika kazi za Kiswahili.Mtafiti aliainisha makosa yaliyofanywa na wanagenzi katika makundi mawili makuu yaani makosa ya kifonolojia na makosa ya kimofolojia.Kisha alibainisha makosa ya kifonolojia ambayo ni uchopekaji wa fonimu, udodoshaji wa fonimu na utumizi wa sauti mbadala. Uchopekaji ulihusu fonimu /u/, /i/, /h/, /y/ au /w/.Udondoshaji ulikuwa wa fonimu /h/, /a/ na /i/. Utumizi wa sauti mbadala uliathiri fonimu kama vile kutumia /r/ badala ya /l/, kutumia /l/ badala ya /r/, kutumia /sh/ mahali pa /s/, kutumia /d/ mahali pa /nd/, kutumia /nd/ mahali pa /d/, kutumia /b/ mahali pa /mb/, kutumia /mb/ mahali pa /b/, kutumia /g/ mahali pa /ng/, kutumia /ng/ mahali pa /g/, kutumia /nj/ mahali pa fonimu /j/, kutumia /s/ mahali pa /z/ na kutumia /sh/ mahali pa /ch/. Pia alitambua makosa ya kimofolojia ambayo ni pamoja na kuchopeka vipengele, kudondosha vipengele, kuyeyusha baadhi ya vipengele, kubadilisha vipashio katika neno na kubadili mpangilio wa vipashio katika neno.Uchopekaji ulihusu vipashio kama vile kuongeza /ma/ katika baadhi ya nomino, kuongeza /ku/, kuongeza viambishi ngeli visivyofaa, kuongeza kiambishi tamati /ng/ katika vitenzi kuonyesha hali ya mazoea. Udondoshaji ulikuwa wa /e/, /i/, /a/, /h/, /w/, /y/, na /u/. Pia, matumizi ya mofimu mbadala yalidhihirika kwa mfano, kutumia /r/ mahali pa /l/, kutumia /l/ mahali pa /r/, /th/ mahali pa /dh/, /ka/ badala ya /ki/, /ng/ badala ya /ng'/, /c/ mahali pa /z/, irabu badala ya viyeyusho, kubadilisha mpangilio wa vipashio katika neno, kubadilisha mofu katika neno na mnyambuliko mbaya wa vitenzi.Aidha, mtafiti aliweza kuonyesha sababu za wanagenzi wa Kiswahili wa shule za upili wenye asili ya lugha ya Kikuyu kufanya makosa haya ya

kimofofonolojia katika kazi andishi za Kiswahili.Pia, mtafiti aliweza kueleza jinsi ya kukabiliana na makosa ya wanagenzi katika kazi andishi za Kiswahili wanapojifunza Kiswahili.

Kupitia utafiti huu, ni wazi kuwa kuna utofauti wa kimofofonolojia baina ya lugha ya Kiswahili na ile ya Kikuyu ingawa lugha hizi mbili ni lugha za Kibantu.Kwa sababu ya tofauti hizi za kimofofonolojia baina ya lugha hizi mbili, wanagenzi wa shule za upili wenye asili ya lugha ya Kikuyu hufanya makosa ya kimofofonolojia wanapoandika kazi za Kiswahili.Aidha, ni dhahiri kuwa makosa haya yana uwezo wa kupunguzwa na kurekebishwa kwa kutumia mbinu mbalimbali ambazo huhusisha kuweka mikakati tofauti tofauti. Kwa hivyo, wakufunzi, wanagenzi, watengenezaji mitaala na washika dau wengine wa lugha ya Kiswahili wanahitajika kuweka mikakati bora ya kushughulikia makosa hayo.

**5.3 Mapendekezo**

Kupitia utafiti huu ni dhahiri kuwa wanafunzi wa shule za upili wenye asili ya lugha ya Kikuyu hufanya makosa ya kimofofonolojia wanapoandika kazi za Kiswahili, hivyo basi tunapendekeza walimu, wanafunzi na washika dau wote watumie mbinu ambazo zimeelezwa kwenye utafiti huu ili kupunguza na kurekebisha makosa haya na hili litapelekea matokeo ya wanafunzi katika somo la Kiswahili kuboreshwa.

Aidha, katika utafiti huu mtafiti ametumia mbinu ya uandishi wa insha pekee ilhali kuna mbinu nyingine za kuchunguza makosa katika lugha kama vile kutumia njia ya masimulizi, kutafsiri vifungu vilivyoandikwa na usomaji wa hadithi.Hivyo basi tunapendekeza tafiti za usoni zitumie mbinu hizi mbadala ili kutafiti makosa ya kimofofonolojia katika kazi za Kiswahili miongoni mwa wanafunzi wenye asili ya lugha ya Kikuyu.

Pia, utafiti huu umechunguza tu makosa ya kimofofonolojia katika kazi andishi za Kiswahili miongoni mwa wanafunzi wa sekondari wenye asili ya lugha ya Kikuyu ilhali makosa haya ya kimofofonolojia pia hutokea katika mazungumzo.Kwa hali hii, tunapendekeza tafiti za usoni kuzingatia pia lugha zungumzwa.

Mtafiti ametafitia tu makosa ya kimofofonolojia ilhali kuna makosa yanayotokea katika viwango vingine kama vile mofosintaksia, sintaksia, semantiki na sarufi, kwa hivyo tunapendekeza tafiti za usoni zizingatie viwango hivi vingine.

Aidha, utafiti huu umejikita katika shule za upili katika jimbo dogo la Kahuro, Murang'a ilhali jamii ya Wakikuyu imesambaa katika maeneo mengine jimboni Murang'a na pia kaunti zingine kama vile Kiambu, Nyeri, Kirinyaga, Laikipia na sehemu nyinginezo, hivyo basi tunapendekeza uchunguzi wa baadaye uhusishe maeneo haya tofauti pia.

Mtafiti pia alitumia shule mojawapo katika jimbo dogo la Kahuro, hivyo tunapendekeza tafiti za usoni zizingatie shule kadhaa ili kutoa taswira pana ya makosa ya kimofofonolojia yanafanywa katika kazi za Kiswahili miongoni mwa wanafunzi wenye asili ya lugha ya Kikuyu.

Pia, hatuwezi kudai kuwa tumeangazia sababu zote za wananagenzi wenye asili ya lugha ya Kikuyu kufanya makosa ya kimofofonolojia katika kazi andishi za Kiswahili na pia namna ya kurekebisha makosa hayo, hivyo basi tunapendekeza uchunguzi wa baadaye uzingatie visababishi zaidi vya makosa ya kimofofonolojia miongoni mwa wanafunzi wenye asili ya lugha ya Kikuyu na pia njia zaidi za kurekebisha makosa hayo ya kimofofonolojia miongoni mwa wanafunzi wanapojifunza lugha ya Kiswahili.

# MAREJELEO

Ali, N. (2013). *Kiswahili Jukwaani*.Blogu ya kujifunza lugha na fasihi ya Kiswahili na Waswahili. Retrieved on July 21, 2024, from https://Kiswahilijukwaani.blogspot.com/2013/12/Kiswahili-ni-nini.html

Allwright, D. na Barley, K. (1991).*Focus on the Language Learner*.Cambridge.Cambridge University Press.

Babbie, E. (1999). *The Basic of Social Research*. Belmont: Wadsworth Publishing Company.

Baraza la Kiswahili la Zanzibar (2010). *Kamusi la Kiswahili Fasaha*.Nairobi.Oxford University Press.

Bitchener na wenziwe (2005).*The Effects of Different Types of Corrective Feedback on ESL Student Writing*.Journal of Second Language Writing, 14, 191-205. Kutoka https://doi.org/10.1016/j.jslw.2005.08.001

Chomsky, N. (1957*). Fundamentals of Language.International Journal of American Linguistics*, 23(3), 235-242.

Chomsky, N. (1967).*Some of general properties of phonological rules.*Language 43:102-128

Chomsky, N. na Halle, M. (1968).*The Sound Pattern of English*.Newyork.Harper& Row.

Cook, V. J. (1992). *Evidence for Multicompetence.Language Learning*, 42(4), 557-591.

Corder, P. (1960). *An Intermediate English Practice book*.Longman.London.

Corder, S. P. (1967). *The Significance of Learner's errors*. 4(50, 161-170.

Corder, S. P. (1967). *Error Analysis and Interlanguage* .Oxford.Oxford University Press.

Corder, S. (1971). *Idiosyncratic dialects and errors analysis*.*In Richards J.E*(Ed*).Error Analysis*: *Perspectives on Second Language* Acquisition.London: Longman.

Crystal, D. (1997). *Dictionary of Linguistics and Phonetics*. Blackwell Publishers Ltd.

Ellis, R. (1994). *The study of second language acquisition*. Oxford.OUP.

Ellis, R. (1997). *Second Language Acquisition*: New York, Oxford University Press, inc.

Ellis, R. (2003). *Second Language Acquisition. An Introductory course.* Mahwah. *NJ. LEA*

Enon, J. C. (1998). *Educational Research, Statistics and Measurement*.Kampala-Makerere University, Department of Distance Learning.

Frederick, F. (2019). *Makosa ya kifonolojia yanayofanywa na wazungumzaji wa Kihaya wanaojifunza Kiswahili Sanifu: Mfano kutoka Bukoba Manispaa (tasnifu ya Uzamili)* .Chuo kikuu Huria cha Tanzania.

Gass S., na Selinker (2001).*Second language Acquisition.An introductory course*.Mahwah, NJ: LEA

Gass S., na Selinker (2008).*Second language Acquisition.An introductory course*.New York.Routledge.

Goldstein, L. na Conrad, S. M. (1990). *Student Input and Negotiation of Meaning in ESL Writing Conferences.*TESOL Quartely, 24(3), 443-460.

Habwe, J. & Karanja, P. (2004). *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili*.Phoenix Publishers.

Harmer J. (2004).*How to Teach Writing*.Harlow.Longman.

Harmer J. (2007).*The Practice of English Language Teaching*.Harlow.Longman.

Iribe M. P. (2016).*Kikuyu Phonology and arthography 16.The Language Loss of the Indigenous,* 239.

Kanake, J. (2013).*Makosa ya Kifonolojia Miongoni mwa Wanafunzi wa Kiigembe katika Ujifunzaji wa Kiswahili*. (Tasnifu ya M.A). Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Kanake, J. & Kobia, J. (2023). Makosa ya Kifonolojia Miongoni mwa Wanafunzi wa Kiigembe katika Ujifunzaji wa Kiswahili. *East African Journal of Swahili Studies*, 6(1), 40-48.

Mount Kenya University

Katamba, F. (1993). *Morphology*.New York: Palygrave.

Katulu, V. (2020). *Uchanganuzi wa Makosa ya Kimofofonolojia katika Lugha ya Kiswahili Miongoni mwa Wanafunzi wenye Asili ya Lugha ya Kikamba*. (Tasnifu ya M.A.). Chuo kikuu cha Pwani.

Konig, E. na Gast, V. (2009).*Understanding English-German Contrast.Berlin*.Erich Schmidt.

Kothari, C. (2004). *Research Methodology*: *Methods and techniques*.New International Ltd.

Massamba, D. P. B. (1986). *On the influence of local language on Kiswahili.The case of Mara Region in Tanzania*, in F. Frederick (2019).*Makosa ya kifonolojia yanayofanywa na wazungumzaji wa Kihaya wanaojifunza Kiswahili sanifu: Mfano kutoka Bukoba Manispaa*. (Tasnifu ya M.A) .Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Massamba, D.(1996).*Phonological theory:History and Development*.Dar es Salaam.Dar es Salaam University Press.

Massamba na wenzake (2001).*Sarufi muundo ya Kiswahili Sanifu* (SAMIKISA): *Sekondari na vyuo*.Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili; Chuo kikuu cha Dar es Salaam.

Massamba, D. (2004).*Kamusi ya Isimu na Falsafa ya lugha*.Dar es Salaam: TUKI.

Massamba na wenziwe (2004). *Fonolojia ya Kiswahili Sanifu (SAMIKISA*): *Sekondari na vyuo*.Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.Chuo kikuu cha Dar es Salaam.

Massamba, D.P (2009*). Kamusi ya Isimu na Falsafa*.Dar es Salaam.TUKI.

Massamba, D. (2010*). Phonological Theory*.*Historical and Development*.Dar es Salaam.TUKI.

Mount Kenya University

Massamba, D. (2012). *Misingi ya Fonolojia* .Dar es Salaam.Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, chuo kikuu cha Dar es Salaam.

Mathews, P. H(1974). *Morphology (2nd Ed)*. Cambridge. Cambridge University Press.

Mdee J. S. na wenzake (2011*). Kamusi ya Karne ya 21*. Nairobi. Longhorn Publishers (K) Ltd.

Mgullu, R. (1996). *Mtaala wa Isimu: Fonetiki, fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili (Swahili Edition)*.Nairobi.Longhorn Publishers.

Mgullu, R. (1999*).* *Mtaala wa isimu*: *Fonetiki*, *Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili:* Nairobi.Longhorn.

Mudhune, E. (1994). *A Contrastive Analysis Approach to the Learning of Swahili Morphosyntax by Luo learners. (*Tasnifu ya M.A).Nairobi: Chuo kikuu cha Kenyatta.

Muftah, M. (2016b). *English past Tense Morphology in Adult Arab EFL Learners: Mental Representaion Mechanism and Types of Errors*. Journal of Advances in Linguisics, 6(3)

https://doi.org/10.24297/jal.v6i3.4666

Mugenda, O. & Mugenda, A. (1999).*Research Methods*; *Qualitative and Quantitative Approaches*.Nairobi: Press.

Mutahi, K. E. (1983). *Sound Change and Classification of Dialects of Southern Mt. Kenya*.Berlin.Dietrich Reimer Verlay.

Mwita, P.N. (2018).*Makosa ya kifonolojia na kimofolojia miongoni mwa wanafunzi wa Kiswahili wazungumzaji wa Kikuria na wa Kiluo*. (Tasnifu ya M.A.).Chuo Kikuu cha Nairobi.

Nchimbi, A. (2008) OFC 008*: Kiswahili .Dar es Salaam.*Taasisi ya uchunguzi wa Kiswahili.

Mount Kenya University

Njogu, K. na wenziwe (2006). *Sarufi ya Kiswahili.Uchanganuzi na Matumizi*.Nairobi.JKF.

Njogu, K., Shafi A. & Longhorn Publishers (2013).*Kamusi ya Karne ya 21*.Nairobi.Longhorn Publishers (T) Ltd.

Norrish, J. (1983). *Language Learners and their Errors*.London: The Macmillan Press Limited.

Norrish, J. (1987).*Language Learning and Their Errors.London*: Macmillan Publishers.

Nyagah, K (2016). *Uchanganuzi wa Makosa ya Kifonolojia na Kimofolojia Yanayojitokeza katika Kazi Andishi za Wanafunzi wa Shule za Upili, Tigania, Jimbo la Meru*. (Tasnifu ya M.A.). Chuo kikuu cha Nairobi.

Obara, J. (2014). *Uchanganuzi wa makosa yanayofanywa na wanafunzi wazungumzaji wa lugha ya Ekigusii*. (Phd Thesis.). University of Nairobi.

Odeo I. na Maina G. (2008). *Isimujamii*. Nairobi. Oxford University Press.

Odlin, I. (1989). *Language Transfer: Cross-linguistic Influence in Language Learning*.Cambridge.University Press.

Richards J. C. (1971). *A non-constrastive approach to error analysis*.In J. C. Richards(Ed), *Error analysis perspectives on second language learning*.London: Longman.

Richards J. C. (1974).*Errors analysis: Perspectives on Second Language Acquisition*: London.Longman.

Richard, J. na wenzake (1985).*Longman Dictionary of Language Teaching and Applied Linguistics*.Essex.Longman.

Richards, J.C. na Richards S. (2002).*Longman Dictionary of Language Teaching and Applied Linguistic.*England: Pearson Education Limited.

Rukwaro, R. (2015). Mukurwe wa Nyagathanga: The stalled tourist hotel.

https://www.researchgate.net

Seedhouse, P. (2004).*The Interactional Architecture of the Language Classroom: A Conversation Analysis Perspective*.Malden, MA.Blackwell.

Selinker, L. (1972). *Interlanguage*, Rawlence Eribaum Associates.

Sheen, Y. (2007). *The Effect of Focused Written Corrective Feedback and Language Aptitude on ESL Learners' Acquistion of Articles*.TESOL Quaterly, 41, 255-283. Kutoka

https://doi.org/10.1002/j.1545-7249.2007.t600059.x

Sheen, Y.na Ellis, R. (2011). *Corrective Feedback in Language Teaching.In* E.Hinkel(Ed).*Handbook of Research in Second Language Teaching and learning* (pp.593-610).Routledge,

TUKI (1990). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*.Dar es Salaam: TUKI.

TUKI (2001).*Kamusi ya Kiswahili Kiingereza*.TUKI, Chuo Kikuu Cha Dar es salaam.

TUKI (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu. Toleo la pili.* Nairobi.Oxford.

Ur, P. (1996). *A Course in Language Teaching: Practice and Theory*.Cambridge.Cambridge University Press.

Waihiga, G. na Wamitila K. W. (2003).*Chemichemi za Kiswahili, kidato cha kwanza*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Mount Kenya University

Walton, L. (1991).Basic Standardsnin Teaching Pathology.Volume 4, issue 6 kutoka

https://doi.org/10.1177/014107689108400611

Wanjala, V. & Mwaura F. (2022). *Athari za Kikuyu katika kujifunza Lugha ya Kiswahili Sanifu katika Shule za sekondari, Jimbo dogo la Othaya, Jimbo la Nyeri, Kenya*. (Shahada ya kwanza katika Shule ya Ualimu.). Chuo kikuu cha Gresta, Thika.

Waweru, M.M. (2012).*Lexical and Phonological errors in the spoken English language of pre-school teachers in classrooms in Kasarani division (Thesis)*.University of Nairobi.

Wilkins, D. (1972).*Linguistics in Language Teaching*. Edward Arnold, Bedford Square, London.

Zighe, M. (2021*). Makosa ya Kisarufi Yanayofanywa na Wanafunzi Wataita wa Shule za Msingi Wanaojifunza Kiswahili Sanifu katika Kaunti ya Taita/Taveta nchini Kenya*. (Tasnifu ya M.A.). Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Mount Kenya University

## VIAMBATISHO

**Kiambatisho 1: Mada ya insha**

**Andika insha isiyopungua maneno 300 juu ya mada ifuatayo: SIKU YA KUKUMBUKWA MAISHANI MWANGU**

**Kiambatisho 2: Mifano ya insha za wanafunzi**

3

# SIKU YA KUKUMBUKWA MAISHANI MWANGU.

Ilikuwa siku ya Jumatatu iliyokuwa siku ya harusi ya dada yangu hiyo siku niliamka mapema sana kujitayarisha. Nilienda bafu kuoga, hiyo siku nilikuwa nimeoga ili ningare ipasavyo nilitoka bafu na kuenda kuvaa nguo nilivaa nguo iliyokuwa inapendeza ilikuwa nyekundu. Nilivaa pia viatu nilijitayarisha haraka nikajipondoa nilikuwa nakaa malkia. Nilifurahia kujiona nikiwa napendeza hivyo sikuwahi tegemea kuwa kwamba naweza pendeza hivyo. Nilienda kwa mama na kumwambia mama anisaidie na simu yake nilipoingia aliniuliza "wewe ni nani?" nilicheka kusikia hivyo kwa sababu mama hakuwa ananijua nilimuuliza kuwa mama wasema hunijui mimi mwanao. Mama alisema kwa vile mimi ninapendeza pia sijulikani sikuwa nakujua alinipatia simu. Nilijipiga picha mingi mno.

Baada ya muda, kila mtu alikuwa amejitayarisha tulikuwa tumemaliza kila kitu tulielekea mezani sisi wote na kuomba. Ngari zilikuwa zimetugoja nje. Tulienda pia kwenye bibi harusi, alikuwa pia yeye alikuwa ametayarishwa walikuwa wanakula tuliambiwa twende tukule alafu twende kwenye harusi ita fanyiwa kwa uwanja. Tulikula na kwenda kwenye harusi ilikuwa inafanyiwa kulikuwa kunapendeza maua, hema na vitu mingi harusi ilianza mambo mengi yalifanywa kuimba na mambo mengi kidogo nilihisi kwenda kujisaidia nikiwa kwenye choo nilisikia wanaume wawili wakiambiana kwamba lazima waibe zawadi zote halafu wamwagilie hema mafuta halafu wachome hema zote pamoja na watu. Niliposikia hivyo nilikuwa nimestuka sana pia nikaacha kujisaidia kwenye choo niligoja waende kidogo nilitoka mbio kwenye choo kama risasi kwa sababu walikuwa wameenda kuendea

SIKU YA KUKUMBUKWA MAISHANI MWANGU

Ilikuwa siku ya Jumatatu ambapo umati wa watu ulikuwa umekuja nyumbani kwetu kusherehekea ili kukumbuka maisha yangu apo awali nikiwa mchanga hadi nimefika kuwa mzee. Wazazi wangu na marafiki wenzake nilio walikuwa wamevalia sherehe hiyo. Moyo wangu ulikuwa umejawa na furaha tele. Vyakula vya aina mingi zilikuwa zimepikwa si mchele, si chapati, mbuzi, ugali, nyama, maharagwe na zingine mingi. Wengeni walianza kuingia kwa sherehe moja baada ya mwingine. Walikuwa wananisalimia kwa heshima kwa sababu nilikuwa kijana mwema na nimesaidia wanakijiji sana. Walikuwa wanashukuru kwa kuongoza maendeleo katika kijiji hicho na bila shaka nilikuwa nimetolea sana kuwasaidia.

Wazazi wangu walikuwa wanafurahia sana kwa kuona kijana wao alikuwa na tumbo njema. Pia bibi yangu na watoto wangu walikuwa na furaha tele. Hiyo siku watu walikuwa wananikubuka kwa vile nilikuwa mtu mzuri na kusaidia maskini. Katika kijiji nilikuwa najulikana kuwa tajiri na kuheshimika. Sherehe ilianza na watu wakuanza kusherehekea. Wimbo ilichezwa na wanakijiji wakuanza kusherehekea na kuimba. Wakati wa kukula vyakula ulifika umati wa watu walifurahia sana kwa vyakula vitamu vyenye zilikuwa zimepikwa. Walinikubuka kwa furaha sana huku wakiomba Mwenyezi Mungu kunisaidia maishani mwangu. Umati wa watu ulisema kuwa nilikuwa kijana mwema, msaidia watu, muombaji mwenyezi mungu lakini sikuwa mchoyo, mkaidi, mtundu au mharibifu. Watu kijijini walikuja na zawadi tele ili kurudisha shukrani kwa vile nilivyosaidia kijiji hicho si watoto, wamama, wazee, vijana au wababa walikuja na zawadi ili kunishukuru. Nilishukuru Mungu kwa kunisaidia maishani mwangu na nikuwa tajiri. Nilimshukuru Mungu na kumuambia abariki hata wanakijiji. Wanakijiji walikuwa na furaha tele kwa mtu

**Kiambatisho 3: Idhini kutoka idara ya maadili ya utafiti**

# Mount Kenya University

REF: **MKU/ISERC/4691** Date: 20 January 2025

TO: **JULIET ASWANI MUKHWANA**

REG: **MAKI/2023/47525**

Dear Sir/Madam,

**RE: MAKOSA YA KIMOFOFONOLOJIA KATIKA KAZI ANDISHI ZA KISWAHILI MIONGONI MWA WANAFUNZI WENYE ASILI YA LUGHA YA KIKIKUYU KATIKA SHULE ZA UPILI: KAHURO, MURANG'A**

This is to inform you that **Mount Kenya University** has reviewed and approved your above research proposal. Your application approval number is **3413.** The approval period is **20/01/2025 - 19/01/2026.**

This approval is subject to compliance with the following requirements:

i. Only approved documents including informed consents, study instruments, MTA will be used
ii. All changes including amendments, deviations and violations are submitted for review and approval by **Mount Kenya University**
iii. Death and life-threatening problems and serious adverse events or unexpected adverse events whether related or unrelated to the study must be reported to **Mount Kenya University** within 72 hours of notification
iv. Any changes, anticipated or otherwise that may increase the risks or affect the safety or welfare of study participants and others or affect the integrity of the research must be reported to **Mount Kenya University** within 72 hours
v. Clearance for export of biological specimens must be obtained from relevant institutions
vi. Submission of a request for renewal of approval at least 60 days prior to expiry of the approval period. Attach a comprehensive progress report to support the renewal
vii. Submission of an executive summary report within 90 days upon completion of the study to **Mount Kenya University**

Prior to commencing your study, you will be expected to obtain a research license from National Commission for Science, Technology and Innovation (NACOSTI) https://research-portal.nacosti.go.ke and also obtain other clearances needed.

Yours sincerely,

MOUNT KENYA UNIVERSITY
ETHICS REVIEW COMMITTEE
P. O. Box 342 - 01000,
THIKA

**Dr. Alfred Owino, PhD**
**Chairman, Mount Kenya University ISERC**

Main Campus, General Kago Road, P.O. Box 342-01000 Thika.
Tel: +254 20 287 8000, Cell: +254 709 153 000
Email: info@mku.ac.ke, Web: www.mku.ac.ke

**Kiambatisho 4: Idhini ya utambulisho**

# Mount Kenya University

## DIRECTORATE OF GRADUATE STUDIES

MAKI/2023/47525

20th January, 2024

*National Commission for Science Technology & Innovation (NACOSTI)*
*Off Waiyaki Way, Upper Kabete,*
*P.O Box 30623- 00100*
*NAIROBI, KENYA*

Dear Sir/Madam,

**RE: JULIET ASWANI MUKHWANA – REGISTRATION NO. MAKI/2023/47525**

The purpose of this letter is to introduce the above named student who is pursuing **Master of Arts in Kiswahili** in the Department of **Psychology, Languages and Humanities** in the School **of Social Sciences.**

The title of the research is **"Makosa ya Kimofofonolojia Katika Kazi Andishi za Kiswahili Miongoni Mwa Wanafunzi Wenye Asili ya Lugha ya Kikikuyu Katika Shule za Upili: Kahuro, Muranga."** It has been cleared by the University's Ethics Review Committee (Certificate attached) and now has to proceed to the field to collect data between **February, 2025 and April, 2025.**

Any assistance accorded to the student will be highly appreciated.

Thank you.

Mount Kenya University
P. O. Box 342 - 01000, THIKA
Office of the Director,
Graduate Studies

Dr. Samuel M. Karenga, Ph.D
Director, Graduate Studies
Enc.

Main Campus, General Kago Road, P.O. Box 342-01000 Thika.
Cell: +254 709 153 000 / +254 709 153 200

**Kiambatisho 5: Cheti cha idhini ya kufanya utafiti (NACOSTI)**



REPUBLIC OF KENYA

NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE,TECHNOLOGY & INNOVATION

Ref No: 401560

Date of Issue: 29/January/2025

RESEARCH LICENSE

This is to Certify that Miss.. Juliet Aswani Mukhwana of Mount Kenya University, has been licensed to conduct research as per the provision of the Science, Technology and Innovation Act, 2013 (Rev.2014) in Muranga on the topic: Makosa ya kimofofonolojia katika kazi andishi za Kiswahili miongoni mwa wanafunzi wenye asili ya lugha ya Kikikuyu katika shule za upili; Kahuro, Murang'a for the period ending : 29/January/2026.

License No: NACOSTI/P/25/415527

401560

Applicant Identification Number

Director General

NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE,TECHNOLOGY & INNOVATION

Verification QR Code

NOTE: This is a computer generated License. To verify the authenticity of this document, Scan the QR Code using QR scanner application.

See overleaf for conditions

**Kiambatisho 6: Fomu ya idhini ya kufanya utafiti**

**MAKOSA YA KIMOFOFONOLOJIA KATIKA KAZI ANDISHI ZA KISWAHILI MIONGONI MWA WANAFUNZI WENYE ASILI YA LUGHA YA KIKIKUYU KATIKA SHULE ZA UPILI: KAHURO, MURANG'A**

**IDHINI YANGU YA KUSHIRIKI KWENYE UTAFITI**

Mimi--------------------------------nakubali kushiriki kwa utafiti huu kwa hiari yangu. Naelewa kuwa hata nikifanya uamuzi wa kushiriki sasa, naweza kujitoa au kukataa kuandika insha yoyote bila hatua yoyote kuchukuliwa kwangu.

Naelewa kuwa ninaweza kuondoa idhibati ya kutumia data yangu niliyoshirikisha kwenye insha kwa muda wa wiki moja baada ya kuandika insha husika. Hayo yakitokea data niliyotoa itafutwa.

Nilipata nafasi ya kuelezwa kwa uwazi yote yanayohusiana na utafiti husika na pia nikauliza maswali palipohitajika.

Pia, naelewa kushiriki kwangu kunahitaji kuwepo kwangu binafsi muda wangu, siri zangu na kuandika kwa uwazi insha nitakayopewa.

Naelewa sitafaidika moja kwa moja na utafiti huu nitakaoshiriki.

Ninaelewa ujumbe wowote nitakaotoa kwenye utafiti huu utachukuliwa kuwa siri kubwa,

Ninaelewa pia kuwa, kwa vyovyote vile katika matokeo ya utafiti huu, jina langu halitatolewa wazi.

Ninaelewa kuwa niliyoyaandika wakati wa utafiti yanaweza kunukuliwa mbele ya bodi ya utafiti, kamati ya utahini ya chuo, kwenye miktadha ya uwasilishaji wa matokeo na kwa washikadau wowote.

Ninaelewa kuwa iwapo nitamfahamisha mtafiti kuwa maisha yangu au ya mtu mwingine kuhusiana na utafiti huu yamo hatarini wanaweza kuripoti kisa hiki kwa ofisi husika pakiwa na idhini yangu au hata bila idhini yangu.

Ninaelewa kuwa fomu za idhini nilizozitia saini yangu wakati wa ushiriki wangu zitahifadhiwa kwa siri katika ofisi zote kwa muda fulani uliowekwa hadi pale bodi ya utahini itakapodhibitisha kazi zote za utafiti wa mwanafunzi.

Ninaelewa kuwa data zote zinazonihusu na ambazo zitafutwa kutoka kwa rekodi za utafiti zitawekwa siri kwa muda wa miaka miwili baada ya mwanafunzi kuwa na vikao na bodi za utahini.

Naelewa kuwa chini ya sheria za uhuru wa binadamu ninaweza kufikia data nilizotoa wakati wa utafiti zikiwa kwenye ofisi au mtandao zilikohifadhiwa.

Ninaelewa kwamba nina uhuru wa kuwasiliana na yeyote aliyeshiriki kwenye utafiti ili kusaka uwazi wa jumbe zote nilizotoa wakati wa ushiriki wangu.

Jina la mtafiti: Juliet Aswani Mukhwana

S.L.P. 411,

Kangema.

0722113926

Barua pepe: aswanijuliet2014@gmail.com

**Warejelewa**

Jina la msimamizi: Dkt.Rose Kawira

Chuo kikuu cha Mount Kenya

S.L.P. 342-01000

Thika.

0723929526

Barua pepe: kkamwara@mku.ac.ke

Mount Kenya University

Chuo Kikuu cha Mount Kenya

S.L.P. 342-01000

Thika.

+254709153000

Barua pepe: info@mku.ac.ke

Saini ya mshiriki--------------------------Tarehe----------------------

Naamini kuwa mshiriki wa utafiti huu anapatiana idhini yake ya kushiriki katika utafiti.

Saini ya mtafiti------------------------Tarehe-----------------------

Mount Kenya University

**Kiambatisho 7: Ripoti ya Turntin**

turnitin Page 1 of 134 - Cover Page Submission ID trn:oid:::17268:92743108

## submission

My Files
My Files
University

### Document Details

Submission ID
trn:oid:::17268:92743108

Submission Date
Apr 24, 2025, 9:17 PM GMT+5:30

Download Date
Apr 24, 2025, 9:19 PM GMT+5:30

File Name
JULIET DARREL-1.doc

File Size
6.8 MB

118 Pages

24,950 Words

142,194 Characters

turnitin Page 1 of 134 - Cover Page Submission ID trn:oid:::17268:92743108

# 18% Overall Similarity

The combined total of all matches, including overlapping sources, for each database.

## Filtered from the Report

- Bibliography
- Quoted Text

## Top Sources

13% Internet sources
4% Publications
16% Submitted works (Student Papers)

## Integrity Flags

**0 Integrity Flags for Review**

No suspicious text manipulations found.

Our system's algorithms look deeply at a document for any inconsistencies that would set it apart from a normal submission. If we notice something strange, we flag it for you to review.

A Flag is not necessarily an indicator of a problem. However, we'd recommend you focus your attention there for further review.

### Kiambatisho 8: Ramani ya Kaunti ya Murang'a




**Asili: Bodi ya Bodii ya utalii nchini Kenya**

**Kiambatisho 9: Ramani ya Kaunti Ndogo ya Kahuro**




Asili: Shirika la ramani nchini Kenya, 2024

Mount Kenya